

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi – Tarehe 15 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 79

Kuongeza Vituo vya Afya Jimbo la Nkasi Kusini

MHE. VICENT P. MBOGO aliuliza:-

Jimbo la Nkasi Kusini lina Kata 11 na Kituo cha Afya kimoja pekee:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Vituo vya Afya hasa katika Tarafa ya Chala, Kate, Myula, Sintali na Ninde?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 hadi mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imejenga na kukarabati Vituo vya Afya vya Nkomolo na Kirando kwa gharama ya shillingi milioni 900. Aldha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetoea shillingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga shillingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na shillingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Vilevile, Serikali imetenga shillingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma matatu ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusogea zaidi huduma za afya kwa wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi inakamilisha utaratibu wa kuingia makubaliano ya utoaji wa huduma za afya (*service agreement*) na Kituo cha Afya cha Mzimwa kinachomilikiwa na Taasisi ya Kikatoliki Abei kwa ajili ya wananchi kupata huduma za afya ikiwemo upasuaji wa dharura ambapo wananchi kutoka Tarafa za Myula na Sintali ni mionganoni mwa watakaonufaika na mpango huo. Aidha, Halmashauri imetenga eneo katika Tarafa ya Chala kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya kupitia fedha za mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga na kupanua vituo vya kutolea huduma za afya katika Jimbo la Nkasi na nchini kote kwa awamu kwa kuwa shughuli hizi ni endelevu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri. Ukanda wa Ziwa Tanganyika akina mama wengi wanakufa kwa kutokupata huduma za afya, hasa upande wa *ambulance boat* kwa sababu kule miundombinu ya barabara hakuna, usafiri wao ni ndani ya maji na vijiji viro vingi sana ndani ya Ziwa Tanganyika ambavyo vinatumia usafiri wa boti. Ni lini Serikali itapeleka *ambulance boat* kwa ajili ya kuokoa akina mama wajawazito? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika mwambao ule wa Ziwa Tanganyika kuna changamoto ya usafiri pale ambapo tunapata dharura za wagonjwa na hususan akina mama wajawazito ambao wanahitaji kwenda kwenye vituo vya rufaa kwa ajili ya huduma za upasuaji. Serikali imeendelea kuweka mipango ya kuhakikisha kwamba maeneo hayo ambayo yana changamoto kubwa za usafiri, hasa *ambulance* kwa maana ya *ambulance boats*, tunaendelea kuangalia utaratibu mzuri zaidi wa kutenga fedha kadri zitakavyokuwa zinapatikana ili tuwezeshe ufanisi wa rufaa katika maeneo hayo ili tuendelee kuokoa maisha ya wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo kwamba suala hili kama Serikali tunalichukua, tutalifanyia kazina kuona namna bora zaidi ya kupata *ambulance boat* ili iweze kusaidia wananchi katika Jimbo la Nkasi Kusini. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Makete, hasa Kata za Ipepo na Ikuo, wana changamoto pia ya kituo cha afya. Kwa Ikuo wana majengo tayari wameshajenga kwa nguvu za wananchi lakini bado Serikali haijamalizia na Ipepo tayari wameshaandaa tofali kwa ajili ya kujenga kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itaongeza nguvu kuhakikisha kwamba majengo haya yanakamilika kwa ajili ya wananchi wangu wa Ipepo na Ikuo, hasa ikizingatiwa kwamba wana zaidi ya kilometra 20 kwenda kufuata huduma za afya na tayari wameshaonesha jitihada za kuweka nguvukazi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya Serikali kwa ajili ya wananchi wangu hao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza wananchi wa Kata za Ipepo na Ikuo katika Jimbo la Makete kwa kuonesha nguvu kubwa ya kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya afya na hatua nzuri ambayo wameifikia. Serikali imeendelea kusisitiza wananchi

kuchangia nguvu zao kuanza ujenzi wa miradi ya vituo vya afya na zahanati na Serikali kuchangia nguvu za wananchi katika umalizaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Festo Sanga kwamba katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuchangia nguvu za wananchi katika ukamilishaji wa maboma. Nimhakikishie kwamba katika maeneo ambayo tutawapa kipaumbele ni pamoja na Kata hizi za Ipepo na Ikuo ili wananchi waweze kupata nguvu ya Serikali kukamilisha vituo hivyo vya afya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, swali la nyongeza.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa Jimbo la Nkasi Kusini, hali ni hiyohiyo ama mbaya zaidi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ambapo tuna kata 37 na vituo viwili tu vya afya. Sasa swali langu, Serikali ina mpango wowote wa kuongeza vituo vya afya Wilayani Muheza ili kusogezwa huduma za afya karibu na wananchi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Muheza lina kata 37 na vituo vya afya viwili tu na hali hii ipo katika karibu majimbo yote nchini. Tunafahamu tuna kata zaidi ya 3,900 na ndiyo maana Serikali imeweka mpango wa kujenga vituo vya afya kwa awamu. Ni kweli kwamba

hatuwezi kukamilisha kujenga vituo katika kata zote ndani ya mwaka mmoja wa fedha, lakini Serikali imedhamiria na inatambua kwamba tuna kazi ya kufanya kwa awamu kwa kadri ya fedha zinavyopatikana na kuendelea kujenga vituo vya afya katika kata zetu na kujenga zahanati katika vijiji na hospitali za halmashauri katika ngazi za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwinjuma kwamba katika mipango ya Serikali inayokuja, tutaendelea kuomba kuidhinishiwa fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga vituo vya afya katika kata nchini kote zikiwemo kata katika katika Jimbo hili la Muheza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Changamoto iliyopo Nkasi ndiyo changamoto iliyopo Kyerwa. Kyerwa tuna kata 24 lakini vituo vya afya vinavyotoa huduma ni viwili na kipo Kituo cha Afya Nkwenda ambacho jengo la mama na mtoto halijakamilika. Lini Serikali itakamilisha kituo hiki ili kiweze kutoa huduma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kutoa ufanuzi, kwamba dhamira na malengo ya Serikali na katika mipango yote ambayo Serikali inaandaa, ni pamoja na kuhakikisha inachangia nguvu za wananchi katika kukamilisha maboma ya zahanati, vituo vya afya na kupanua hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo hili la Kyerwa ambapo kuna vituo vya afya viwili na Kituo cha Afya cha Nkwenda ambacho kimeshajengewa jengo la *RCH* na halijakamilika, ni miongoni mwa vituo ambavyo vitaendelea kupewa kipaumbele katika bajeti za Serikali ili viweze kukamilishwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba katika mwaka ujao wa fedha, Mheshimiwa Waziri akija kuwasilisha bajeti hapa, tuna vituo takribani 121 ambavyo tunataraja kwenda kujenga kwa fedha za Serikali Kuu na fedha za mapato ya ndani ya halmashauri. Kwa hiyo kwa kuititia mpango huo tutaendelea kusogezza zaidi huduma ikiwemo katika Jimbo hili la Kyerwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Hitaji la Vifaa Tiba Kituo cha Afya
Mwabayanda – Maswa**

MHE. ESTHER L. MIDIMU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ununuzi wa Vifaa Tiba ikiwemo vya upasauaji katika Kituo cha Afya cha Mwabayanda Wilayani Maswa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kituo cha Afya Mwabayanda kilipatiwa shilingi milioni 400 kwa ajili ya upanuzi kwa kuwa awali ilikuwa ni zahanati. Ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya Mwabayanda umekamilika na kituo kimeanza kutoa huduma za dharura za upasuaji kwa akina mama wajawazito kuanzia mwezi Oktoba 2020 baada ya kupatiwa vifaa tiba kutoka kwenye vituo vingine vilivyojengwa katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imetoa shilingi bilioni 26 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya afya vilivyojengwa awamu ya kwanza na ya pili na vifaa vya shilingi bilioni 15 tayari vimeshapokelewa na taratibu za kupeleka vifaa vya shilingi bilioni 11 zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Mwabayanda kilijengwa katika awamu ya nne; na hivyo vituo vyote vya afya vilivyojengwa awamu ya tatu na ya nne vitatengewa fedha ya ununuzi wa vifaa tiba katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Aidha, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kuititia mapato yake ya ndani itoe kipaumbele cha ununuzi wa vifaa tiba kwa awamu ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha za ununuzi wa vifaa tiba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, swalii nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swalii la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza, naomba nipipongeze Serikali kwa kuongeza bajeti ya madawa na vifaa tiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Mwabayanda jengo la kuhifadhi maiti liko tayari lakini halina friji, je, ni lini Serikali itapeleka friji ya kuhifadhia maiti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa hospitali na vituo vya afya vya Mkoa wa Simiyu tuna upungufu wa madawa; je, Serikali imejipangaje kutupelekea madawa za kutosha kwenye hospitali na vituo vyetu vya afya? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napokea pongezi zake kwa Serikali kwamba imetenga fedha kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na shilingi bilioni 30 mwaka 2015 mpaka takribani shilingi bilioni 270, karibu mara tisa ndani ya miaka hii mitano. Hiyo ni dalili kwamba Serikali inathamini na imedhamiria kuhakikisha inaboresha upatikanaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba katika vituo vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jengo la *mortuary* kukamilika na kuhitaji jokofu, naomba nimueleze Mheshimiwa Mbunge Esther Lukago Midimu kwamba Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya huduma kama ambavyo tulifanya katika Kituo hiki cha Mwabayanda. Pia tumeelekeza watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa baada ya Serikali kupeleka fedha katika vituo hivyo na kukamilisha miundombinu, ni wajibu wao pia kupeleka sehemu ya fedha za maendeleo, ile asilimia 40 au 60 kwa ajili ya kununua baadhi ya vifaa tiba ili kuboresha huduma katika jamii zao. Kwa hiyo, ni muhimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Maswa aone namna bora pia ya kutenga fedha za kununua jokofu kwa ajili ya chumba cha kuhifadhi maiti katika jengo lile la Kituo cha Afya cha Mwabayanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na upungufu wa dawa; Serikali imeendelea kuboresha sana upatikanaji wa

dawa katika vituo vyetu kutoka asilimia 65 mwaka 2015 mpaka takribani asilimia 90-94 katika mwaka huu wa fedha. Lengo la Serikali, kwanza ni kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa kwa kuboresha makusanyo ya fedha za uchangiaji wa huduma za afya katika vituo vyetu. Pili ni kuendelea kupeleka fedha Bohari Kuu ya Dawa ili kuendelea kupata dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya afya katika Mkoa wa Simiyu na nchini kote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya dawa yanayojitokeza katika zahanati zetu ni sawa na yanayojitokeza katika Zahanati za Ipinda, Kyela na hata pale mijini. Ni mpaka lini tutasubiri tatizo hili liishe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha; kwanza bajeti ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba lakini pili, imeendelea kuboresha sana upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vyetu. Ni kweli pamoja na maboresho haya bado kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa katika baadhi ya vituo na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ambayo Serikali tumeyatoa, kwanza ni kuhakikisha watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatumia vizuri fedha zitokanazo na

uchangiaji wa huduma za afya kwa maana ya *cost sharing*. Tumejifunza kwamba baadhi ya halmashauri hazitumii vizuri fedha za *cost sharing* na tumewapa maelekezo kuhakikisha angalau asilimia 50 hadi 60 ya fedha za uchangiaji zinakwenda kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swalii la msingi, Serikali imeendelea kuongeza bajeti na itaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa kwa kuongeza bajeti na kusimamia matumizi bora ya dawa katika vituo vyetu. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kulifanyia kazi suala hilo. Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu sisi ni Madiwani katika mabaraza yetu kufuatilia kwa karibu matumizi ya dawa katika vituo vyetu na kuendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha makusanyo yanakuwa bora zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Butondo, swalii la nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kishapu na wananchi wa Kishapu kwa ujumla wameweza kujenga *health centers* tatu; *Health Center* za Dulisi, Mwigumbi na Mwang'halanga. Hata hivyo, *health centers* hizi zina upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba lakini pia lipo tatizo la upungufu mkubwa wa wafanyakazi (watumishi). Je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala zima la kutatua tatizo hili katika Wilaya ya Kishapu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa vituo vya afya vitatu, lakini kwa kuhakikisha kwamba vituo

hivyo vinaanza kutoa huduma ili kuweza kuboresha huduma za afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu katika swali la msingi, lakini katika maswali ya nyongeza yaliyofuata ni kwamba hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vyetu imeendelea kuimarika. Hata hivyo, tunafahamu bado kuna changamoto katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika kata hizi ambazo zipo katika Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu ambalo Serikali inaendelea kulitekeleza; moja, ni kuhakikisha tunaendelea kupeleka dawa katika vituo hivyo kutoka Bohari Kuu ya Dawa kwa wakati na kuendelea kuboresha bajeti ya dawa katika vituo hivyo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani na fedha zinazotoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Boniphace Butondo kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana kuhakikisha vituo hivi vinapata dawa na vitendanishi vyta kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baada ya ujenzi wa vituo vingi vya afya, *automatically* tunakuwa na upungufu wa watumishi. Hiyo ni hatua moja. Serikali imeanza na hatua ya ujenzi wa Vituo vya Afya, nasi sote ni mashahidi, tumejenga vituo vingi kwa wakati mmoja, lakini tunaendelea na hatua ya pili ya kuajiri watumishi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuomba kibali cha ajira na kadri watumishi watakavyopatikana, tutahakikisha tunawapeleka katika Vituo hivi vya Afya katika Jimbo la Kishapu na pia katika majimbo mengine kote nchini. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa ili niweze kuiliza swali dogo la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kutujengea Hospitali ya Nyang'wale ambayo imekamilika

kwa asilimia 90; lakini majengo hayo ambayo yamekamilika, anayatumia Mkurugenzi kama Ofisi zake na jengo la Halmashauri lipo kwenye asilimia 34:

Je, Serikali ipo tayari kuongeza fedha ili kukamilisha jengo la Halmashauri ili Mkurugenzi aweze kuhamia? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo haya ya Hospitali za Halmashauri ambayo yamekamilika kwa asilimia 90 na kuendelea, maelekezo ya Serikali ni kuhakikisha majengo yale yanaanza kutoa huduma za awali za afya katika Hospitali hizo za Halmashauri. Ndiyo maana katika hospitali zote 67 za awamu ya kwanza tayari huduma za awali za *OPD* zinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuelekeza kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Wilaya ya Nyang'wale ifanye utaratibu wa kuhakikisha huduma za afya katika hospitali hii iliyokamilika kwa asilimia 90 kwa wananchi, angalau kwa kuanza na huduma za *OPD*. Pili, Serikali katika mpango wa bajeti wa mwaka ujao itatenga zaidi ya shilingi bilioni 34 kwa ajili ya kukamilisha Hospitali zote za Halmashauri 67 ambazo zilianza ujenzi mwaka 2018/2019 ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Nyang'wale.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nawapongeza kwa jinsi ambavyo wameweza kutujengea vituo vya afya viwili; cha Buza

pamoja na Malawi na vyote vimemalizika katika Halmashauri yetu ya Temeke. Sasa nauliza:-

Je, vifaa tiba vitaingia lini; kwa sababu sasa ni muda mrefu hatujapata vifaa hivyo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vituo vya afya vikiwemo vya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke vimekamilika na kuna changamoto ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao tutakwenda kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha vituo hivi vya afya vinapelekewa vifaa tiba.

Katika swali langu la msingi nimesema, katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi billioni 26 zimeshatolewa tayari; na shilingi billioni 15 vifaa tiba vimeshapelekwa kwenye vituo vya afya vilivyojengwa kwenye awamu ya kwanza na ya pili; na shilingi billioni 11 zipo katika hatua za manunuzi kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Afya hivi vya Temeke vilijengwa awamu ya tatu na awamu ya nne, kwa hiyo, vitakuwa katika mpango wa bajeti wa mwaka 2021/2022. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo litaendelea kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 81

Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee

MHE. GHATI Z. CHOMETE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee wenyewe umri kuanzia miaka 60 katika Halmashauri za Mkoa wa Mara inatekelezeka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, inayoelekeza kutoa matibabu bila malipo kwa wazee wenyewe umri wa miaka 60 na kuendelea wasio na uwezo kwa kuwatambua na kuwapatia huduma mbalimbali za afya. Hadi Desemba, 2020 jumla ya wazee 2,344,747 wametambuliwa sawa na asimilia ya 87 ya makadirio ya wazee wote nchini. Kati yao wanaume ni 1,092,310 na wanawake 1,252,437. Aidha, wazee wasiokuwa na uwezo 1,087,008 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bure na wazee 856,052 wamepatiwa kadi za matibabu ya Afya ya Jamii (*ICHF*).

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2021 Halmashauri za Mkoa wa Mara zimefanya utambuzi wa wazee 70,170 kati ya lengo la kuwatambua wazee 196,000. Kati ya wazee walitambuliwa, wanaume ni 32,900 na wanawake ni 37,270. Wazee 39,664 wamepewa vitambulisho vya matibabu kati ya wazee 70,170 walitambuliwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoaa wa Mara na Mikoa mingine inaendelea kufanya utambuzi kwa wazee na kuhakikisha wazee wote wanaotambuliwa wanapewa vitambulisho vya matibabu bila malipo. Aidha, Serikali itaendelea kuwatambua wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea wasio na uwezo ili waweze kunufaika na Sera ya Matibabu Bila Malipo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, swali la nyongeza.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na Sera ya Matibabu Bure kuendelea kutekelezeka, lakini bado kuna wazee wengi hawajapatiwa vitambulisho hivyo vya kuwawezesha kupata matibabu hayo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wazee wote wenye sifa wanapata vitambulisho hivyo ili waweze kunufaika na Sera ya Matibabu Bure? (*Makof!*)

(b) Kuna malalamiko hata kwa wale wazee wachache wenye vitambulisho hivyo; wanapofika hospitalini wanaambiwa hakuna dawa: Je, ni lini Serikali itahakikisha ukosefu wa madawa huu unakwisha ili kuwaondolea wazee wetu kero hiyo? Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Sera ya Wazee inatambua kwamba tunahitaji kuainisha wazee wote wenye umri wa miaka 60 na kuendelea wasio na uwezo ili waweze kupata matibabu bila malipo. Serikali imeendelea kuweka utaratibu kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauti zetu kupita katika vijiji kwa kushirikiana

na Watendaji katika Vijiji na Kata kuwatambua wazee hao wenyе sifa, lakini pia kuhakikisha wanapata vitambulisho kwa ajili ya matibabu bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba bado hatujafikia asilimia 100 kama ambavyo nimejibu kwenye swalı la msingi, lakini jiithada za kuhakikisha tunafikia hapo zinaendea. Naomba nichukue nafasi hii kuwaelekeza Watendaji Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mitaa wote kote nchi kuhakikisha wanaweka mpango kazi wa kuwatambua wazee wote wenyе umri wa miaka 60 na kuendelea, wasio na uwezo na kuweka mipango ya kuwapatia vitambulisho ili waweze kupata matibabu bila malipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni endelevu, haliwezi kwisha kwa sababu kila siku kuna mtu anafikisha miaka 60. Kwa hiyo, hatuwezi kusema tumemaliza wazee wote, kwa sababu ni suala endelevu, kila mwaka kuna watu ambao *wata-turn* miaka 60 na Serikali itaendelea kuwatafutia vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika vituo vyetu kumekuwa kuna malalamiko kwa baadhi ya vituo na baadhi ya Halmashauri kwamba wazee wetu wakifika kwa ajili ya matibabu pamoja na vitambulisho vyao, wanakosa baadhi ya dawa muhimu. Kuna sababu mbili; sababu ya kwanza ni kwamba magonjwa mengi ambayo yanawapata wazee wa miaka 60 na kuendelea mara nyingi baadhi ya dawa zao hazipatikani katika ngazi ya vituo. Kwa hiyo, mara nyingine kunakuwa na changamoto ya magonjwa yale kwa ajili ya *advanced cases*, lakini wanahitaji kupata labda kwenye ngazi ya wilaya na ngazi ya rufaa, wakienda kwenye vituo vyetu mara nyingine hawapati zile dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka utaratibu wa kuendelea kwanza kuwaelimisha wananchi hao, lakini pia kuweka utaratibu wa kuona namna gani zile dawa muhimu katika maeneo husika zitapatikana ili kuwarahisishia wazee wetu kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili ni ile ambayo nimeelezea kwa ujumla wake kwamba Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba katika vituo vyetu kote nchini ili kuhakikisha wazee wetu na wananchi kwa ujumla wanapata dawa kama ambavyo imekusudiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro swali la nyongeza.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Changamoto iliyopo Mara ya wazee kutokutibowi bure ipo kwenye Jimbo la Ngara ambapo hata wale wazee waliokuwa na vitambulisho walinyang'anywa walipofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kufika kwenye Jimbo la Ngara kushuhudia namna ambavyo Sera ya Matibabu Bure haitekelezwi kwa hao wazee na kutoa muafaka wa namna nzuri ya hao wazee kupata huduma za matibabu bure? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Matibabu Bila Malipo kwa Eazee inahusika katika mamlaka zote nchini kote, ikiwepo Halmashauri ya Ngara. Kwa hiyo, naomba kwanza nipokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Jimbo la Ngara kuna baadhi ya wazee wenye vitambulisho walinyang'anywa. Suala hilo halikubaliki na wala siYo maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngara na Mamlaka za Serikali za Mitaa za Ngara kuhakikisha wanalfanya kazi suala hili mapema. Serikali inaelekeza kutoa

vitambulisho nya matibabu kwa wananchi, wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea wasio na uwezo. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kunyang'anya vitambulisho vile kwa sababu ni kuwanyima haki wazee hao ambaao sera inawatambua kwamba wanahitaji kupata vitambulisho hivyo kwa ajili ya matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kulitekeleza hilo, lakini kabla sijaenda, lazima Halmashauri ya Ngara itekeleze maelekezo haya ya Serikali kuhakikisha inaendelea kutoa vitambulisho kwa wazee na hakuna ruksa ya kumnyang'anya mzee yejote kitambulisho kwa ajili ya matibabu. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu tuna *machine ya X-Ray* tuliletewa toka mwaka 2002. Swali langu ni hili, katika hospitali hiyo hatuna mtaalam wa *X-Ray*:

Je, ni lini Serikali italeta mtaalam wa *X-Ray* katika Wilaya hiyo? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkta. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu wana mashine ya *X-Ray* ambayo kwa kipindi kirefu imekosa mtumishi kwa maana ya mtalaam wa *X-Ray*. Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeendelea kuwasiliana kwa karibu na Wizara ya Afya, lakini pia na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuona namna gani tunapata watumishi hawa ili tuweze kupata mtumishi mmoja na kumhamishia katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Wataalam hawa bado ni wachache lakini jitihada za Serikali ni kuendelea kuwasomesha ili tuweze kupata wataalam wengi ili waendane na kasi ya ujenzi wa

vituo vya afya ambavyo kimsingi vitahitaji kupata watalaam hawa wa *X-Ray*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshalifanyia kazi na tulishaainisha mtumishi kwa ajili ya kumpeleka Meatu na wakati wowote atakwenda kuanza kutoa huduma ya *X-Ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kikoyo swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na nia njema ya Serikali yetu kutoa tiba bure kwa wazee wetu, lakini zoezi zima limegubikwa na ukiritimba wa kutoa tiba kwa wazee wetu.

Je, Serikali haioni busara kuoanisha vitambulisho hivi vinavyotolewa kwa wazee na Bima ya Afya ili wazee wetu wapate tiba stahiki? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme, Serikali imeendelea kuhakikisha inapunguza changamoto ambazo Mheshimiwa anaziita ukiritimba wa Matibabu kwa Wazee Bila Malipo na ndiyo maana tumeainisha utaratibu wa kuainisha, kuwatambua wazee wetu na kuwapa vitambulisho. Hiyo ni sehemu ya jitihada ya Serikali kuhakikisha ule ukiritimba unapungua na kuwawezesha wazee wetu kupata matibabu bila malipo na bila changamoto yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupokea wazo lake la kuanganisha vitambulisho pamoja na sehemu ya matibabu kwa wazee ili Serikali iweze kulifanyia tathmini na

kuona uwezekano wa kufanya hivyo au uwezekano wa kuendelea kuboresha utaratibu uliopo ili tuweze kuboresha huduma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bahati Ndingo, aah! Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nilitaka kuongeza kwenye swalii la Dkt. Kikoyo kwenye suala la *ku-link* huduma za matibabu kwa wazee na Bima ya Afya. Jambo moja ambalo lilituchelewesha labda kuleta kwenye Bunge lako Muswada wa Bima ya Afya kwa wote ilikuwa ni kuweka utaratibu kama huo ambaao ukishafanya Bima ya Afya ni *compulsory*, maana yake lazima Serikali ije na utaratibu wa kuona ni jinsi gani Bima za Afya zitapatikana kwa watu hao kama wazee, akina mama wajawazito pamoja na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, swalii la Dkt. Kikoyo ni zuri. Pale ambapo Serikali italeta Muswaada wa Bima ya Afya, pia itaweka sasa utaratibu ambaao utaondoa hizi changamoto za matibabu bure kwa wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kwamba tukimaliza, nadhani tutakuwa tumepata mwarobaini wa tatizo hili. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Ndingo, swalii la nyongeza.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tunatambua kwamba Serikali ina vituo takribani 16 nchi nzima vya kulelea wazee wetu, lakini huduma za afya zinazopatikana ndani ya vituo vile kwa kweli ni kama huduma ya kwanza tu:-

Je, Serikai haioni kuna haja ya kuweka huduma bora ndani ya vituo vya kulelea wazee wetu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, majengo au nyumba za kulelea wazee wetu zilizopo kote nchini zinaendelea kupewa huduma za muhimu kwa kutumia taasisi mbalimbali ikiwepo Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuwezesha wazee wetu kuishi katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la huduma za afya katika maeneo hayo, kumekuwa na utaratibu wa karibu wa uratibu kati ya Maafisa Ustawi wa Jamii na Watoa Huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufika katika maeneo hayo, lakini pia kuweza kuchunguza afya za wazee wetu na kuwapatia matibabu pale inapobidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu tutaendelea kuuimarisha kuona namna gani wataalam katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanaweka utaratibu wa mara kwa mara wa kuwatemeala wazee wetu katika maeneo hayo wanayoishi na kutambua wale wenye dalili za kuhitaji matibabu waweze kupata matibabu kwa urahisi zaidi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 82

**Hitaji la Minara la Simu Kata la Masisiwe, Nyanzwa,
Irole na Ibumu - Kilolo**

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Masisiwe, Nyanzwa, Irole na Ibumu ambazo zina shida kubwa ya mawasiliano?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer Andrea Mathew Kundo*, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Serikali ya Awamu ya Sita, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Sambamba na hilo, naomba niwapongeze wanawake wote wa Tanzania, kwa sababu wameendelea kuonesha mfano wa kuigwa, tukishuhudia katika Awamu ya Nne, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Katika Awamu ya Tano, alikuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Makamu wa Rais na katika Awamu ya Sita, amekuwa mwanamke wa kwanza katika Nchi yetu ya Tanzania kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini kumsaidia katika nafasi ya Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kilolo lina Kata 24 ambapo Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) imeishakamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata tatu ambazo ni Lugalo ambapo ina mnara wa *Halotel*, Udekwa ambapo kuna mnara *Vodacom* na *Ukwega* ambapo kuna minara miwili ya *Tigo* na *Halotel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi za Serikali baadhi ya kata za jimbo hili zinachangamoto za upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kama vile Kata za Masisiwe, Nyanzwa, Ibumu na baadhi ya maeneo ya Kata ya Irole. Jiografia ya jimbo hili ni ya milima na miti mirefu ambapo kwa kiasi kikubwa sana inaathiri upatikanaji wa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Irole kuna baadhi ya maeneo yanapatikana huduma za mawasiliano kupitia mnara wa mawasiliano wa *HTT*, uliobeba watoa huduma watatu ambao ni *Airtel* ambayo inatoa teknolojia ya *2G*, *Vodacom* ambapo wanatoa teknolojia ya *2G* na *3G* na *Tigo* ambao wanatoa *2G* na *3G*. Pamoja na uwepo wa huduma za mawasiliano kutoka kwa watoa huduma nilotaja, bado kuna maeneo ndani ya Kata ya Irole yana changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) iliifanyia tathmini Kata ya Ibumu na hatimaye kukijumuisha Kijiji cha Ilambo katika zabuni ya awamu ya tano ya mradi wa kufikisha mawasiliano mipakani na kanda maalum. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) ambapo mikataba ya utekelezaji wa mradi huo ilitiwa saini tarehe 6 Julai, 2020. Mradi huu utakapokamilika utaweza kuhudumia Vijiji vya Ibumu, Kilala, Kidewa, Ilambo na Kilumbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *UCSAF* itavifanyia tathmini vijiji vya Kata za Masisiwe, Nyanzwa na baadhi ya vijiji vya Kata ya Irole ambavyo huduma ya mawasiliano imekuwa changamoto kwa kiasi kikubwa sana. Huduma inatolewa na mnara wa *HTT* uliopo na hatimaye vijiji husika vitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Justine L. Nyamoga, swalilala nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri ambayo yanatoa matumaini kwenye maeneo yale ambayo kumewekwa ahadi za kuweka minara. Hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Kata ya Masisiwe na Kata ya Udekwa hakuna mawasiliano kabisa na tayari watu wawili wameanguka kutoka kwenye miti wakijaribu kutafuta mtandao na kuumia na kulazwa katika Hospitali ya Ilula mmoja na ya Kilolo mmoja.

Sasa, je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi katika kata hizi, kwanza ili kutoa pole kwa watu hao, lakini pili ili kuweza kuona yeye mwenyewe na nafahamu yeye ni mtu ambaye ametembelea maeneo mengi ili aweze kujiona hali halisi na kuweka msisitizo wa kuweka minara katika maeneo hayo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, maeneo yenye mitandao, yenye wananchi wenye matumiani makubwa sana yakutumia vifurushi vya bei ndogo, yalikatishwa tamaa na ongezeko la bei ya vifurushi ambapo ilitarajiwa vishuke. Tunaishukuru Serikali kwamba imerudisha katika ile hali ya kawaida, lakini matumaini ya wananchi ilikuwa ni kushushwa. Sasa je, ni lini Serikali itarudia ule mpango wake wa awali wa kushusha vifurushi, ili Watanzania wakiwemo wananchi wa Kilolo amba wanataka sana kutumia vifurushi hivi katika shughuli zao za kibashara, waweze kufurahia bei nafuu ya vifurushi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maswali yangu hayo mawili madogo yajibiiwe.

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Engineer Andrea M. Kundo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Justin Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, nimesema kwamba Serikali tayari imeshaanza kufanya tathmini katika Kata ya Irole pamoja na Masisiwe ili tuweze kuingiza katika mpango wa awamu ya tano na ya sita katika mwaka wa fedha wa 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala la pili, nafahamu kabisa hili ni swali ambalo Waheshimiwa Wabunge wote wangeweza kuliuliza. Naweza kusema kwamba kazi ya Serikali ya kwanza ni kuhakikisha kwamba *in-stabilize* bei iliyopo na hilo ndilo ambalo tumelifanya kwa sasa. Naona kwamba kulikuwa na changamoto ambapo makampuni yaliweza kuwa na bei tofauti tofauti ambazo ziliwaumiza sana wananchi, lakini Serikali ikatoa maelekezo ya kuhakikisha kwamba bei ya hapo awali inarejea kama ambavyo Watanzania walikuwa wanakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunafahamu kwamba, katika kurejesha hizi gharama za vifurushi, kuna changamoto yake. Kupandisha kifurushi ni mchakato ambao unahusisha ujenzi wa mifumo ambayo itawenza ku-*support* hicho kifurushi kipyा ambacho utakingiza sokoni. Vile vile unaposema kwamba urudishe maana yake kwamba unaanza kufanya *reverse engineering* maana yake unaanza kurudisha kwenye mfumo ule ulioko zamani, kama ulikuwa umeshautoa maana yake sasa inabidi uanze kuusuka tena ili uanze kutoa bei ambazo zilikuwa zinatolewa hapo kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge pia ameongelea namna gani Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba bei hizi, zinashuka zaidi ya sasa ambavyo Watanzania wangetarajia. Changamoto ya biashara ya mawasiliano, kitu ambacho tunakiangalia Serikali ni kwamba hapa tunatakiwa kuangalia tuna-*balance* namna gani kati ya *consumer*, watumiaji wa huduma, Serikali pamoja na mtoa huduma. Ni lazima tuangalie ile *production cost* yake, ni lazima aweze kufanya biashara katika kiwango ambacho anaweza akapata faida ili Serikali pia iendeleee kupata kodi lakini kodi hizohizo ziweze kurudi kujenga barabara na zahanati na hatimaye Wabunge katika Majimbo yao

wanayotoka tuweze kushuhudia kuna mabadiliko ya barabara na zahanati ambazo zitakuwa zinajengwa. Naomba kuwasilisha. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yustina A. Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza nafasi ya swali la nyongeza. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unalenga kupeleka mawasiliano katika maeneo yote ya nchi yetu. Je, ni lini sasa Mfuko utawezesha upatikanaji wa mawasiliano katika kata na maeneo yasiyo na mawasiliano katika Mkoa wa Manyara? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rahhi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote jukumu lake la msingi ni kuhakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano kwa Watanzania wote, hasa katika maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara. Maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara maana yake watoa huduma wengine hawatoweza kupeleka huduma hiyo kwa sababu wanaongozwa zaidi na *business plan* zao, *business case* zao na ndio maana kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, sasa Serikali inafanya tathmini katika maeneo yote ambayo yana changamoto ya mawasiliano katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie kwamba, tumeshaanza kufanya tathmini mipakani pamoja na maeneo maalum ambayo yalikuwa na changamoto kubwa sana ambapo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika mara kwa mara, lakini mpaka sasa tathmini hiyo imeshakamilika. Kuanzia mwaka huu wa fedha, tayari

tunatarajia kuanza kutangaza zabuni kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo. Nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuen A. Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia swali la nyongeza. Changamoto iliyoko Jimbo la Kilolo ni sawa na changamoto iliyoko katika Hifadhi ya Same ambayo katika hifadhi hiyo barabara kuu inapita kuelekea katika Jimbo la Same Mashariki. Katikati ya Hifadhi hiyo, hakuna mawasiliano ya simu, jambo ambalo linapelekea vijana wengi kwenda kufanya mambo ya kiukorofi, kuteka baadhi ya magari na kuwapora wananchi mali zao. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha kwamba inajenga minara ya simu maeneo hayo ili endapo ukorofiki kama huo vijana wataufanya, waweze kutoa mawasiliano kwa ajili ya kutetea haki yao? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Zuen Bushiri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari ina mpango wa kuhakikisha kwamba tunapeleka mawasiliano katika maeneo ya mbuga na hifadhi ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yasiwe na changamoto tena kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Pamoja na kwamba kuna changamoto ya mitandao kuititia maeneo mbalimbali ya Tanzania, lakini halikadhalika kuna changamoto pia ya wizi wa kimitandao,

tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana kupitia hii mitandao. Swali langu, je,ni lini Serikali itaweza kudhibiti wizi huu wa kimtandao unafanywa na simu? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna Mbunge hajazima *microphone*.

Angalieni *microphones* zenu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utapeli wa kimtandao viko chini ya makosa ya kimtandao na Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015. Hata hivyo watekelezaji wa sheria hii ni pamoja na vyombo vingine vyatya dola, ikiwemo na Jeshi la Polishi. Tunafanya juhudzi za kutosha kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa umma, kwa sababu ndicho kitu ambacho ni cha msingi sana kwa Watanzania kuelewa namna gani wanawea wakatumia simu zao za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia changamoto ambayo ilikuwepo ni pamoja na wale waliokuwa wanapewa majukumu ya kuandikisha au kuuza zile *lines* za simu, ambao walionekana kutokuwa na uaminifu na hatimaye kuwa wanawatapeli Watanzania badala ya kusajili *line* moja kwa mtaa mmoja, matokeo yake anajikuta kwamba Mtanzania amesajili *line* tano kabla ya kuondoka katika kituo cha kusajili *lines* hizo. Matokeo yake hizi *lines* zitakapochukuliwa na watu ambao wanania ovu matokeo yake ndio zitakuja kutumika kwa ajili ya matatizo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa umma lakini pia tunatumia teknolojia ambayo itaanza kudhibiti, matatizo ambayo yangesababishwa na watu ambao wamepewa

majukumu ya kuuza hizi *lines*. Namhakikisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine, Serikali bado inayafanya kazi na kufanya uchambuzi wa kutosha ili kujiridhisha kwamba tunatumia njia gani ambayo itakuwa rafiki zaidi kwa Watanzania bila kuwabugudhi katika maisha yao ya kila siku. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Changamoto ya mawasiliano iliyopo katika Jimbo la Kilolo inafanana kabisa na changamoto ya mawasiliano ambayo tunayo katika Jimbo la Handeni Mjini, hasa maeneo ya Kwa Magome, Malezi, Mlimani, Konje, Kwediyamba, Kwenjugo, Msasa, Kideleko na Mabanda. Je, ni lini, Serikali itapeleka mawasiliano katika maeneo hayo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema Serikali inabidi ifanye tathmini, ni kwa sababu tumekuwa na uelewa ambao unatofautiana kidogo. Kuna maeneo ambayo tayari unakuta kwamba kuna mnara mmoja, kuna minara miwili, lakini wananchi wetu wanatamani kuona kila kijiji kina minara mitatu au minne. Kazi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuititia Serikali yetu, ni kuhakikisha pale ambapo hakuna kabisa mawasiliano na ndipo Serikali inapokwenda kufikisha mawasiliano kwa wananchi. Ndio maana tunasisitiza sana, Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafika katika maeneo husika na kufanya tathmini na kujiridhisha kama tatizo ni kwamba hakuna mawasiliano ama mawasiliano yaliyopo hayana ubora unaotakiwa na kama hayana ubora

unaotakiwa basi tutaelekeza *TCRA* kuhakikisha kwamba inawawajibisha watoa huduma katika maeneo husika kulilingana na makubaliano ya utoaji wa huduma nchini. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho la Wizara ya Maji. Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum. Swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 83

Uvunaji wa Maji ya Mvua

MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA aliuliza:-

Kijographia Tanzania ipo kwenye ukanda wenyewe mvua za kutosha:-

Je, Serikali imejizatiti vipi kuhamasisha zoezi la uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca W. Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Nchi yetu ipo kwenye ukanda wa mvua za kutosha, hivyo ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ni muhimu kwa kuwa itawezesha kuwa na maji ya uhakika kwa kipindi chote cha mwaka bila kujali hali ya hewa. Vilevile, miundombinu hiyo ni muhimu kwa kuwa itawezesha kudhibiti mafuriko na pia kuokoa miundombinu, ikiwemo ya kuhudumia maji pamoja na mali na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza azma hiyo mkakati mwingine ni Wizara ya Maji kukutana na *TAMISEMI* kwa lengo la kuhusisha mashule, kujenga *gats* za maji na matenki, pia kuhamasisha wananchi wanapojenga nyumba zao waweke miundombinu rafiki ya kukusanya maji, lengo zoezi liwe shirikishi. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa ukarabati wa mabwawa kwa kila wilaya, hususan katika wilaya kame.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 Wizara imekamilisha ukarabati wa mabwawa ya Mwadila lilioko Wilaya ya Maswa Mkoa wa Simiyu, usanifu kwa ajili ya kukarabati mabwawa matatu ya Itobo lilioko Wilaya ya Nzega, Ingekument lilioko Wilaya ya Monduli na Horohoro lilioko Wilaya ya Mkinga na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa mawili ya Muko na Chiwanda yaliyoko Wilaya ya Mombasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, usanifu wa Malambo ya kunyweshea mifugo sita, umekamilika katika mwambao wa barabara kuu ya Dodoma Babati, ikihusisha Wilaya ya Bahi malambo mawili na Chemba malambo manne. Vile vile, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga mabwawa ya kimkakati ya Kidunda Mto Ruvu, Falkwa katika Mto Bubu na Ndembela Lugoda katika Mto Ndembela.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo kwa kweli yanatia Faraja, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika llani ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 150 lbara ya 100 imeweka bayana kwamba, tunataka tupeleke maji vijiji kwa asilimia 85 lakini mijini kwa asilimia 95. Na kinachoonekana hapa kinakosekana ni elimu kwa wananchi, je. Wizara iko tayari sasa kuja na mpango Madhubuti wa kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili wawe na utaratibu huu mzuri wa kuvuna maji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, maji yanapotiririka yanaharibu miundombinu kwa kiasi kikubwa na mara nyingi ni miundombinu ya barabara, reli lakini pia wakati mwингine na mabwawa na *scheme* za umwagiliaji. Na kwa mfano, katika eneo la Kongwa mara kadhaa tumeona kwamba, barabara inasombwa na maji lakini pia, kule katika Mto Mkondoaa eneo la Kilosa, reli mara kadhaa inasombwa na maji. Sasa kwa nini Serikali isije na mkakati mahsuswi wa kuhakikisha kwamba, tunakuwa si tu, na mabwawa machache lakini tutafute mabwawa mengi nchi nzima ambayo yatakuwa yanazuia maji ambapo maji haya yatatumika kwa matumizi ya kunywa lakini pia, kwa ajili ya matumizi ya kilimo? Ahsante. (*Makoff*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli llani inatutaka kufika mwaka 2025 vijijiini kote maji yawe yamefika kwa asilimia 85 na maeneo ya Miji kwa asilimia 95. Wizara inaendelea kutekeleza llani kwa ufasaha sana na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Maji ni kwamba, maji haya ya mvua kwetu sisi tunayachukulia kuwa ni fursa na sio laana. Hivyo, nipende kumwambia Mheshimiwa Shangazi kwa umahiri alionao, Wabunge wote humu ndani tunafahamu umahiri wa Mheshimiwa Shangazi vile ni Mwenyekiti wa Simba *Sports Club* humu Bungeni. Lakini vile vile, ni Katibu wetu sisi Wabunge tunaotokana na Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninafahamu tutaendelea kushirikiana lakini Wizara tutaendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi namna bora ya uvunaji wa maji katika makazi yetu na kama Wizara ya Maji, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya *TAMISEMI*, ili tuweze kuunganisha nguvu ya pamoja kuona wananchi tunawapa elimu, namna bora ya kufanya *design*, namna pale wanapojenga makazi yao. Kwasababu, mvua hizi tukiweza kufanya ni zoezi la shirikishi, maji yatakuwa ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata kwenye mashule yetu kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi tutahakikisha na wao tunaendelea kutoa elimu kwa wakuu wa shule, ili kuona hata kwenye mashule yetu, watoto wasiendelee kuteseka. Maji hayana sababu ya kwenda kuharibu miundombinu mingine ambayo tunahitaji katika maisha yetu ya kila siku na maji haya tuweze kwenda kuyatumia vyema. Lakini vile vile, tutaendelea kuona namna bora ya kupata matenki ya bei nafuu kwa maeneo ya vijiji, illi ikiwezekana basi maji haya yaweze yakavuliwa kwa ushiriki wa pamoja na isije ikapelekea tena kuwa ni gharama kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika swalı lake la pili, kama Wizara nipende tu kusema nimepokea ushauri huu tutaendelea kuufanya kazi Mheshimiwa Shangazi tutaonana, illi tuweze kuendelea kushauriana vema na Wizara tutakwenda kutekeleza vema. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, swalı la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, katika Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha kuna mradi mkubwa wa maji wa vijiji (8) maarufu kama Mradi wa Magehe, mradi huu unagharimu bilioni 8, upembuzi yakinifu umeshafanyika kilichobaki ni utekelezaji tu. Nilitaka kufahamu ni lini Serikali itatekeleza mradi huu mkubwa kwa wananchi wa Ngorongoro?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imezingatia mradi huu wa maji wa Magehe kwa umuhimu wake na tunaona kabisa ni mradi mkubwa ambao utakwenda kugharimu Serikali shilingi bilioni 8. Nikutoe hofu Mheshimiwa Catherine namna ambavyo umeweza ukafatilia suala hili muda mrefu na umekuwa ukiliuliza mara kwa mara

kwangu pamoja na kwa Mheshimiwa Waziri, tutatekeleza mradi huu kwa awamu katika mwaka wa fedha ujao.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Mbulu Vijiji liko juu ya Bonde la Ufa na vijiji vingi sana havina maji, ni kwasababu ya Bonde la Ufa. Na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, alifika wakati wa kampeni na kuahidi vijiji vile vitapata maji kutoka kwenye Ziwa la Madunga, Je. Mheshimiwa Waziri, lini ahadi ya Mheshimiwa Rais itatimizwa kwa wananchi hawa kupata maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge suala hili kama tulivyokubaliana, tunaliingiza kwenye mpango mkakati wetu wa mwaka wa fedha 2021/2022 na mradi huu utaaanza utekelezaji wake mara moja mara baada ya Mwaka wa Fedha mpya kuanza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwanza kabisa, nimshukuru Waziri na Naibu Waziri wake kwa namna ya kipekee kabisa, kwa namna ambavyo wanani pa ushirikiano. Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipokuja kwenye ziara ya kuomba kura, alisema atahakikisha anachagua Waziri ambaye anawaza nje ya *box* na hakika watu hawa wanafanya hivyo. Sasa swali langu, nawashukuruni pamoja na kunipa mabwawa manne, lakini nataka kujua sasa, ni lini ujenzi huo wa hayo mabwawa utaanza? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mabwawa haya manne yatajengwa kwa nyakati tofauti kulingana na fedha tutakavyokuwa tunazipata, ninaamini Mheshimiwa Mbunge wewe ni shahidi mzuri pale Chemba tumepatendea haki sana, hivi majuzi tu tumetoka kuchimba visima na hata haya mabwawa tunakuja kujenga mwaka ujao wa fedha lakini tutaanza kwa awamu taratibu mpaka kuhakikisha mabwawa yote yanakamilika. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa swali niulize swali dogo la nyongeza. Natambua Wizara imetupa mradi mkubwa wa maji kutoka Nkome kwenda Nzela Rwezela lakini nilitaka kuuliza swali dogo. Tunayo Kata ya Rubanga haina kabisa mfumo wa maji na kina mama wanatembea umbali wa kilometra 10 kupata maji katika Kijiji cha Mwamitilwa, Mtakuja, Ludenge, Je. Serikali haioni umuhimu wa kunipatia angalau visima viwili viwili katika vijiji hivyo vitano? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kata ya Rubanda, Serikali inafahamu umuhimu wa kuleta visima na kama nilivyoongea na wewe Mheshimiwa Musukuma, wewe ni Mbunge ambaye umefatilia suala hili kwa karibu, tayari tumekutengea visima viwili vyaa kuanzia katika mwaka wetu wa fedha ujao. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana, Waheshimiwa tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Niwakumbushe tu jambo moja kwasababu ndio tunaendelea na hili Bunge letu refu. Waheshimiwa Wabunge mnapoombaa maswali ya nyongeza muwe mmeiyatazama maswali ya

msingi ili Serikali iweze kuwajibu kikamilifu maswali mnayoyaauliza. Nitatoa mifano miwili, swali Na. 81 lilikuwa linahusu matibabu bure kwa wazee, watu wamesimama hapa wanaauliza vituo vya afya, watu wamesimama hapa wanaauliza hospitali. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge kimsingi nilipaswa kuwaambia hayo maswali hayana uhusiano na swali la nyongeza. Lakini nyie mnafahamu wananchi wenu kule wanatazama na sikutaka kuwakatisha, wananchi wenu wataona hamuulizi sawasawa ama hujasoma sawasawa swali. Kwa hiyo, soma swali la msingi ili la nyongeza liendane na swali la msingi, ili Serikali iweze kukujibu jibu ambalo ni kamili, jibu ambalo wananchi wako wataweza kuona kwamba kuna jambo linafanyika huko, la sivyo na wao wanajibu tu kwa kadri wewe ulivyouliza. Lakini sasa, tunawapa wakati mgumu. (*Makof*)

Swali la pili, ni Na. 83 swali hili linahusu uvunaji wa maji ya mvua. Watu hapo tumekuja na kila aina ya maswali ya nyongeza. Eeeh! Haya visima vya maji na mambo mengine mengi tu yameelezwa hapa. Sasa, hii ni mifano tu kwa hiyo, mtu unapopewa fursa ama unapoomba fursa ya kuuliza swali la nyongeza soma kwanza swali la msingi, kwasababu ndilo ambalo upande wa Serikali wanakuwa wamejiandaa kujibu kikamilifu. Ukitaka uvunaji, uliza uvunaji kuhusu Jimboni kwako wao watakujibu kikamilifu. Sasa ukileta habari nyiningine na wao watakujibu habari nyiningine halafu usipoona matokeo usiliaumu Serikali. Nadhani tumeshaelewana. Na sisi hapa mbele hatutaki kukukatisha kwamba, swali hilo halina uhusiano na swali la msingi. Kwasababu tutakuwa tunakusumbua kidogo kule Jimboni.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa ya Wabunge ambao wametembelewa na wageni. Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango na Mgeni huyu ni Ndg. Neema Nchemba kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye ni mke wake. Sijajua amekaa wapi? Aaah! Jamani sasa kama hawaja... Tilitaka tutangaze hapa kwamba Mheshimiwa Mwigulu

Nchemba ameoja jamani watu wasiwe wanasogea soga
kwenye kiti. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Ullega,
ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni
Viongozi wa Jumuiya ya Kuhifadhishe *Quran*Tanzania kutoka
Mkuranga Mkoani Pwani, wakiongozwa na Mwenyekiti wao
Sheikh Othman Karibuni sana, karibuni sana. Ally Kapor.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Ullega amewaiba hadi wa Dar es
Salaam sasa wanatoka Mkuranga hatari kabisa hii.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Sofia Mwakagenda,
ambao ni mtoto wake Ndg. Titus Mwakagenda na rafiki yake
Ndg. Samson Mushi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana,
karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi
Mwanaisha Ulenge, ambaye ni rafiki na mdau wa maendeleo
kutoka Tokyo nchini Japan Ndg. Miyo Sunoda. Na huyu sijui
amekaa wapi? Jamani waleta matangazo hapa mbele
muwe mnatutendea haki.

Wageni watano wa Mheshimiwa Kwagirwa
Nhamanilo ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Mji
Handeni Mkoani Tanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa
Halmashauri Ndg. Mussa Mkombati. Karibuni sana, karibuni
sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Amsabi Mrimi ambaye ni kaka
yake na Diwani Kata ya Mosongo Wilayani Serengeti Mkoani
Mara Ndg. Samson Mrimi. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Askofu
Josephat Gwajima, ambao ni rafiki zake kutoka jijini Dar es
Salaam na hawa ni Dkt. Peter Nyaga na Dkt. Elisha Muliri.
Karibuni Sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Naona Mheshimiwa Askofu Gwajima ametembelewa na Watumishi wenzake. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA
WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA
FEDHA 2021/2022**

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano na nimeshaletewa majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wangependa kuchangia siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Juliana Shonza, atafatiwa na Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam Mwagao, ajandae.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mama yetu kipenzi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kutupia jicho kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii, kwa kumteua Naibu Waziri ambaye kimsingi atawajibika moja kwa moja kwenye kusimamia Idara hii ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hayo kwasababu, ni Afisa Maendeleo wa Jamii kwa hiyo nisingekuwa Mbunge leo hii Juliana Shonza ningekuwa Afisa Maendeleo ya Jamii kwa hiyo, ninajua changamoto mbalimbali ambazo zinaikumba Idara hii. Ukiangalia chanzo cha kuanzishwa Idara ya Maendeleo ya Jamii, ni zile

changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza kipindi kile miaka 1750 kipindi ambacho kulitokea na mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi hayo ya viwanda yalipelekea changamoto mbalimbali kwenye jamii ikiwepo, ukosefu wa ajira, watoto wa mitaani, lakini vile vile, migomo pamoja na maandamano ndipo walipoamua wakaona kwamba sasa kuna umuhimu wa kuja na sekta au Idara ambayo moja kwa moja *ita-deal* na masuala ya jamii kwa maana ile mifumo mizima ya jamii ambayo inaletwa na mabadiliko mbalimbali kwenye jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema haya yote kwasababu, leo hii kwenye halmashauri zetu tunao maafisa maendeleo ya jamii lakini katika namna ya kushangaza na kusikitisha sana, maafisa maendeleo hawa hawafanyi majukumu yao ya kimsingi, ile dhana halisi ambayo ilipelekea kuanzishwa kwa Idara hii ya Maendeleo ya Jamii imeachwa na hatimaye sasa hivi, maafisa hawa wamegeuka kuwa maafisa mikopo. Kitu ambacho sio jukumu lao la kimsingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kwamba kwenye jamii yetu sasa hivi changamoto ziko nyingi. Kuna masuala ya ubakaji kwa watoto, ulawiti na hii imekuwa ni changamoto kubwa sana. Kesi nyingi sana ambazo zipo huko kwenye jamii zetu, nyingi zinalishia kule kule kwenye jamii, hazisikiki na haki inakuwa haitendeki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa Mheshimiwa Rose Tweve kuna siku alisimama hapa akazungumza kwa hisia sana kwamba kuna mtoto ambaye amebakwa na mzazi wake na mwisho wa siku akaambukizwa na UKIMWI, lakini kesi hiyo hajaenda popote, mzazi huyo yuko mtaani, anaendelea kudunda wakati mtoto huyu tayari *future* yake imeshaharibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu changamoto kama hizi ziko nyingi. Unaweza kujiuliza kwamba kesi kama hizi ziko ngapi kwenye jamii yetu? Hata hivyo, sisi kama Serikali

ni nani ambaye tumemweka kule chini ambaye moja kwa moja anawajibika kwenye kushughulikia hizi kero na changamoto na mifumo hii ya kijamii ambayo inaleta athari kwenye jamii yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala zima la mmomonyoko wa maadili, suala zima la miradi mikubwa ya maendeleo ambayo Serikali imekuwa inapeleka fedha nyingi sana kule chini kwenye jamii yetu; lakini mwisho wa siku miradi ile imekuwa haiendelei, inakuфа. Ukiangaliza chanzo ni nini? Ni kwa sababu jamii ile haijashirikishwa ipasavyo kuweza kuji-*engage* kwenye ule mradi ili waweze kuona kwamba nao ni sehemu ya ule mradi na kwamba Serikali imewaletea ule mradi siyo kwamba ni mradi wa Serikali peke yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo ni la msingi sana, nami nikaona kwa sababu sasa hivi tumepata Naibu Waziri wa kusimamia suala hili, ni vyema niweze kutoa maombi yangu kwamba jambo la msingi la kufanya kwa sasa hivi, cha kwanza kama akiona inafaa, Serikali iweze kuangalia ili tupitie upya ule mfumo wa upatikanaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii na majukumu yao. Warudi wakafanye kazi yao ya msingi kule kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, Serikali imekuja na Mpango mzuri sana na imetuahidi kwamba ikiwezekana ndani ya Bunge hili wataleta Muswada wa Bima ya Afya kwa wote. Muswada huo ni mzuri kwa sababu upo kwenye llani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ila swalii la msingi la kujiuliza ni je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba mradi huo unaweza kutekelezwa ipasavyo na ukaléta tija kama ambavyo Serikali imekusudia? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu suala la Bima la Afya kwa wote siyo suala la Serikali peke yake, maana yake ni Serikali pamoja na wananchi wote kwa pamoja tuna jukumu la kuchangia na kushiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba mradi huu, mkakati wa Serikali na sera

hiyo inaweza kutekelezwa ipasavyo na kuweza kuleta matunda ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la msingi ni kwamba tumejiandaa vipi? Kwa sababu hili ni suala la elimu. Tutoke kwenye ule mfumo wa kuanzisha miradi au mikakati au sera halafu tunawapa taarifa wananchi. Tuingie kwenye mfumo wa kuwaelimisha wananchi wafahamu umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu, tunaishi kwenye jamii ambayo ina misingi mbalimbali. Tunatofautiana masuala ya mila na desturi; na mapokeo juu ya mambo mbalimbali ya kijamii. Kwa mantiki hiyo, ni lazima tupate watu ambao wataenda kule chini kuelimisha jamii waone umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko dini ambazo mpaka sasa hivi wao hawaamini kabisa kuhusiana na suala la tiba za kisasa. Zipo jamii zetu ambazo zinaamini katika ugonjwa wowote, ni mtu amelogwa. Hizi ni changamoto zilizopo kwenye jamii yetu. Pia ziko jamii ambazo zinaamini sana kwenye mitishamba kuliko kwenda hospitali. Kwa hiyo, ukiangalia mabadiliko haya na suala zima la mfumo kwenye jamii; ili Serikali iweze kutekeleza azma yake hiyo ambayo ni njema sana kwa Watanzania, ni lazima tuwatumie Maafisa Maendeleo ya Jamii waende kule chini wakaelimishe jamii waweze kuona umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijikite kwenye kutoa ushauri wangu kwa Serikali. Kwanza napenda kuishauri Serikali ipitie upya mfumo mzima wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, warudi wakafanye kazi zao za kimsingi. Tunafahamu kwamba kule chini wako Maafisa Ushirika ambao kimsingi ndio ambao wanajasili VIKOBA pamoja na *SACCOS*. Naamini hawa wanaweza wakatumwa vizuri na wakaleta maendeleo, wakafanya kazi ya kusajili vile vikundi vya vijana, akina mama pamoja na watu wenye ulemavu ili hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii

wabaki kwenye jukumu lao la msingi la kushughulika na matatizo ambayo yapo kwenye jamii yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili kwa Serikali, kwa sababu tunatambua kwamba imekuwepo changamoto pia ya muda mrefu kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii tulionao sasa hivi hawatoshi; nikisemea tu kwenye Mkoa wangu wa Songwe tunazo wilaya nne, lakini tuna Maafisa Maendeleo ya Jamii wawili tu. Sasa huko chini kwenye vijiji na Kata bado hatuna Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe tu ushauri kwa Serikali kwamba katika kipindi hiki ni vyema wakaangalia namna gani ya kuweza kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii kama ambavyo Serikali imefanya na imefanikiwa kuajiri Watendaji wa Vijiji. Kwenye kila Kijiji Tanzania kumekuwa kuna Watendaji wa Vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini hata kwa hili la Maafisa Maendeleo ya Jamii haliwezi kushindikana kwa sababu ni Idara ambayo ni nyeti sana; na kama tukiipa kipaumbele kama ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha kuipa kipaumbele Idara hii, naamini hizi changamoto za kijamii za kimfumo zitapungua ikiwezekana, kumalizika kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine, nataka kuishauri Serikali kwamba wanasema jambo lolote ili liweze kufanikiwa, ni lazima liandaliwe. Kwa hiyo, vile vile kwa sababu tunakwenda kwenye Bima ya Afya kwa wote, waangalie sasa namna gani ambavyo watawaita hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii baada ya kwamba wameshaajiriwa na kupatikana kwa kutosha ambao ndio tunategemea kwamba waende kule chini wakaelimishe jamii, ni vyema Serikali sasa ikaangalia na wao pia waweze kuelimishwa, waandaliwe ili vile vile waweze kutafsiri ile Sera ya Serikali kulingana na tofauti za kijamii ambazo tunazo, kulingana na mila na desturi na tamaduni zote ambazo zipo kwenye jamii yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala la vitendea kazi. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Wengi wako maofisini, hawafanyi kazi yoyote ya kwenda kule chini kwenye jamii kwa sababu tu inawezekana hawana vitendea kazi, lakini kwa sababu walikuwa bado hawajajua kwamba wao wanasimamia kwenye majukumu gani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri pia Serikali yangu ya Awamu ya Sita kwamba ni vyema, kama ambavyo imefanya vizuri kwenye Maafisa Kilimo, sasa hivi kila Afisa Kilimo amepewa usafiri, vile vile wale Waratibu Kata wa Elimu wamepewa usafiri. Naamini hata kwa hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii wakipewa vitendea kazi, wanaweza wakafanya kazi nzuri zaidi na hata miradi ya Serikali itapiga hatua mbele kwa sababu hawa ndiyo wa kwenda kuelimisha jamii na kuhakikisha kwamba Serikali inaweza kufikia yale malengo ya milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru kwa nafasi. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam Mwagao na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ajiandae.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa, kabla sijachangia naomba kutoa pole kwa Watanzania wote kwa ajili ya msiba mkubwa ambaao ultupata tarehe 17 wa Mheshimiwa wetu Rais, Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli. Pia nitoe pole kwa Rais wetu wa sasa, Mheshimiwa Mama Samia Hassan Suluhi kwa ajili ya msiba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie na nitaanza na kuzungumzia ukurasa wa 67 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika ukurasa huo wa 67,

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza nia ya Serikali ya kuanza Awamu ya Pili ya ujenzi wa Mji wa Kiserikali wa Mtumba. Jambo hilo ilmenipa faraja sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu na wafanyakazi wengi wamehama kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwe na makazi ya kutosha ili wafanyakazi hawa wafanye kazi bila kuwa na shida ya upangaji wa nyumba na usumbufu wa aina yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ipo miradi ambayo Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakisaidiana na mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu ambaye ni Rais wetu wa sasa, walikuwa wameipanga. Naiomba sana Serikali izingatie sana jambo hilo. Kwanza, kuna Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato. Uwanja huu ni muhimu sana kwa Serikali yetu; kwa uchumi wetu na kwa sababu Dodoma ni Makao Makuu tutakuwa na wageni wengi ambao watatoka nje ya nchi watakuja na ndege kubwa ambazo zitahitaji kutua katika Mji wetu wa Dodoma. Vile vile kutakuwa na mwingiliano wa watu wengi, kwa hiyo, tutaweza kufanya biashara kuititia kiwanja hiki cha ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja huu wa ndege utakuza uchumi wa Jiji la Dodoma kwa sababu watu watafanya biashara mbalimbali. Walioko pembezoni mwa uwanja watafanya biashara kwa sababu kutakuwa na wageni wengi ambao watakuwa wanatua katika uwanja ule na kuondoka. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukazingatia kwamba Mji Mkuu wa nchi yetu uwe na uwanja mkubwa wa ndege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine ni kwamba kuna mpango ule wa kujenga barabara ya kuzunguka Mji wa Dodoma (*ring road*). Barabara hii ni muhimu sana. Bado ina umuhimu mkubwa, nami nafarijika kwa sababu Serikali yetu imejipanga kutekeleza. Faida kubwa ambayo tutaipata kwenye barabara hii, itasaidia kupunguza msongamano wa magari katika Jiji letu la Dodoma. Magari yale makubwa

yenye mzigo, yakinika Dar es Salaam na maeneo mengine, yakiona hayana haja ya kuingia mjini, yatazunguka kupitia hiyo barabara kuelekea Mwanza, Iringa au Arusha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara hiyo itatusaidia magari kama malori na wale wa usafiri wa kawaida ambao hawana nia ya kuingia mjini, waweze kwenda haraka na kuzunguka. Hiyo italeta mandhari nzuri sana ya Mji Mkuu wa nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mkuu hauwezi kukamilika kama hakuna maji ya kutosha. Mji huu watu wameongezeka sana, kwa hiyo, kile kiasi cha maji kilichokuwa kinatosheleza miaka ya nyuma sasa hivi hakitoshi. Tunahitaji kuwa na mkakati wa kuwa na maji ya kutosha katika Jiji la Dodoma. Mpango wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria, naomba sana Serikali izingatie; pia kuna Mpango wa kujenga Bwawa la Farkwa ambalo ni jirani sana hapa Chemba, hilo pia litasaidia kuungeza kiwango cha maji katika Jiji letu la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie sana hayo. Ili Mji wetu uweze kuonekana kwamba ni Mji Mkuu unahitaji kuwa na mambo hayo muhimu sana. Lazima wageni wetu wakifika wasikutane na shida ya maji. Kwa kweli maji ndio sura ya Jiji lolote katika Dunia. Kama hakuna maji, hata wageni wetu watatushangaa, tumeletaje Mji Mkuu Dodoma hakuna maji? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba tunatoa kipaumbele maji yaletwe Dodoma na yawe ya kutosha, yaendane na idadi ya watu wanaohamia katika Mji wa Dodoma. Baada ya miaka mitano kutakuwa na watu wengi zaidi. Kwa hiyo, suala la maji ni muhimu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia Mji Mkuu wa nchi yetu, naomba kidogo sasa nizungumze katika eneo la kilimo hususan katika eneo la mbegu. Wakulima wetu wengi bado wanalima kilimo cha zamani, cha mazoea. Wanatumia mbegu za zamani ambazo hazina tija. Hii

inatokana na ukweli kwamba, pamoja na nia njema na bidii ya Serikali kuendelea kufanya utafiti juu ya mbegu bora zenyetija lakini bado kiwango cha mbegu hakitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kiwango hakitoshelezi, shida imekuwepo kwamba mbegu inayopatikana ni kidogo, kwa hiyo, bei inakuwa kubwa. Tuki-*apply* ile *law of demand; supply* ikiwa ndogo, *demand* kubwa automatically bei itakwenda juu. Mwaka huu wakulima wetu wamenunua mbegu ya mahindi, nami nimenunua pia. Nilikuwa nanunua kilo mbili kwa shilingi 15,000/= *just imagine*, kijijini nani anaweza kununua mbegu kilo mbili kwa shilingi 15,000/=? Kwa hiyo, unaweza kuona ni kwa kiasi gani bado tunahitaji mbegu bora za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Januari kule kwetu Mpwapwa tulitembelea kiwanda kimoja kimoja kiko kule Morogoro, kinaitwa *Mahashree Agro-Processing Tanzania Limited*. Kiwanda hiki ni cha watu kutoka India, wanakamua mafuta ya mbegu mbalimbali na tulikwenda baada ya wao kuja Mpwapwa kutafuta Soko la Karanga. Sasa kabla hatujawaunganisha na wakulima wetu tuliona ni vizuri sana tujiridhishe tuone kiwanda hiki kina-*capacity* ya kiasi gani kununua karanga kwetu. Kwa hiyo, tulienda mimi, Mkuu wa Wilaya na Watendaji wa Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipofika kwenye kile kiwanda tulikuta kweli wana *capacity* kubwa sana ya kununua mbegu mbalimbali pamoja na karanga. Alichotuambia yule mwenye kiwanda ni kwamba, shida iliyoko katika maeneo yetu ya Mpwapwa na Kongwa, zile mbegu siyo bora, hazitoi mafuta ya kutosha. Kwa hiyo, alikuwa ana-*suggest* kwamba ni vizuri sana tukapata mbegu ambazo zitakuwa bora, zitakuwa na tija kwa wakulima wetu na zitatoa mafuta ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la mbegu ni muhimu sana na tunaiomba sana Serikali yetu izingatie, pamoja na mambo mengine, ili kilimo hiki kiweze kuwasaidia wakulima, lazima tuwe na mbegu bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni kwamba katika maeneo yote yenyе kilimo kama ya kwetu huko kwenye karanga na kadhalika, haitasaidia hata tukipata mbegu bora kama barabara zile zinazotoka kwenye maeneo ya kilimo hazitatengenezwa. Hilo ni jukumu ambalo nataka niwa-*assign TARURA*. Ni muhimu sana watu wetu wakipata karanga au mazao ya kutosha kama alizeti na kadhalika, ni muhimu sana kukawa na njia za kuyaleta kwenye masoko. Wakati mwingine yameharibikia shambani kwa sababu hakuna namna ya kuyaleta kwenye masoko. Kwa hiyo, suala la barabara Serikali naomba iendelee kulitilia mkazo na hasa barabara za vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. Aah, samahani, nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Mpango huu wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la elimu; Elimu ya Msingi na Sekondari pamoja na Vyuo. Mwaka 2016 Serikali ilianza Mpango wa kusomesha watoto bure katika shule za msingi na sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne (*O-Level*). Mpango huu wa Serikali uliungwa mkono sana na ukafurahiwa na wananchi kila kona ya nchi hii. Watoto waliokuwa wanakwenda kuchunga ndege katika mashamba ya mpunga, wanachunga ng'ombe, wote walipelekwa madarasani. Sasa hivi ni mwaka 2021 watoto hawa ambao walianza kusoma elimu bure wanakadiriwa kufikia milioni mbili na mwaka kesho watafanya mtihani wa darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema Serikali ina mpango wa kujenga shule 1,000 mpya za sekondari. Upungufu ninaouona kwa idadi hii kubwa ya wanafunzi takriban milioni mbili, hata kama wanafunzi hawa watafaulu kwa asilimia 80, inaonekana mpango huu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa madarasa kujenga shule 1,000 bado ni mdogo sana. Mimi napiga hizi hesabu naona hapa kuna upungufu wa karibu madarasa 103,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna madarasa 103,000, mnakuja na mpango wa kujenga shule 1,000 mpya, hawa watoto wasomea chini ya miti? Bahati mbaya sana watoto hawa ni wajukuu wa Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu ndio aliyeleta Mpango huu wa kusoma bure; na watoto wameupokea wakaenda darasani na sasa hivi wanasona siyo mchezo. Baadaye tutatengeneza *tension* kubwa sana ya nchi hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ataanza kuzuia watu wasiende likizo na wapi, sasa hii ni hatari. Hili jambo inaonekana kama anaachiwa Waziri Mkuu peke yake, wakati hili ni janga la nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mpango huu wa bajeti kwa haya madarasa 1,000 Wabunge muyakatae. Ninyi Wabunge shauri yenu mwaka kesho watoto watakuja kwenye majumba yenu, hakuna Mbunge atakayekuwa salama, hizi shule ni chache. Mheshimiwa Waziri wa Serikali za Mitaa na Manaibu tafadhalini sana rudini mkaandae mpango mwingine mpya mjenao hapa vinginevyo hali itakuwa tete hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kitu kibaya kama Waziri Mkuu bajeti yake watu wakang'ang'ania shilingi, hii itakuwa ni hatari sana katika nchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuheshimu sana katika jambo hili, lakini wasaidizi wako ulionao naona wanataka kukutengezezea bomu haya madarasa ni mdogo. Mimi kwangu tu kwenye Jimbo la Sengerema nahitaji shule mpya 30 na nchi hii ina majimbo karibu 200, itakuwaje? Hii ni hatari Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la walimu; walimu wa shule za msingi na sekondari katika nchi hii wako laki mbili na sitini na moja kama na mia mbili hamsini na tatu. Walimu wa shule za msingi wako laki moja na sabini na tano na amia nane, walimu wa sekondari wako elfu themanini na tano. Upungufu walimu elfu arobaini. Kwenye mpango ajira zinazookeana hapa ni chache. Hawa wanafunzi 40,000 Serikali iliwekeza, imewasomesha hawa wanafunzi kwa pesa za mikopo, leo hawa walimu wako mitaani halafu ninyi mna upungufu wa walimu 40,000, hamtoi ajira. Mwaka kesho ni janga la kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani bajeti yetu hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, msimfedheheshe Waziri Mkuu. Waziri wa Fedha, Waziri wa Kazi, Waziri wa Elimu liangalieni hili suala kwa sababu huko shuleni sisi ndio tunajua shule moja unakuta ina walimu 16 wanafunzi elfu moja na zaidi. Kwa mfano, kwangu Shule moja ya Msingi Mnadani wanafunzi wa darasa la sita ni 500, sasa kwa shule nilizonazo mimi tu peke yake kwa Sengerema Mjini wanafunzi watakaofanya mtihani ni zaidi ya wanafunzi 7,000 sasa hii si ni hatari, tutawapeleka wapi hawa wanafunzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui bwana mwaka kesho itakuwaje. Kila atakayekuwa anaingia humu atakuwa anameza dawa za ugonjwa wa moyo, hatari itakuwepo kubwa sana mwaka kesho. Tunaiomba Serikali katika jambo hili ilitilie mkazo wa hali ya juu sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasam, hilo la ugonjwa wa moyo kila anayeingia humu ndani ni unabii au ni kitu gani?

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, hali itakavyokuwa kwa sababu, nachotaka kukwambia sasa hivi bado tuna maboma kule. Kwa mfano, mimi nina ujenzi wa sekondari 15 ambazo hazijakamilika jana nilikuwa naangalia hii hesabu mimi mwenyewe nikawa naogopa, hawa nilionao sasa hivi elfu saba sijamaliza kuwapeleka sekondari, mwaka kesho kuna bomu llingine linakuja na mwaka huu bado wanakuja hawa watu, sasa najiuliza...

NAIBU SPIKA: Sawa, sasa kuhusu ugonjwa wa Wabunge, hilo hata wewe fanya mazoezi usijenao humu ndani. Wabunge hawa wa Mheshimiwa Spika Ndugai watarudi wazima kabisa humu ndani. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kukwambia mimi niko *serious* katika jambo hili. Mimi nafikiri huu mtaala wa ualimu muufute katika vyuo vikuu kwa sababu mnawapeleka watu wanakwenda kusomea ualimu, una upungufu wa walimu hamtaki kuajiri wako mtaani, inakuwaje? Mnafikiri hawa wazazi ambao watoto wao wamekwenda kusomea ualimu na wako nyumbani mnategemea nini? Hawa vijana wetu itakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu tunao, lakini katika huo upungufu tullionao wa walimu hamtaki kuajiri, mnakuja na ajira 6,000. Mimi nashindwa kuelewa jambo hili. Jamani twendeni mbele ya safari, lakini mjue kwamba tunakwenda kufanya kampeni 2025 na kampeni tuanze sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe kama hunisikilizi ananisikiliza Mheshimiwa Samia. Mheshimiwa Samia ndiyo atajua hawa 40,000 upungufu utakuwaje. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasam, hebu tuelewane kidogo, hebu kaa kidogo nikueleweshe.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inakuwa hatari.

NAIBU SPIKA: Wewe changia hoja, hakuna mtu anayehitaji kutishwa, hayupo. Mara useme watu hawatarudi, mara watu watarudi na *pressure*, aah aah, wewe changia tu hoja yako umalize.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu umezilinda hizo maana tayari umeshanipoteza moja hiyo. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tabasam inabidi nikupeleke darasani. Usiwe unabishana na Kiti. (*Kicheko*)

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, sibishani.

NAIBU SPIKA: Eeh, usibishane. Na mimi pia sipangiwi muda wa kuzungumza humu ndani unayepangiwa ni wewe, malizia mchango wako.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa walimu elfu arobaini. Mheshimiwa Waziri Mkuu utaangalia katika bajeti yako uone namna gani tutafanya ili tuondoe hili tatizo kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni maboma. Yako maboma yaliyojengwa kwa ajili ya madarasa, yako maboma yaliyojengwa kwa ajili ya nyumba za walimu, lakini yako maboma yaliyojengwa kwa ajili ya zahanati na yako maboma yaliyojengwa kwa ajili ya vituo vya afya. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba uunde kikosi kazi kipite nchi nzima, kitakuletea taarifa iliyo sahihi kwa sababu, kuna taarifa nyingine zinafichwa kwa ajili ya usalama wa hawa wakuu wetu walioko kule. Wanaogopa kusema maboma yaliyopo kwa sababu wanaonekana tayari pesa zinazokusanywa katika halmashauri zetu zinatumika vibaya. Maelekezo yako uliyokuwa unayatoa kwa ajili ya hizi Halmashauri zetu kutenga fedha, hazina mapato ya kutenga fedha kumaliza maboma haya ni lazima Serikali isaidie mpango huu wa haya maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine tulilonalo sisi kule ni la vyuo hivi vya VETA pamoja na maendeleo ya jamii. Hivi vyuo naombeni vitumike vizuri kwa sababu uwekezaji uliotumika hapa; kwa hii miaka sita tumewekeza shilingi trilioni moja na milioni mia sita na hamsini, kila mwezi tunawekeza katika elimu shilingi bilioni 23. Sasa hizi shilingi bilioni 23 kwa miaka yote hii mpaka sasa hivi leo ni miezi 72 sawa na shilingi trilioni moja na milioni mia sita, halafu baadaye hawa wanafunzi wakishindwa kufaulu wanarudi nyumbani. Ushauri

wangu, darasa la saba wakishindwa kufaulu wapelekwe moja kwa moja kwenda kwenye hivi Vyuo vya Maendeleo ya jamii pamoja na vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Taufiq, Mheshimiwa Subira Khamis Mgali ajiandae.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku chache zillzopita kupitia Bunge lako hili Tukufu tulikaa na kujadili na kuitisha Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano. Yote ambayo tumeyapitisha, yote ambayo tumeyajadili na leo hii tupo kujadili na kuitisha bajeti za Wizara mbalimbali, tutambue kwamba ufanisi wa jambo hili hauwezi kabisa kupatikana ikiwa wananchi wetu hawana afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ripoti ya CAG inayohusiana na mashirika ya umma, ukurasa namba 128, utaona jinsi ambavyo CAG kwa uwazi kabisa ameweza kuonesha ukosefu wa mamlaka ya kudhibiti bei za dawa pamoja na vifaa tiba. Tunatambua na tunafahamu kwamba, Watanzania wote au niseme asilimia kubwa ni maskini, si wanyonge, lakini ni maskini. Watanzania hawa hawawezi kabisa kumudu bei ghali za dawa pamoja na vifaa tiba. Kutokuwepo kwa chombo hiki cha kudhibiti bei za dawa pamoja na vifaa tiba kumesababisha wafanyabiashara wanaouza dawa pamoja na vifaa tiba kujipangia bei kadiri wao wanavyoona inafaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu kuu mbili zinazosababisha dawa na vifaa tiba kuwa na bei ya juu sana. Serikali yenyewe ambayo inapaswa kuwa namba moja

kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma nzuri za afya kwa bei nafuu ndiyo ambayo imekuwa ikisababisha wafanyabiashara kupandisha bei za dawa pamoja na vifaa tiba kwa sababu katika hospitali zetu hakuna dawa kabisa. Serikali hii ambayo siku zote inajinasibu kwamba imekuwa ikitekeleza yale ambayo imepanga imekuwa ni namba moja kusababisha wananchi wetu kushindwa kumudu dawa hizi ambazo nimezielezea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo basi, naomba niseme hivi, tunayo *MSD* ambayo kazi yake ni kununua na kusambaza dawa pamoja na vifaa tiba katika hospitali zetu, lakini kumekuwepo na upungufu mkubwa wa dawa hizi ambazo naelezea pamoja na vifaa tiba. Ni kwa nini basi kumekuwepo na huu upungufu? Ni kwa sababu Serikali imekuwa ikikopa fedha kutoka *MSD* na hairejeshi kwa wakati na wakati mwingine hairejeshi kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2017, 2018 na 2019, Serikali hii ilikuwa inadaiwa shilingi bilioni 53.63. Tungetegemea kwamba katika Ripoti ya *CAG* ya sasa tuone ni jinsi gani Serikali imeweza kupunguza, kama siyo kumaliza kabisa deni hilo ambalo ni kubwa sana. Hata hivyo, katika ripoti hii mpya ya *CAG* inasema, Serikali mpaka sasa inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 256. *This is a shame* kwa sababu huwezi kuwa inapoitwa leo wewe unazidi kuongeza madeni. Tulitegemea Serikali iwe ndiyo namba moja kuwa na huruma kwa Watanzania hawa. (*Makofî*)

TAARIFA

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Eric Shigongo.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu kumkumbusha mzungumzaji aliyejekuwa anazungumza kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imechukua hatua za kutosha kabisa za kuimarisha *MSD*.

Kiongozi Mkuu wa *MSD* kwa sasa alitoka Jeshini. Chini ya uongozi wa Meja Jenerali huyu, *MSD*imefanya *improvement* kubwa sana ikiwemo kuanzisha kiwanda chake yenewe cha kutengeneza *paracetamol*. *MSD*inatengeneza *paracetamol* zake yenewe na imeweza kushusha *cost* za kufanya *dialysis* katika nchi yetu. Kwa hiyo, kusema kwamba, ni *shame* sio jambo sahihi, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Lambert, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hiyo siipokei kwa sababu nilichokitaja hapa kwamba Serikali inadaiwa shilingi bilioni 256 ni kutokana na Ripoti ya CAG.

Sasa Mheshimiwa Mbunge pale kama anadhani kusema kwamba wamejenga kiwanda cha kutengeneza *Panadol* ndiyo iwe sababu sasa ya kusema kwamba mna haki ya kukaa na shilingi bilioni 256, *yet* Waziri husika anakuja hapa mbele anatuambia kwamba tunazo dawa katika hospitali, *it can't be.* (*Makofii*)

TAARIFA

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, kuna Taarifa nyiningine kutoka kwa Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya.

TAARIFA

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie mzungumzaji Mheshimiwa Agnesta kwamba sasa hivi tunajadili kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu, hatujaanza bado kujadili Hotuba ya CAG, nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Lambert.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa sababu nafahamu na kutambua kwamba Mheshimiwa Khadija anafahamu fika kabisa kwamba anachokisema sicho kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee kujikita katika ushauri kuhusiana na jambo hili kwa upande wa Serikali. Kwa sababu ikiwa tutakuwa hatuna chombo hiki maalum au mamlaka maalum ambayo itadhibidi bei za dawa pamoja na vifaa tiba, mwisho wa siku tutakuwa na Watanzania ambaao usiku na mchana wanaumwa na magonjwa madogo lakini wanakosa dawa ambazo kimsingi dawa hizo zilipaswa kuwepo. Kauli mbiu ya Serikali ya sasa ni ushindani wa viwanda na maendeleo ya watu iende sasa ikajielekeze katika kulipa hizi shilingi bilioni 256 ili mwisho wa siku *MSD* waweze kuleta dawa kwa wingi kuliko ilivyo sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia hapa wengine wanachangia, Waziri alikuwa anajibu anasema dawa zipo, hakuna kitu kama hicho. Ni *knowledge* ya kawaida tu *MSD* wanategemea Serikali ilipe madeni na wenyewe waende kuagiza dawa, lakini mwisho wa siku *MSD* inaonekana imekuwa na yenyewe ikikopa kule inakoagiza dawa. Kwa hiyo, inafika sehemu ambayo haiwezi tena kuagiza mpaka Serikali iweze kulipa madeni. Kwa kipindi hiki ambacho tunapitia katika mlipuko wa wimbi la pili la *Covid-19* ni vema basi Serikali hii ikafanya kwa vitendo kulipa hili deni ili mwisho wa siku tuweze kuhakikisha kwamba tunaona hili suala la *Covid-19* hatupati shida ya dawa katika hospitali zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa hii mamlaka ambayo nimeisema mwisho wa siku Watanzania wanakwenda kununua dawa katika *pharmacywanakutana* na bei ghali sana. Hii ni kwa sababu wafanyabiashara wa dawa hizi hawana kitu kinachowa-*limit* kwamba dawa hii inapaswa kuuzwa kwa bei kuanzia elfu moja mpaka elfu tano. (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeshakwisha ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo na Mheshimiwa Njalu Silanga ajiandae. (*Makofi*)

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuleta hoja yake hapa ambayo ni Mapitio na Maelekezo ya Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge 2021/2022. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kuhusiana na Mkoa wa Dodoma lakini baadaye nitazungumzia kuhusiana na suala zima la ugonjwa wa UKIMWI, madawa ya kulevyu pamoja na kifua kikuu. Sisi katika Mkao wa Dodoma kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu na pia kuifanya kuwa Jiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo inatakiwa itekelezwe katika Mkao wa Dodoma ili kusudi iweze kuleta picha halisi na sura halisi ya Makao Makuu. Ipo mingi ambayo imetekelizwa, lakini nina ushauri kwamba tuna uwanja wa ndege wa Msalato, sisi wananchi wa Dodoma tunafurahia sana kuwepo uwanja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi uwanja huu pesa zake zipo, lakini tatizo lipo kwenye fidia, kwamba wale wananchi ambaeo walitakiwa walipwe fidia, wako wananchi kama 1,053 kati yao waliolipwa fidia ni 874, kwa hiyo bado 176. Kwa hiyo tunaiomba Hazina iharakishe kuwalipa wananchi hawa ili kusudi mwisho wa siku kazi iweze kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna waathirika ambao ni *outer ring road* ya Dodoma, barabara ambayo ikijengwa itaondoa sana msongamano wa magari katika Mkoa wetu wa Dodoma. Barabara hiyo ina kilometa 112 na waathirika ambao wanatakiwa kulipwa ni 2,672 ambao wanatakiwa kulipwa zaidi ya bilioni 15.7. Kwa hiyo naiomba Serikali ione umuhimu wa kuharakisha kuwalipa waathirika hawa ili kusudi kazi iweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba niikumbushe Serikali kuhusiana na barabara muhimu ambazo zitaleta maendeleo ya kiuchumi katika Mkoa wa Dodoma, barabara hizi zikijengwa kwa kipindi muafaka ina maana kwamba wananchi wa Dodoma tutafaidika Zaidi. Tunaishukuru sana Serikali kwa maendeleo yote ambayo imeifanya lakini pia tukipata barabara hizi zitatusaidia sana. Miongoni mwa barabara hizo ni pamoja na Barabara ya Mpwapwa - Gulwe - Kibakwe ambayo ina kilometa 124; Stesheni ya Gulwe - Kongwa Junction - Simanjiro hadi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna daraja la *TANESCO* Mpwapwa linahitaji kufanyiwa matengenezo na daraja la Godegode ambalo limekuwa tatizo kubwa sana. Sambamba na hilo, Marehemu aliye kuwa Rais wetu pia alituahidi kwamba itajengwa bandari kavu ya kilometa sita katika eneo la Ihumwa. Kwa hiyo tunaombia Serikali ione kwamba mambo haya yanafanyika. Pia naomba nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba pale anapokuwa akitembea kuhusiana na mazao ya kimkakati, yale mazao matano, basi aone pia na zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma, tufanyiwe liwe zao la mkakati ili wananchi wa Dodoma waweze kuondokana na suala la umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu masuala ya UKIMWI. Mimi ni Mwenyekiti wa Masuala ya UKIMWI kuna mambo kadhaa nilitamani kuyakumbusha, lakini niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imeifanya ya kufanya maambukizi yaweze kupungua. Hata hivyo, naomba kutoa ushauri kwamba, kundi la vijana inabidi

liangaliwe sana kwa sababu hili ndio kundi la waathirika wakubwa, Serikali iweze kuweka nguvu Zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tuna ule Mfuko wetu wa *Aids Trust Fund*, Serikali ione umuhimu wa kuwa na vyanzo vya kudumu vya kutunisha Mfuko huu. Jambo kubwa ambalo nataka pia niwaambie Waheshimiwa Wabunge hasa wanaume, kwa sababu takwimu imeonyesha kwamba wanaume wengi hawajitokezi kupima UKIMWI.

Kwa hiyo tunaomba tuanze mfano na Wabunge wanaume humu ndani, waweze kupima UKIMWI na wakitoka hapo waweze kwenda kuhamasisha kwenye zile jamii zao kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara zetu tulikutana na wenye VVU, wakasema wao wanaishi kwa malengo kwa sababu wanaijua afya yao na sisi tunaoishi kwa matumaini maana yake hatujui afya zetu. Kwa hiyo natamani kwamba hebu idadi ya wanaume wajitokeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu tohara. Kwa kweli tohara ya wanaume pia ni muhimu sana kwa sababu imeonekana kabisa inasaidia kutokuleta maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu madawa ya kulevyia. Vijana wetu wengi sana wameathirika na madawa ya kulevyia. Kwa hiyo tunaishauri Serikali ijenge Ofisi ya Kanda ili kusudi kuweza kuwashudumia hawa vijana hasa wale waraibu waweze kupata hizi dawa za *methadone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo napenda niishauri Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya UKIMWI, kifua kikuu na dawa za kulevyia watoe elimu ya lishe katika vituo vyote vya tiba na mafunzo, kwa sababu hii elimu ya lishe itawasaidia wale wenye VVU au wale wagonjwa ili kusudi afya zao ziweze kuimarika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda sio rafiki sana naomba niseme kwa uchache kwamba, kwenye magereza yetukumekuwa kuna shida sana ya msongamano, hivyo kusababisha magonjwa ya kuambukiza hasa *TB*. Kwa hiyo naomba Serikali iliangular hili jambo, tuweze kupambana na kifua kikuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja na nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye ajiandae.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema ambapo nimeweza kusimama ndani ya Bunge hili na pia niwatakie Waislam wote *Ramadhan Kareem*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vizuri bajeti ya Ofisi yake kwa mwaka wa 2021/2022. Nikimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ninukuu sehemu ya kipande cha Hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan wakati wa shughuli ya kumuaga Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano kama ifuatavyo; "Tunapokwenda kumpumzisha Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tunaweza kusema bila kigugumizi kuwa tuko tayari kuiendeleza kazi yake nzuri kwa nguvu kasi na ari ile ile."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimenukuu maneno haya ya Mheshimiwa Rais Mama Samia na nampongeza sana, baada ya kuona ahadi aliyoiahidi na uwasilishaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu inaenda sambamba. Nasema hivyo kwa sababu nikiangalia majumuisho yake ya mambo ambayo Serikali itajielekeza nayo, akifanya *summary* ya bajeti

yake nzima, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati iliyoanzishwa na Hayati Rais Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mradi huo ni ununuzi wa ndege na Serikali imesema hapa imeshalipia ndege tatu, majadilliano mbalimbali yamefanyika ndani ya Bunge, nayaunga mkono, lakini nataka kusema moja tu, wengi wamekuwa wakinukuu taarifa ya CAG, hata watumiaji wengine wa taarifa hii baada ya kuwasilishwa Bungeni, lakini nataka niseme, tusimuwekee maneno zaidi CAG, kwa sababu kwenye ukurasa wake wa 16 na 17 pamoja na hasara ya Shirika la Ndege hii, CAG hajasema kama uwekezaji huu ni hasara, badala yake ameshauri kudhibiti garama za uendeshaji pamoja na za kibashara ili kampuni hii isiendelee kupata hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania tupate tafakuri mpya, kama TANROAD tunaiwekea zaidi ya triliioni tatu kwa ujenzi wa barabara na haiandai taarifa ya kuonyesha kwamba tunahitaji kuona faida na hasara, ni huduma tu kwa sababu barabara zinasaidia sekta nyingine, ufile wakati tuliamini shirika la ndege linatoa huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mradi mwengine wa kimkakati ambapo Waziri Mkuu kuitia hotuba yake amesema atauendeleza ni ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na mradi huu CAG amekagua na nataka niseme ni mradi pekee ambao ameukagua wenyewe kurasa nyingi kama 32. Watumiaji wengi wa ripoti yake wamejielekeza kwenye kipengele kimoja cha kutokuwepo kwa upembuzi wa kina, ningombaa niwashauri waisome vizuri...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgusu, subiri kidogo, Mheshimiwa Halima naona umesimama.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, yes. Mheshimiwa Subira ni Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Bajeti...

NAIBU SPIKA: Ngoja nijue ni kuhusu utaratibu, taarifa au kitu gani?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa.

NAIBU SPIKA: Sawa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa kutokana na alichokisema, nasema hivi Mheshimiwa Subira anafahamu chini ya taarifa ya Msajili wa Hazina ya Mashirika ya Umma ya Serikali, kuna mashirika ambayo yanatoa huduma na kuna mashirika ya kibiashara. *ATCL* ni shirika la kibiashara, kwa hiyo ni muhimu wakati tunachangia haya mambo, tujue linatoa huduma lakini ni la kibiashara, halijawekwa pale kutoa huduma *perse*, linafanya huduma *then we expect to make profit*. Kwa mazungumzo anayozungumza asi-*mislead* juu ya jukumu la shirika letu la ndege. Ni hayo tu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgatu, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokea hiyo taarifa kwa sababu hakunisikiliza vizuri. Ni kweli natambua na yeye ni mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Bajeti, nimesema ni kweli shirika la *ATCL* ni milongoni mwa mashirika 28 ambayo taarifa ya *CAG* imesema imepata hasara, ni shirika pekee la kibiashara, lakini nimetoa maoni yangu kwamba kama *TANROADS* tunaiona inatoa huduma inatengeneza barabara ni kwa nini usifike wakati shirika hili ambalo nalo lina wajibu wa kuchochea sekta nyingine kuitia huduma ya usafiri wa anga, kwa nini nalo lisitoe huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee katika mradi huu wa Mwalimu Julius Nyerere pamoja na ukaguzi mzuri uliofanywa na *CAG*, nimeainisha kwamba katika kuhuisha upembuzi yakinifu *CAGamesema*, tathmini ya athari za mazingira imefanyika, usanifu wa kiufundi na utafiti ya

geology umefanyika, utafiti wa kitaaluma ufanisi wa miamba umefanyika. Naomba nimnukuu kwenye ukurasa wa 128, maelezo ya CAG namnukuu: "Kulingana na tathmini iliyofanywa hadi sasa, nilibaini kuwa hakuna udhaifu mkubwa wa kiufundi ambao unaweza kuzuia mradi kufikia malengo mahsus iyaliyokusudiwa."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi, wasimlishe maneno Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hiyo ndio ripoti. Katika hili niiombe Serikali, katika moja ya hoja kwenye mradi huu ni makubaliano ya mkataba ya asilimia nne kwa ajili ya miradi ya kijamii ya maeneo yanayotekeleza mradi huu. Wananchi wa Rufiji, wananchi wa Morogoro vijijini wanasubiri kwa hamu mchango wa asilimia nne wa mkandarasi wa gharama ya mradi kwa ajili ya miradi ya elimu na kwa ajili ya miradi ya afya. Kwa hiyo niiombe Serikali hilo lishughulikie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo yalitolewa maoni hapa pamoja na wachangiaji, tuongeze bidhaa ili tuweze kukusanya mapato Zaidi. Mradi huu unaenda kuleta bidhaa ya umeme, umeme utakuwa mwingi ambao unatakiwa uuzwe nchi za jirani na Serikali imejipanga vizuri, inajenga sasa *transmission line* ya Singida – Namanga ambayo itawezesha kiwango cha umeme kingine kuuzwa nchi jirani tukapata mapato na kutekeleza miradi mingine ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze pia katika moja ya kipaumbele cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia makusanyo ya mapato. Katika hili nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anapitia, natambua tulipokuwa tunamwona kwenye ziara mbalimbali akija kwenye halmashauri zetu, anakuja na taarifa kabisa na wengi wale ambao waliokuwa wanajihuisha na ubadhirifu wanasimamishwa, wanapisha uchunguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe katika hili kwa kuwa tunatafuta mapato ya nchi yetu na kwa kuwa Serikali imepewa maelekezo na Mheshimiwa Rais Mama Samia ya

kupanua wigo wa ukusanyaji mapato; na kwa kuwa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameainisha namna gani Serikali ina mpango wa kupunguza mashauri katika Mahakama, katika hili naomba niseme, katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, naomba Serikali iimarishe mamlaka za rufaa za kodi. Fedha ya mapato inaweza ikapatikana pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza kwa mujibu wa taarifa ya CAG, kuna kesi zaidi ya 1,097 zenye thamani ya triliuni 360, utaona ni kiasi gani cha fedha zilizopo kwenye masuala ya kesi mbalimbali. Endapo Serikali itaingilia kati na hapa nakumbuka hata Hayati Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu alitoa maelekezo hayo kwamba mamlaka za kodi za rufaa zisikilize hizi kesi haraka ili kama kuna mapato yoyote Serikali iweze kuyapata.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali na nampongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Njalu Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Nani anazungumza? Nimeshakuona, Mheshimiwa Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 76 jambo ambalo limetokea hapa Bungeni mapema leo. Ripoti ya CAG ndio kwanza imefika katika Bunge lako Tukufu na kwa kawaida

inatakiwa ichakatwe katika Kamati za Bunge lako, lakini tumeanza kuijadili humu ndani wakati hajachakatwa na Kamati na kuleta humu ndani katika Bunge lako. Nomba mwongozo wako kuhusu jambo hili.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 76, anaposimama Mbunge kuomba mwongozo swali linakuwa kama jambo hilo alilolieza linaruhusiwa au haliruhusiwi kufanya Bungeni. Sasa kwa sababu taarifa ama ripoti ya CAG imeshawekwa mezani hapa Bungeni na ikishawekwa mezani hapa Bungeni ni taarifa kwa umma wote. Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge, Bunge litajadili mahsusni taarifa ya CAG baada ya kupitia kwenye Kamati kama utaratibu wetu ulivyo, lakini Mheshimiwa Mbunge hakatazwi kuitazama ile taarifa ya CAG na kutoa wazo lake kuhusu jambo lolote analoona linahusiana na hoja iliyopo mezani. (*Makof*)

Nadhani hii sehemu ya mwisho ndio ambayo Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa kuitilia maanani. Unapojadili hoja ya CAG usije na hoja peke yake kwa sababu hajjawekwa mezani kwa ajili ya mjadala, lakini unaangalia taarifa ambayo tunaisema ama bajeti ya Serikali kama jambo hilo unalolisema lina uhusiano, hukatazwi kulisema. Kwa hiyo muktadha ni huo, Bunge kama Bunge halitahojiwa kwenye hoja zinazotokana na taarifa ya CAG, lakini Mbunge hakatazwi kutumia taarifa ya CAG kwenye mchango wake. Huo ndio mwongozo wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Njalu Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, ajiandae.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kuwapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika Awamu ya Tano na Awamu hii ya Sita. Serikali ya Awamu ya Tano na Serikali ya Awamu ya Sita tulijikita sana kuhakikisha tunapeleka huduma bora kwa wanachi wetu.

Tumejenga vituo vya afya tumejenga zahanati na tumejenga Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo kila Mbunge na kila maswali yanapoulizwa tuna tatizo kubwa la watumishi wa kada ya afya. Ningehauri Serikali katika kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ilete bajeti mahsus kwaajili ya kada ya watumishi hawa ili kusudi fedha nyingi ambazo tunaendelea kuziwekeza kwenye zahanati zetu na kwenye hospitali pamoja na vituo vya afya ili majibu kwa wananchi wetu yaweze kupatikana kulingana na utekelezaji wa kazi tunazoendelea kuzifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo linakuwa la kusikitisha wakati mwingine Kijiji kimoja kina wakazi 4,000, 2,000 huko Usukumani lakini nesi anakuwepo mmoja kwa siku nzima yule nesi tunampa wakati mgumu wa kutoa huduma kwa wananchi wetu ambao tunakuja kuwakilisha humu. Ningeomba jambo hilo Serikali ilichukue na ilifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Waziri Mkuu imezungumzia mambo ya Ushirika imezungumzia mambo mengi sana. Tunaotoka kwenye mazao ya kimkakati haya ambayo tunayaona kabisa Serikali ina nia nzuri ya dhati kuhakikisha kwamba inatengeneza ushirika, inatengeneza AMCOS, inatengeneza TMX lakini yako majukumu ambayo TMX anatakiwa ayafanye lakini yako majukumu ambayo watu wa ushirika wanatakiwa wayafanye, lakini yako majukumu mwananchi naye ayatekeleze kulingana na jinsi alivyohangaika kupata hayo mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la TMX ni taasisi ya Serikali lakini inatakiwa kutafuta masoko nje ya nchi lakini kinachotokea kwenye TMX ya hapa kinachofanyika yeye anaondoka anaenda kijijini anaenda kuusimamia ushirika na anaenda kuchukua 1% ya bei inayopatikana jambo hili haliwezekani na jambo hili tunawaumiza wakulima wetu na halina tija yoyote katika Taifa letu hili. Nitatoe mfano kwa miaka ya nyuma kulikuwa na chombo kinaitwa Mamlaka ya

Pamba ambacho ilipewa jukumu la kuuza pamba yote ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yaliyotokea Shirika lile lilifilisika na liliteta madhara makubwa na hatima yetu leo ushirika wote ulifilisika kwasababu ya vyombo hivi. Na mfano TMX wameanza tangu mwaka 2018 kwa kasi 2019 tukainga na tatizo la kukosa masoko ya zao la pamba TMX hawa nilidhani wangeonyesha njia yao kubwa kuhakikisha kwamba sasa wanauwezo wa kutafuta masoko na kuuza mazao yetu yale lakini matokeo yake hakuna kilichofanyika na Serikali ilibidi kuingilia kati kuhakikisha kwamba wanatatua changamoto hiyo TMX alikaa pembeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana Serikali ijaribu kuangalia inapoleta mipango mizuri hasa inapokwenda kwa wananchi wetu na tuelewe 70% ya watanzania ni wakulima na wafugaji

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, (*Kicheko*)

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njalu Silanga naona Jirani yako anataka kukupa taarifa Mheshimiwa Boniventura Kiswaga

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba TMX imejiondoa kwenye jambo lake la kimsingi la kutafuta masoko na kuwa dalali wa wakulima kuwanyonya wakulima badala ya kuwaongezea masoko wakulima. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njalu Silanga unaipokea taarifa hiyo?

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwasababu ni mojawapo ya waathirika katika wilaya yake ya Magu, iliokea sana mwaka jana na mwaka huu kwenye zao la choroko pale Maswa ulifanyika mnada wakati korosho inanunuliwa katika bei za kawaida ilikuwa 1500 mpaka 1400. *TMX* walipokuja kufungua mnada wao waliwauzia wakulima bei ya 1350 kwa hiyo, tayari shilingi 1500 ikawa ni *short* kwa wakulima wetu hawa na ikatolewa *order RAS* wa Simiyu akasema halmashauri *i-top* ile tofauti kwa wakulima jambo ambalo yako mambo mengine inabidi Serikali iyatazame na kuyachunguza hasa Wizara ya Fedha kwasababu TMX wako kwenye Wizara ile wahakikishe kwamba unapoleta mikakati ya kuja kuwasaidia wakulima si mikakati ya kuja kuwanyonga wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba...

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njalu Silanga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bashe

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kumpa taarifa msemajji na Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Kilimo imeshachukua hatua kwenye suala la TMX na haitofanya shughuli za minada katika msimu wa mwaka huu na tunafanya tathmini ya ujumla kwahiyio wasiwe na hofu majaribio yaliyofanyika mwaka jana tumeona matokeo na tumeona athari kwahiyio tumeshafikia maamuzi kwamba ushirika utaendelea kufanya shughuli zake za ushirika na TMX itarudi kwenye *core function* yake. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Nadhani hiyo inatoa picha namna ambavyo Serikali inasikiliza sana maoni ya Wabunge humu ndani mmeefanya jambo jema. Mheshimiwa Njalu Silanga.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa lakini iwe taarifa ya vitendo maana mwaka huu Bunge la Kwanza tulipokaa humu Waziri Mkuu aliulizwa swali la papo kwa papo akaeleza kwamba ushirika TMX

hawataingilia katika mazao haya. Kilichotokea mikoa mingine ilianza kutekeleza walipofika Shinyanga wafanyabiashara gari zao zilizuiliwa na kupigwa mnada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kauli yake Mheshimiwa Naibu Waziri anayoizungumza iwe kauli ya kulieleza Bunge na iwe kauli ambayo ni mahsus kwa watanzania. Maana tunachozungumza hapa tumetumwa kuja kuwawakilisha watanzania na tumetumwa kuja kuzungumza changamoto zao ambazo wanazipata na cha ajabu zaidi yako mazao mengine hayahitaji hata kuyaingiza kwenye mifumo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoamini choroko ni zao la wakinamama ambalo walikuwa wakililima vizuri kwa mahitaji madogo madogo sasa unapobeba kilo 3, kilo 7, kilo 7 kwenda kuziweka kwenye godauni unatengeneza umaskini na manung'uniko kwa wananchi wetu hawa. Jambo hili halikubaliki na kwa sababu Serikali hii ni sikivu ya Chama Cha Mapinduzi ninaamini haya ninayoyazungumza wataenda kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu Serikali katika maeneo ambayo imefanya upembuzi yakinifu katika maeneo yetu mfano kutoka Bariadi kuja mpaka Singida ningeomba jambo hili kwenye bajeti hii basi watengee barabara ile iweze kutengenezwa na watu waweze kusafiri na kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna uwanja wa ndege pale Mwanza kuna njia ya kutokea pale llemela *by pass* ya kuingia kwenda *airport* ningombia Serikali nalo hili ichukue ilifanyie kazi ili wananchi waondokane na msongamano wa kupita pale Mwanza katikati ambao unakuwa ni msongamano mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo Serikali ningeomba kuendelea kuishauri kwamba mambo mengi mazuri yameendelea kufanywa na Serikali ya Awamu

ya Tano na naamini na Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kufanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupertia Ofisi ya Waziri Mkuu tunahitaji sisi ndege ziendelee kununuliwa kwasababu ndege ndio huduma mbadala ya haraka kuleta huduma. Lakini ningemba sana ipatikane ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza kwasababu ni watu wengi wanaotoka Mwanza kuja hapa hata viongozi wa kiserikali hawa wakati mwingine inabidi waende Dar es Salaam ndio waende Mwanza jambo ambalo linatupotezea muda. Naiomba Serikali ndege zile tatu zije sisi tuendelee kusafiri kwa ndege, tuendelee kutoa huduma nzuri kwa watanzania ili mambo yaende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nape Moses Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga ajiandae.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kwa niaba ya wananchi wa Mtama nitoe pole kwa familia ya Dkt John Pombe Magufuli kwa kuviwa na Mheshimiwa Rais. Lakini kwa wana CCM kwa kuviwa na Mwenyekiti wa chama chetu na kwa watanzania nitoe pole nyingi sana kwa kifo cha huyu mzalendo wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajisikia fahari kwamba nilishiriki ndani ya chama na nje ya chama katika mchakato wa kumpata Dkt John Pombe Magufuli mwaka 2015. Amefanyakazi nzuri kwa Taifa letu ameacha alama nyingi kubwa ambazo hazitasahaulika. Lakini ameacha mafunzo mengi kwa nchi yetu, kwa chama chetu, kwa bara la Afrika na hata dunia inajadili mafunzo aliyotuachia. Kwa hiyo, ninajisikia fahari kwamba nilishiriki mchakato wa kupatikana

kwake, na namshukuru Mungu kwa maisha ya Dkt John Pombe Magufuli kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kikipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa kusimamia vizuri mchakato wa mpito kutoka Rais Dkt. Magufuli kwenda kwa Mama Samia usimamizi mzuri uliofanywa na chama umethibitisha kwamba CCM bado ni chama bora sana kwa nchi yetu, kwa Bara la Afrika na duniani. Wamesimamia vizuri mchakato niwapongeze viongozi na chama changu. Siyo nchi nyingi zinaweza kusimamia mchakato wa namna hii wengine ingekuwa fujo na vurugu. Chama kimeonyesha uwezo mkubwa wa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwahiyu nakipongeza chama changu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuiheshimu katiba ya nchi yetu na kusimamia vizuri hongereni sana Mabeho na wenzako kwa kazi nzuri mliyofanya katika kipindi chote cha mpito. Nchi yetu imepitia Awamu tano na sasa tuko Awamu ya Sita ya uongozi Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikaa miaka karibia 24. Awamu ya pili ya mzee Mwinyi, Awamu ya Tatu ya mzee Mkapa, Awamu ya Nne ya mzee Kikwete, Awamu ya Tano ya Dkt Magufuli na sasa Awamu ya Sita ya mama Samia Suluhu Hassan. Katika awamu zote hizi chama kimesimamia viongozi wake kufanyakazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere alikuja mzee Mwinyi. Mzee Mwinyi Pamoja na kuendeleza mambo mazuri sana yaliyofanywa na Mwalimu Nyerere kuna baadhi ya mambo alifanya maboresho na marekebisho na ndiyo maana tukaenda vile tulivyokwenda. Alipomaliza mzee Mwinyi akaja mzee Mkapa akaendeleza mambo mazuri yaliyofanywa na mzee Mwinyi na akafanya baadhi ya maboresho na marekebisho pamoja na ndoto zake lakini tukasonga mbele na yale mazuri ya mzee Mwinyi na marekebisho aliyoyafanya mzee Mkapa tukasonga mbele nchi yetu ikapiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, akaja mzee Kikwete pamoja na ndoto zake za chama na mengine lakini alifanya baadhi ya marekebisho kwenye yale yaliyotokea wakati wa mzee Mkapa. Akaja Dkt Magufuli Awamu ya Tano amefanya mambo makubwa lakini alifanya marekebisho makubwa sana kwenye mambo yaliyotokea kwenye awamu zilizopita. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yale ndiyo yameipa heshima Tanzania yetu leo na tukamuunga mkono akafanya marekebisho na haikuwa nongwa hata kidogo. Amekuja Rais wa Awamu ya Sita mama Samia pamoja na ndoto nzuri na muendelezo wa ndoto na amesema hadharani tutaendeleza yale aliyoaanzisha Dkt John Pombe Magufuli na sidhani kama kuna mtu anataka haya mambo yaachwe kama yako mahali ni marekebisho madogo madogo ambayo yanafanyika vizuri na mama Samia ameanza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Awamu ya Sita pia kama zilivyo fanya awamu zingine ataendeleza ndoto lakini kule ambako anapaswa kufanya maboresho ili mambo yatekelezwe vizuri nadhani tumpe ushirikiano ayafanye hayo maboresho. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee Mwinyi alituambia kila zama na kitabu chake zama za Mwalimu zili kuwa na kitabu chake, zama za mzee Mwinyi na kitabu chake, na wakati huo mzee Mwinyi alifanya marekebisho makubwa na haikuwa rahisi kutoka kwa mwalimu amekaa miaka 24 anakuja mzee Mwinyi anafanya marekebisho haikuwa rahisi na wakati mwingine anafanya marekebisho mbele yake anasema ruksa tumevutana na *IMF* sasa tukae mezani haikuwa rahisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mzee Mwinyi akatuambia kila zama na kitabu chake, tumekuwa na vitabu vitano sasa tunaandika kitabu cha sita wito wangu kwa viongozi Wabunge wenzangu wana CCM na watanzania tumsaidie

mama kwa kumuunga mkono aandike kitabu cha awamu ya sita, tusigombane bila sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni yetu sote tumsaidie mama na yeye aandike kitabu chake tusimshike mikono kumwandikia kitabu tumuache aandike kitabu chake na ndugu zangu *legacyhaitetewi legacyinajitetea* yenyewe na hasa ile inayofanywa na mtu kama Dkt. Magufuli *legacy* yake itajitetea itajisimamia kwa miaka *unless* mtu ana mashaka na *legacy* yake lakini kama hamna mashaka na *legacy* yake *legacy* yake itasikilizwa itasemwa itaombewa na sisi watoto wajukuu na vitukuu kwasababu haya aliyoafanya watayakuta tu hatuna sababu ya kugombana hatuna sababu ya kutoana macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa kiongozi kwenye chama nimesimamia Idara ya Maktaba na Nyaraka duniani kama kuna chama bora kime-document mambo mengi ya kutosha CCM ni karibia namba *one* kwa kila kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye *document* zetu tumesema kujikosoa na kukosoana ni silaha ya mapinduzi na kujiimarisha na siyo dalili ya udhaifu chama chetu Kimeenda namna hiyo kwa miaka ya kutosha...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nape kengele ya pili imeshagonga ahsante sana nimeambiwa na katibu hapa

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Serikali kwa uamuzi kwa uamuzi wa kuondoa *TMX* nendeni mkasimamie okoeni zao la korosho na ufuta hongereni kwa uamuzi huo ahsanteni sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati atafuatia.

MHE. JULIANA D. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba hii ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sote tunafahamu kwamba kuna ongezeko kubwa sana nchini la mashine za kamari almaarufu kama beting za kachina na mashine hizi zinafungwa sana kwenye mikusanyiko ya masokoni, kwenye vituo vya daladala, vituo vya taksi bajaji na bodaboda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine hizi za kamari sasa hivi zinaingizwa hapa nchini kama *spear parts* na zinakuja kuwa-*assembled* hapa hapa nchini kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba TRA haina idadi Kamili za mashine hizi za kamari ambazo zipo nchini. Hii inawezesha *TRA* kukosa mapato yake kihalali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine hizi za kamari zipo hapa nchini kwenye maduka mpaka ya Mangi ambazo *TRA* kule kwenye maduka ya Mangi hawana ofisi zake. Kwa hiyo, inashindwa kuhakiki na inashindwa kukusanya kodi zake ipasavyo ninaushauri kwa Serikali kwenye suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba Serikali ifanye uhakiki upya wa kutoa leseni kwenye mashine hizi za kamari leseni kwa mashine moja moja mashine moja inapewa leseni moja hii itasaidia Serikali kupata idadi kamili za mashine zilizopo lakini na kukusanya kodi yake ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sote tunajua kama kamari ni kitu haramu na baadhi ya nchi haziruhusiwi kabisa lakini naomba kushauri Serikali pia kuweka sheria kali ambazo zitamlinda kijana zitamlinda mtoto mwanafunzi siyo tu wanavyosema kuanzia miaka 18, ningeshauri Serikali iweke hata kuanzia miaka 25 kwasababu kijana wa miaka 18 bado hajaweza kujipambanua na wanaingia kwenye huu mtego wa kamari hizi tunaenda kupoteza nguvu kazi ya Taifa. Unakuta mwanafunzi sasa hivi haendi darasani anatoka nyumbani anaenda shule lakini anaishia hapo katikati kwenye kucheza hizi kamari. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili suala kwa umakini zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaona kuna haja ya kuendeleza hii kamari za mtaani lakini haikusanyi kodi

yake ipasavyo. Kwa mwezi *TRA* inawatoza hawa wafanyabiashara ya kamali shilingi 100,000 lakini wao kwa siku wanafunga Sh.300,000 mpaka shilingi 700,000 na kwa mwezi wanafunga shilingi 9,000,000 mpaka Sh.21,000,000. Napenda kuishauri Serikali iangalie suala hili kwa makini zaidi, kwanza ni vitu ambavyo vinaenda kuharibu vizazi vyetu huko nje, kwa hiyo, kama kodi wa wachatozwe kodi kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Waziri wa Fedha, nakumbuka jambo hili liliwahi kuzungumzwa siku za nyuma pia. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali iangalie namna ya kutoa elimu kwa sababu kuna watu wanaingia huko hawajuwi madhara yake. Madhara yake ni makubwa sana, kuna watu wanapata hasara sana kwenye vitu hivyo, wanaopata faida ni wachache. Hakuna mtu anayendesha kamari ili yeeye apate hasara, hayupo. Wanaofaidika ni kama asilimia 1 kwenye mia moja, kwa hiyo, tuangalie namna ya kuelimisha vijana wetu lakini kuelimisha umma kwa ujumla kuhusu mambo haya.

Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Selement Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, ajiandae.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo kwa kweli imesheheni vipaumbele vyote vitakavyokwenda kurekebisha uhalisia wa maendeleo ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa mtumishi wa CCM kwa muda mrefu sana na nimepitia nafasi mbambali mpaka hapa nilipofikia. Hapa niliposimama inawezekana nikazungumza nitakayoyazungumza sitoweza

kusahau au sitaweza kumsahau Hayati John Pombe Magufuli. Hata hivyo, siyo tu Hayati Magufuli, tunao viongozi ambao wameondoka wako mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka wakati Sokoine anafariki takribani zaidi ya miaka ya 10 hakuna *impact* yoyote ambayo ilikuwa inaonyesha kwamba tumkumbuke kwa matendo yake. Tulikuwa tunasikiliza kwenye asasi mbalimbali wakiwa wanatukumbusha wanasiasa na Serikali jinsi ya kuenzi viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri Hayati Magufuli amekuwa ni kiongozi bora Barani Afrika na ni kiongozi ambaye Marais wa Afrika walikuwa wanatamani kuiga mifano yake. Sasa ikitupendeza pale Morogoro *roundabout* twendeni tukaweke picha yake. Kwa *legacy* ambayo amelacha Hayati Magufuli na kama Bunge hilli kila Mbunge anayesimama anamzungumzia na sisi tufike mahali sasa tuwaonyeshe Watanzania kwamba tunamuunga mkono kwa vigezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze mdogo wangu Mheshimiwa Bashe. Tulipokuja Disemba kuapa nilikaa naye hapa kantini lakini nilimueleza kuhusu zao la korosho na *TMX*, namshukuru sana amekuwa msikivu na alituelewa watu wa Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Wabunge wengine wakajua *TMX*. Kule kwangu Mtwara zao kubwa la biashara ni korosho. Nilikuwa nasoma kwenye ripoti yao wanasema watakuja kuwa madali lakini udalali wao korosho zetu zitanunuliwa *online*. Makampuni yote ya korosho ambayo yako Tanzania hususani Mtwara, yana wazawa na matajiri wengine wapo Vietnam, India na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia *TMX* kufika mahali wao wakala *number one*, kinachotokea ni nini? Ni kwamba mfanyakia biashara aliyeajiriwa yuko Mtwara tayari atakuwa amepoteza ajira kwa sababu korosho zitakuwa zinanunuliwa *online*. Kampuni ambayo iko India na iko

Tanzania na hapa kuna wafanyakazi, kama wako 20 watapunguzwa atabakia mfanyakazi mmoja. Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa kuwa wasikivu na kukubaliana kwamba *TMX*sasa ifike mahala ikae pembedi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimshukuru Waziri wa Maji. Waziri wa Maji alinitembelea Mtwara kuja kuangalia chujio na nikamueleza shida ya Mtwara siyo chujio ni maji na Serikali ikiweza kutupatia maji ya Mto Ruvuma tatizo la maji litakuwa limekwisha. Pia nikamueleza Waziri wa Maji kwamba mabomba yanayotumika hususani kwenye Jimbo la Mtwara Mjini yalifungwa na mkoloni, ni ya chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata leo kama mtaweka chujio likawa linafanya kazi lakini linapita kwenye bomba ambazo zina kutu. Kwa hiyo, maji yale hayatakuwa na usalama, yataendelea kuwa na ukakasi na chuma. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Maji atusaidie kwenye mpango wake kwa sababu ameshafika mahala amesema kwamba atatutengea fedha na upembizi yakinifu utafanyika basi hilo naomba alisimamie kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tumekuwa tunazungumza ajira za vijana, kweli hili ni janga la kitaifa. Sisi Wabunge wa Mkoa wa Mtwara tuna maeneo mengi sana ya mapori na yanahitaji kufanyiwa kazi kwenye suala la kilimo lakini hatuwezi. Hii ni kutokana na jinsi tulivyowaandaa vijana wetu kwenye familia zetu hawawezi ku-*compete* na kwenda shamba kulima bila Serikali kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano, leo tunawatibusi vijana ambao wanakula madawa ya kulevyia kwa gharama kubwa sana lakini tunapeleka asilimia 10 kwa ajili ya vijana, akina mama na wale mavu, twende sasa na mpango endelevu, wapo vijana wako tayari kwenda kulima shambani lakini Serikali ichukuwe hatua sasa ya kuwawezesha vijana hawa tuwapeleke mashambani wakalime kilimo cha kisasa ili sasa tuweze kutoa ajira zingine mpya tofauti na zile ambazo tunazungumza.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele ya pili imeshagongwa.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima na Mheshimiwa Masache Kasaka ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu lakini niseme Ramadhan Kareem kwa Waislam wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri Mkuu na Mawaziri wote waliooko katika Wizara yake bila kumsahau Mheshimiwa Jenista Mhagama. Kwa kweli wananchi wa Iringa wanasema kwamba mambo makubwa yaliyofanyika katika Mkoa wetu wa Iringa hatuwezi kumsahau Dkt. John Pombe Magufuli. Amefanya mambo makubwa ambayo hata kuyasimulia tunashindwa. Wameniambia niseme tu neno moja, *gendelage ludodi baba, gendelage ludodi, Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wote waliochangia kuhusu *TARURA* kupatiwa fedha za kutosha. *TARURA* ndiyo ambayo inahudumia barabara nydingi sana za vijijini ambazo ndizo zina matatizo mengi. Kwa mfano, Mkoa wetu wa Iringa mtandao wa barabara za *TARURA* ni karibu kilometra 4,597.9 na una mvua nydingi sana, milima, maporomoko, hivyo, *TARURA* inatakiwa iwe na pesa nydingi kwa ajili ya kujenga madaraja, makalvati kwa sababu barabara nydingi zimeharibika. Hizi barabara ni za kiuchumi zinapitisha mazao ya misitu ambapo magari ni mazito

yanafanya barabara hizi zinakuwa hazipitiki wakati wa mvua.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitende haki, nitaje baadhi ya barabara ambazo sasa hivi hazipitiki. Katika Wilaya ya Mfindi kuna hii barabara Mtiri – Ifwagi - Mdabulo - Kilosa haipitiki kabisa. Kuna barabara ya Ibwanzi – Lulanda; Nyololo – Mtwango; Mafinga - Mgololo, hizi barabara Mufindi wanapata mteso makubwa mno. Ukienda kwenye Wilaya ya Kilolo kuna barabara ya Boma la Ng'ombe – Jingula. Kata ya Masisiwe, kuna Kata ya Nyanzwa, Kijiji cha Mahenge na Magana kuna madaraja mawili yamekatika kiasi mtandao wa barabara hakuna kabisa. Ukienda katika Jimbo la Kalenga kuna barabara ya Lumuli – Magungu – Magulilwa - Nyenza, hizi barabara ni mteso makubwa sana kwa wananchi wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda kuwatembelea wakwe zangu kule Mwanza nilikuta kuna barabara pale llemela za VETA – Igombe TX; Airport - Nyagugi kama kilometra 18, toka nimeolewa bado hazijafanyiwa kazi yoyote. Naomba Waziri atusaidie kuziangalia barabara hizi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu walimu wanaohitimu katika vyuo vyetu vya elimu. Tunao walimu ambao kwa kweli wamekuwa wakijitolea mara nyingi hasa katika Mkoa wa Iringa hata katika maeneo mengine lakini zinapokuja ajira hawaajiriwi. Pamoja na kuwa Mkoa wetu wa Iringa umefanya vizuri sana katika elimu, tumekuwa tatu bora na hawa walimu wanachangia kwa sababu wamekuwa wanajitolea kwenye masomo ya sayansi na hisabati. Niombe Serikali iwave kipaumbele, hii itasaidia hata wengine kuwa na moyo wa kujitolea hata kama wamemaliza masomo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze pia kuhusu watu wenyе ulemavu. Nishukuru Serikali kwamba imetoa ile sheria kwamba watu wenyе ulemavu angalau kila mtu aweze kupata ile asilimia mbili. Hata hivyo, kuna wamama wengi

ambao wamezaa watoto wenye ulemavu ambao kwa kweli wanapata matatizo makubwa sana kuwalea wale watoto kwa sababu wengi wamekimbiwa na waume zao unakuta wao ndiyo wanahudumia wale watoto kuanzia masomo na malezi. Niombe labda ile asilimia mbili na wenyewe wangepatiwa ili hawa watoto waweze kusomeshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni uhaba wa watumishi katika sekta ya afya. Vimejengwa vituo vya afya na hospitali nzuri sana ila kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi katika sekta ya afya. Nikichukulia tu mfano Kilolo tuna hospitali ya mfano, ni nzuri sana na imeshakamilika lakini kuna upungufu wa watumishi 93. Wilaya hii kwa ujumla ina upungufu wa watumishi katika sekta ya afya kwa asilimia 40.

Niombe kwamba tunapokamilisha hivi vituo vya afya basi iendane na kukamilisha kabisa watumishi kwa sababu bado unaona wananchi wanapata shida sana kwenda kutafuta huduma wakati tayari tumeshajengewa vituo vya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu wazee. Wazee ni dawa na baraka lakini wamekuwa na changamoto nyingi sana. Niombe Serikali iangalie changamoto za wazee. Hata leo imezungumziwa kuhusu matibabu ya wazee na nishukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kwenye kongamano la afya za wazee katika Mkoa wetu wa Iringa na wanakushukuru sana. Lile kongamano lilifanya tukajua changamoto nyingi za wazee, wazee hawahitaji dawa wakati mwininge wanahitaji kuangaliwa wajijue kwamba wanahitaji kula lishe, kufanya mazoezi au faraja. Wazee wengi sasa hivi wameondolewa kulipia kwenye nyumba zao lakini bado wanalipa kodi ya ardhi. Naomba pia ile kodi ya ardhi itolewe kwa sababu tumeshawaondolea kulipia kodi ya nyumba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Bima ya Afya labda sasa izingatie ili wazee wetu waweze kutibiwa, kuchekiwa afya ya macho na vipimo vyote. Pia wanahitaji kupewa

dawa lakini hazitoshi na leo lile swalí limeeleza mambo makubwa sana kuhusu wazee. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nizungumzie kuhusu matatizo ya maji kwenye Mkao wa Iringa. Nishukuru sana kwamba Wizara ya Maji inafanya vizuri sana mijini lakini bado vijijini wamama wengi wanapata shida. Mkao wetu wa Iringa una mito mingi; Mto Lukosi, Mto Ruaha ila kule vijijini maji hakuna. Ni kwa nini wasivute maji ili wananchi wa Iringa wapate maji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mama Samia, kwa kweli akina mama tunaweza na tunashukuru baba yetu alimteuwa akawa Makamu wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati muda wako umeisha.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakupa *big up*, naunga mkono hoja. (*Makofí*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Ask. Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Kasaka na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa, ajiandae.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nikushukuru sana kwa kunipa muda ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwaambia ndugu zangu Waislamu wa Jimbo la Kawe na Waislam wote wa Tanzania nzima kwamba *Ramadhan Kareem* na *Ramadhan Mubarak*. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa makusudi ya kuokoa muda, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampa pole kwa kuondokewa na aliyekuwa Rais wake ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba uniruhusu kwa sababu huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhan, nianze hotuba yangu kwa kunukuu andiko moja kwenye Maandiko Matakatifu. Kitabu cha Hosea 4:6 inasema hivi: "Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa". *The English version says: "My people are destroyed for lack of knowledge".* Pia andiko hilo hilo limeandikwa kwenye Kitabu cha Methali 29:18. Kitabu hiki killandikwa na Suleiman Bin Daudi, Mfalme aliyewahi kuishi miaka mingi iliyopita, alisema hivi: "Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maono". Kiingereza chake, anasema: *"My people are destroyed for lack of vision"*. Kwa hiyo, tunapata ujumla kukosa maono kunaangamiza na kukosa maarifa kunaangamiza; *lack of vision destroys and lack of knowledge as well as destroys*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa nimesema hayo? Kwa sababu nimekuwa nikijuliza sana, kwa nini nchi zetu za Kiafrika na Taifa letu likiwemo, haziendi kwa *speed* ya maendeleo kama inavyotakikana. Ukiangalia *resources* ambazo zimo ndani ya Bara la Afrika na nchi yetu, hazihusiani na *speed* ya maendeleo ambayo Waafrika na Watanzania tuko nayo. Kwa nini? Nimekuwa nikiangalia, kwa mfano, asilimia 91 ya *reserve* ya almasi duniani inatokea Bara la Afrika; na asilimia 64 ya dhahabu duniani inatokea Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi, kwenye nchi yetu tuna dhahabu, tuna almasi, ambavyo ni *precious stone*, pia tuna *Semi-precious Stone*, tuna *Ruby, Emerald, Green Garnet, Aquamarine, Honey Color Opal, Black Opal, Rhodolite, Moon Stone*, tuna madini ambayo unaweza kuyataja mpaka

ukaimaliza dunia yote yako ndani ya nchi yetu ya Tanzania, lakini hatuendi kwa *speed* inayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegundua jambo moja. Jambo la kwanza, *natural resources* haiwezi kufanya kazi yenye *wala* bila *human resource*. Unapokuwa na madini, lazima uwe na akili ya kuyageuze madini hayo kuwa barabara, maji au umeme. Kwa hiyo, naweza kusema basi, *human resource is superior to natural resources*, kwa sababu unahitaji binadamu ili ageuze hizi *natural resources* kwenye maisha kamili ya watu ya kila siku. Nikaona hili ni tatizo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ambalo nataka kuliongelea kwa dakika zangu hizi chache, Tanzania tunashindwa kuendelea mbele kwa kasi kwa sababu hatuna mwendelezo wa *regime* moja kutoka *regime* nyiningine. Ni kana kwamba Mheshimiwa Nape Mbunge wa Mtama alikuwa amedukua hotuba yangu; sijui kama ni mtalaam wa *Itau* hapana, kwa namna nyiningine nafikiri ama aliona maono ama alifanya udukuzi fulani ambao nitaufuatilia baadaye. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema ni hiki, hebu tuone; Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwl. Julius Kambarage Nyerere, alitawala kwa miaka 24. Wakati anamaliza utawala wake, aliacha viwanda 411 vinafanya kazi. Unaweza kuvitaja, Kiltex, *Musomatex Mwatex Sunguratex*, you can name vyote, viwanda vilikuwa vinafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuja Mheshimiwa Rais wetu wa awamu ya pili kama alivyo sema Mheshimiwa Nape ali-*improve* baadhi ya mambo, lakini hakuendelea na wazo la viwanda, palikuwa kimya. Akaingia Rais wa tatu, viwanda vilevile vilivyoachwa na Mwalimu badala ya kuviendeleza, akaanza kuvibinafsisha vikauzwa vyote vikaondoka. Kwa hiyo, hakuna muunganiko kati ya *regime* ya kwanza na *regime* ya tatu. Tutakesha kama hakuna muunganiko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haikutosha, amekuja Rais nne ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kiwete ambaye hatukumwona akishughulika na viwanda hata kidogo, tulimwona akishughulika na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukamwona Rais anayefuata, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, tena anasema, "Tanzania ya Viwanda." Viwanda vilevile ambavyo Mzee Mkapa alivibinafisha na kuviuza, huyu tena anasema Tanzania ya Viwanda. Hapo ndipo tunaanza kupambana tena kuanza viwanda wakati viwanda vimebinafisha, vimeingia mikononi mwa watu binafsi, nao awajajenga viwanda bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikagundua jambo moja ambalo napenda niliseme. Kila Rais aliyeingia madarakani ali-*perform* vizuri *colorful* kwa namna yake; Mwalimu Nyerere ali-*perform* vizuri sana kwa namna yake; Mwinyi ali-*perform* vizuri sana kwa namna yake; Mkapa ali-*perform* vizuri sana kwa namna yake; Mheshimiwa Jakaya Kikwete ali-*perform* vizuri sana kwa namna yake; Mheshimiwa Magufuli aka-*perform* vizuri sana kwa namna yake; naamini na Mheshimiwa Samia ata-*perform* vizuri sana kwa namna yake pia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, namna zao hizi, kama kila mtu ana namna yake, unategemea nchi itaendeleaje? Kwa sababu kila mtu ana namna yake; na namna ya mmoja ni kinyume cha namna ya aliyetoka. Tutaendaje kama namna hizi hazifanani? Hii inanipelekea kusema, ili tuendelee, tunahitaji agenda ya pamoja ya Taifa lote. Kwa namna gani tu-*define* maono ya Tanzania ya miaka 30 ijayo. Inaweza ikawa miaka 30 au miaka 50, tuwe na vitu ambavyo sisi Watanzania tutaviita maendeleo. Siyo lazima vitu hivyo viitwe maendeleo Marekani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ujenzi wa maghorof siyo maendeleo kwetu. Tunaweza kusema maendeleo kwetu ni kila Mtanzania awe na maji safi na salama. Tunaweza kusema maendeleo kwetu; kila Mtanzania

mwenye uwezo wa kusoma shule, asome Chuo Kikuu na amalize, asiwepo asiyesoma Chuo Kikuu. Tunaweza kusema maendeleo kwetu sisi, wafanyabiashara wafanye biashara vizuri, tuwe na *export*. Tunaweza kutafsiri maendeleo tunayoyaita maendeleo katika nchi ya Tanzania na tukaacha kutafsiri maendeleo kutumia jukwaa la Wamarekani au watu wa Ulaya, tukaamua kuwa na miaka 50 ya kile ambacho sisi tunaamua kuki-*achieve* kama maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila Rais anayeingia madarakani, aingie kutimiza kwa namna yake na kwa sarakasi yake vile vitu ambavyo sisi tumevitafsiri kama maendeleo kututimizia kwa namna yake. Kama hatutafanya hivi, tuna hatari. Kwa sababu Katiba yetu inampa nafasi kila Rais anayeingia madarakani kwa namna yake, kwa hekima yake na kwa namna anavyotafasiri yeye maendeleo awaletee maendeleo Watanzania. Siku moja tutakapopata Rais ambaye hayuko sawasawa, tutaishia kulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ombi langu sasa kwa dakika chache hizi, naomba ikiwa ni nia yetu tuendelee, tuwe na *vision* ya miaka 50 ya Taifa na hii *vision* tuitafsiri, tuseme *vision* yetu ni kila mmoja apate maji, kila nyumba iwe na umeme, asipatikane Mtanzania anayekaa kwenye nyumba ya majani; tu-*define vision* yetu. Halafu tunasema, inapoingia *regime*, inapoingia Rais, lazima ilani ya chama chake izungumze mambo ambayo sisi tumejiwekea kama maono ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano. Patakapotokea Rais akaanza kufanya mambo yake ambayo hayako ndani ya ilani, kuna mtu wa kumwuliza hapa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Amirijeshi Mkuu kwamba hutakiwi kufanya hayo? Hayupo! Tutakapokuwa na *vision ambayo* imewekwa kwamba tunahitaji ku-*achieve mambo* kadha wa kadha na kila *regime* inapoingia, iwe ya kijani, ya *blue* au ya namna yoyote, itatimiza yale ambayo tumejiwekea kama maendeleo kwetu na maono ya Taifa letu. Tafuta sarakasi zako ama kwa ukali, ama kwa nguvu,

ama kwa namna yoyote, ilimradi yale maono tuliyojiwekea kama Taifa yatokee kwa haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. Nasema tena, katika jina la Mwenyezi Mungu *Subhan-huwa-taallah* na katika jina la Yesu Kristo na katika jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima. Mheshimiwa Masache Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Nailbu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia na Watanzania kutokana na kifo cha Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. Pia nampongeza Rais wetu wa Awamu ya Sita, mama yetu Mheshimiwa Samia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba hii nzuri ambayo nitapenda kujikita kwenye Sekta ya Madini. Kama ambavyo tunajua, Serikali ya Awamu ya Tano wakati inaingia madarakani ilirekebisha mazingira ya uchimbaji na tukaweza kutoka pale tulipokuwa na kupata mapato kutoka shilingi bilioni 150 mpaka kufikia takribani shilingi bilioni 550, kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi watu wa Wilaya ya Chunya tuliweza kutoka uzalishaji wa kilo 20 kwa mwezi mpaka sasa hivi tunafika kilo 230 kwa mwezi. Haya ni mafanikio makubwa ambayo yanaweza kupelekea kulipa kodi. Mwanzoni wakati Serikali Awamu ya Tano inaingia madarakani tulikuwa tunalipa kodi ya shilingi milioni 150, lakini sasa hivi tunaweza kulipa kodi zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa mwezi. Haya ni mafanikio makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima twende mbele zaidi, tusiridhike na hapa tulipofika. Ili tuweze kwenda, kuna sheria mbalimbali ambazo kubadilishwa; na moja kati ya sheria ambazo zimebalishwa iliweza kuwataka wale wanaofanya utafiti kwenye madini, kuhakikisha majibu ya tafiti zao yanapelekwa kwenye Taasisi ya Jiolojia (*GST*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wetu ni nini? Ushauri wetu ni kwamba zile tafiti ambazo zimeshapelekwa *GST*, zinyambuliwe katika lugha nyepesi ambapo wachimbaji wetu wazipate na kuweza kuzitumia ili uchimbaji wao sasa ufanyike vizuri. Badala ya uchimbaji huu wa ramli unaofanyika kwa wachimbaji wadogo, itatuwezesha sasa kupata mapato mengi zaidi na mapato haya yatasaidia kuongeza wigo wa mapato ya Serikali na kuleta mapato makubwa zaidi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa *GST*hawa wenzetu, bado ofisi zao ziko Dodoma. Nchi nzima huku tukitaka kupima viwango vyetu vya madini, ni lazima tuje Dodoma. Nashauri sasa kwa Wizara kuhakikisha kwamba washuke chini zaidi kwenye *level* ya kanda ili *GST* wawepo kwenye kanda na wachimbaji wetu wadogo wasifunge safari kutoka Chunya kuja Dodoma, waishie kwenye kanda. Hiyo itaweza kutusaidia sana. Ni imani yangu kwamba Serikali itawasaidia wachimbaji wadogo na uzalishaji wao kuongezeka zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee pia kwa upande wa kodi. Kwa sisi wachimbaji wadogo, kodi imekuwa siyo Rafiki. Tunaomba Serikali iangalie namna gani ambavyo itaweza kutusaidia. Leo hii kwa mchimbaji huyu anaweza akapata leo kiasi cha shilingi milioni 50, lakini akiipata leo, inawezekana mwaka mzima asipate tena. Sasa nini cha kufanya? Namna nzuri ya kufanya na kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo, tuone namna bora zaidi ya kubadilisha sheria, ili wakati ambapo mchimbaji anaenda kuuza madini yake na kodi hii aweze kukatwa pale pale; kama ambavyo kodi hii inakatwa kwenye mrabaha wa 6% na *inspection fee* 1%, unapouza unakatwa pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia yale malalamiko tuliyonayo wafanyabiashara na wachimbaji wetu kwa akaunti zetu kufungwa na *TRA*, hili suala halitakuwepo. Maana nikienda kuza madini yangu, pale pale nitakwa na kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itawasidia wachimbaji wetu. Kwa kauli ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Mama yetu Samia amesema tusifungiwe akaunti. Kwa hiyo, akaunti za wachimbaji hazitafungwa na sheria hizi zikibadilishwa, hawataweza tena kupata matatizo yoyote ya kikodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaloweza kulielezea ni namna ambavyo ile *Service Levy* tunavyoilipa kwenye Halmashauri. *Service Levy* tunayolipa kwenye Halmashauri ni asilimia 0.03, ndivyo wachimbaji wanavyoilipa. Sasa kwa maeneo ya Wilaya, kama Wilaya ya Chunya ambako ndiko tunakochimba madini, tunalipa kodi zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa mwezi, lakini malipo yanayobakia kwenye Halmashauri ni asilimia 0.03. Ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuona namna bora zaidi ya kubadilisha hii sheria angalau kiwango hiki sasa hivi kiweze kupanda kutoka 0.03% iweze kwenda 1% au 2% ili mapato mengi yaweze kubaki kwenye Halmshauri zetu kule ambako wachimbaji wanafanya uchimbaji huu. Hiyo itaweza kusaidia haya matatizo madogo madogo tunayokimbizana nayo sasa; ya madarasa, madawati na kadhalika, kile kiwango ambacho tunakipata kitaweba kufanya kazi vizuri zaidi kwenye Halmashauri zetu kule na Serikali haitakimbizana na hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, naiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu na ninampomgeza sana Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kukushukuru. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa anayoendelea kutupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amekuja na hotuba ambayo ni dhahiri inakwenda kutimiza yale ambayo chama chetu kimelekeza Serikali katika awamu hii kupitia ilani yetu ya mwaka 2020 - 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya sijasema niliyodhamiria, nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu kutoka Jimbo la Mtoni ambapo mvua zinazoendelea kunyesha kule Zanzibar, baadhi yao kupitia Shehia ya Sharifu Musa Zone ya Chemchem B, wamepata athari ya Kingiliwa na maji katika majumba yao. Nitumie nafasi hii kuziomba mamlaka zenyenye dhamana katika Serikali ya Zanzibar na katika Jimbo letu la Mtoni waone namna gani watakwenda kuwasaidia wananchi wale ili tatizo lile liwaondoke na lisijirejee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Waziri Mkuu, napenda nichangie suala la umeme. Ni vyema sana, nami nimefarijika kwa kweli nilipoona Serikali imeshalipa sehemu ya fedha za Mradi wa Bwawa la Umeme. Bwawa lile halina tija tu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania peke yake ama kwa wananchi wanayoishi Tanzania Bara, lakini bwawa lile pia litaleta faida kwa sisi tunaotokea upande wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nikumbushe, Kisiwa cha Unguja, kinapokea umeme kupitia waya uliotandikwa chini ya Bahari kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar na Kisiwa cha Pemba kinapokea umeme kutoka Tanga uliotandikwa chini ya Bahari hadi Pemba. Umeme ule unatoka katika Mamlaka ya Shirika la Umeme la upande wa Tanzania Bara, *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bwawa likichimbwa, umeme ukizalishwa, bei ikishuka, wananchi wa

Tanzania wakiwemo wananchi wa Zanzibar na Jimbo langu la Mtoni, watanufaika kwa bei ya umeme kushuka na kuboresha maisha yao. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hii na ninawatia moyo, sisi wananchi wa Tanzania na sisi viongozi tuko nyuma yenu katika jambo hili na tutawaunga mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipate fursa sasa ya kuzungumzia Mfuko wa Jimbo hasa kwa majimbo ya upande wa Zanzibar; mfuko ule wa kuchochaea maendeleo ya jimbo katika Bunge la Muungano. Fedha hizi zimekuwa zikiandaliwa, zimekuwa zikitolewa, lakini mpaka jana majimbo takribani yote ya Zanzibar hayajapokea fedha za Mfuko wa Jimbo katika majimbo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Serikali yetu imeshatoa hizo fedha, lakini yawezekana fedha zile zimekwama Ubungo. Kwa kuwa kuna *flyover*, sidhani kama kuna foleni tena; yawezekana fedha zile zimechelewa kupata boti, lakini kwa kuwa boti ziko nyingi, sidhani tena; lakini yawezekana fedha zile zimeelekezwa kabla ya kufika katika Mfuko wa Mbunge wa Jimbo, zikamsalimie shangazi, zimsalimie na mjomba na ziangalie kidogo uzuri wa binamu, halafu ndio ziingie katika Mfuko wa Jimbo. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ione namna bora fedha hizi zitatoka na kama zitapita kumsalimia mjomba, kumsalimia shangazi na kuangalia uzuri wa binamu, lakini zifike kwa wakati katika majimbo yetu. Maana wananchi wa Jimbo la Mtoni wanazisubiri fedha hizo zikasaidie kutatta changamoto zinazowakabili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilivyoanza kuingia katika Majimbo yetu upande wa Tanzania Bara, nasi kwa kifua mbele tukaanza kujinasibu kwamba ile miradi ambayo imeibuliwa na wananchi; mfano katika Jimbo langu la Mtoni, wameibua mradi wa kujenga daraja ambao lingeweza kuwaunganisha watoto wavuke kwa haraka kutoka *school*, kutoka upande mmoja wa Shehia kwenda upande wa pili;

wameibua mradi wa kujenga jaa la kukusanya taka kwa muda kabla ya Manispaa kuja kuzichukuwa, wanachosubiri ni fedha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, wakati mambo haya yakiendelea kupangwa, jambo hili lizingatiwe sana. Hatuna tatizo na namna fedha zinavyopita, lakini zipite kwa haraka ili wananchi wa Jimbo la Mtoni na majimbo mengine ya Zanzibar waweze kujivunia hatua hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala la Muungano kwa namna ambavyo limezungumzwa katika hotuba ya Waziri Mkuu. Naipongeze sana Serikali yetu kwa namna ambavyo inaendelea kushughulikia masuala ya Muungano. Leo naomba nishauri pla namna nyingine ambayo labda ipo, lakini natamani iendelee kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za Muungano zipo nyingine kuzitatua kwake ni kuziondoa katika mambo ya Muungano; lakini zipo nyingine ambazo kuzitatua kwake ni kuziba mianya ile inayoleta changamoto na kuyaunganisha zaidi kwa mambo ya Muungano yaliyo imara zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa natolea mfano suala la mpira wa miguu. Natambua huko nyuma Zanzibar ilipata kuwa Mwanachama wa Mpira wa Miguu (*CAF*) Afrika. Baadaye kutokana na sheria za *CAF* na namna Muungano wetu ulivyo, ikashindikana. Sasa kwa nini tuendelee kufikiria kutenganisha baadhi ya mambo wakati ni muhimu tukaweza kuyaunganisha vizuri na yakaondoa changamoto hizo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali iendeleze nguvu katika kujitapa na kuyasema wazi yale mafanikio ya kimuungano, kwa sababu changamoto huwa zinasemwa sana na wakati mwingine zinataka kutuamisha sisi tuliozaliwa baada ya Muungano, kama vile Muungano una matatizo

mengi sana. Kumbe Muungano una raha nyingi sana. Muungano huu umetupa fursa Wazanzibari kutoka Zanzibar ambapo hakuna milima mikubwa mikubwa, tukafika Dar es Salaam, tukaona milima ya wastani ya Kisarawe, tukasogea Morogoro tukaona milima mikubwa mikubwa ya Ulugulu, tukasogea Kilimanjaro tukaona milima mikubwa sana ya Kilimanjaro. Hiyo ni moja ya raha na faida za Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano huu umewapa fursa ninyi wenzetu wa Tanzania Bara kuvuka maji na kwenda kushuhudia neema za Zanzibar zikiwemo *shadow* na poda nzuri zinazopakwa na wanadada wa Zanzibar. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, neema na faida za Muungano ni nyingi. Basi naiomba Serikali yetu, katika bajeti yake inavyoendelea kusema, iyataje waziwazi mambo ya Muungano ambayo yanafanya vizuri kwa faida ya kizazi chetu na kizazi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtoni, nashukuru sana na mimi naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Kuna Wabunge wameleta ujumbe hapa kwamba akina dada tutaambatana huko tukachukue zile poda, huko Mtoni. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ajiandae.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amewasilisha hotuba yake vizuri, hotuba ambayo imebeba matarajio makubwa sana, hasa kwa sisi vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda moja kwa moja kujielekeza kwenye hotuba, ukurasa wa 34 ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea kuhusu suala la uvuvi. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu amesema kwamba Serikali inakwenda kufufua Shirika la Uvuvi (*Tanzania Fisheries Corporation*), napenda kupongeza jitihada hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufufua Shirika hili la Uvuvi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongelea pia ujenzi wa bandari na ujenzi wa meli za uvuvi. Napenda sana kuongelea hapa; pamoja na kufufua Shirika hili la Uvuvi, pamoja na kujenga bandari hizi, pamoja na kujenga meli, lazima tuangalie Sheria yetu ya Uvuvi ya mwaka 2003 na kupitia upya Kanuni zetu za Uvuvi, bado si rafiki sana kwa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania tumebarikiwa sana kuwa na vyanzo vingi vya maji na wakati sisi tunasoma tulikuwa tukisoma kwamba Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maziwa yenye kina kirefu duniani na ni la pili kwa kina kirefu likiwa na kina cha kilometra 1.47. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitarajia sasa katika urefu huu wa kina cha Ziwa Tanganyika na umaarufu wake basi utuneemeshe sisi Watanzania, hasa tunaotokea Kanda ya Ziwa Tanganyika, lakini matarajio yetu yamekuwa ni tofauti. Najisikia vibaya kusema hivi lakini Ziwa Tanganyika tumesahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza kabisa tunaona kwamba sekta ya uvuvi hii kama ingewekezwa vizuri ingeweza kutengeneza ajira nyingi sana kwa vijana. Wizara hii ya Waziri Mkuu ni Wizara ambayo inabeba dhamana ya kushughulikia ajira za vijana. Kwa hiyo niiombe sana Wizara hii ipige jicho mbele zaidi kuona namna ambavyo tunaweza kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi na tukaleta tija kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira limekuwa la kidunia, limekuwa suala la Kitaifa. Hatuwezi kutatua

changamoto hii nzito ya vijana kwa kutegemea asilimia nne za vijana. Kwa hiyo naomba Wizara hii itie nguvu katika sekta ya uvuvi, iwekeze katika vyombo nya kisasa nya uvuvi. Ni aibu mpaka leo Ziwa Tanganyika halina vyombo nya kisasa nya uvuvi; ni aibu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ajabu sana katika Kanuni zetu hizi, tunaona leo tunahamasisha vijana wajilingize katika uvuvi, wafanye biashara ya uvuvi, lakini sheria zetu bado ni kandamizi kwa vijana. Leo hii ukitaka kupata leseni ya kusafirisha samaki nije, kwanza kila aina ya samaki lazima uwe na leseni tofauti. Tafiti zilizofanywa na shirika la utafiti zimesema Ziwa Tanganyika lina aina zaidi ya 400 za samaki. Sasa leo ukitaka kusafirisha sangara uwe na leseni yake, ukitaka kusafirisha mgebuka uwe na leseni yake, ukitaka kusafirisha kuhe uwe na leseni yake; jambo hili ni kandamizi kwa wavuvi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika hili kutokana na utafiti uliofanywa, tumesema tuna aina zaidi ya 400 na katika idadi hii tuna samaki pia wa mapambo ambao wangekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa watalii wetu, lakini Wizara yetu ya Uvuvu ipo kimya. Niombe sana Wizara hii ya Uvuvu iwekeze katika utafiti, tujue hawa samaki wa mapambo tunanufaika nao vipi, hasa sisi tunaotokea Ukanda wa Ziwa Tanganyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na samaki hao wa mapambo, Ziwa Tanganyika hili lina samaki ambao wanaweza kuzalisha umeme na kwa utafiti uliofanywa ni hadi kufikia volti 900; ni umeme mkubwa sana huo. Niombe sana Wizara hii ya Uvuvu ijitahidi sana kuwekeza katika tafiti, maana tafiti hizi zimefanywa na zipo na Wizara inazijua na inazo. Kwa hiyo niombe sana suala hili liweze kuangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunajaribu kuongea na wavuvi, wana changamoto nyingi sana. Wavuvi wanafanya kazi katika mazingira magumu na hali ikiwa wenyewe ndio watu wa kwanza wanaotoa kura kwa Serikali hii. Wavuvi wametupatia kura nyingi lakini wamesahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza katika Kanuni zetu hizi za Uvuvi, leo hii mimi kijana nikitaka kujajiri kwenye sekta ya uvuvi, nikisema nataka kusafirisha samaki, kwanza Ukanda wa Ziwa Tanganyika hatuna maabara ya kupimia *sample* ya samaki. Lazima *samples* hizo tukazipime Mwanza na kipimo cha *sample* kwa mwezi kwa leseni moja, nimesema kila aina ya samaki ana leseni yake, leseni moja ni shilingi 150,000 kwa mwezi, kwa mwaka ni shilingi 1,800,000, hiyo ni kwa leseni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukiwa na leseni tatu au nne *imagine* itakuwa ni shilingi ngapi. Tunaua biashara ya vijana wetu, tunaua malengo na matarajio ya vijana wetu. Niombe sana Wizara husika waone namna ya kufanya ili hizi leseni ziwekwe pamoja. Niombe sana Wizara iingilie kat. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara hii ndiyo inasimamia ajira, lazima iwe na vivu na maeneo yote ambayo yanaweza yakatoa ajira. Lazima yenyewe iwe ya kwanza kushirikiana na hizi Wizara nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye kipengele kingine; wakati tunasema kwamba tutaanzisha viwanda ni wazi kwamba hatuwezi kuanzisha viwanda kama hatuna *raw materials*. Kwa hiyo lazima tuwekeze kwenye kupata malighafi ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi hizo. Sasa hatuwezi kuanzisha viwanda kama tumeshindwa kuwekeza kwenye malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 wakati wa ziara ya Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Mkoani Katavi, aliahidi kiwanda cha kusindika samaki. Mpaka leo Serikali iko kimya hatuoni dalili zozote na sisi vijana tunatamani maana tunajua kwamba kiwanda kile kikifunguliwa vijana tutapata ajira. Sasa leo zinatoka takwimu hapa kuna viwanda kadhaa, tunajiuliza hawa vijana wanaoajiriwa wako wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana Wizara husika, twendeni *site*, twendeni tukaongee na wavuvi, twendeni tukapokee kero za wavuvi ili sekta hii iweze kutupatia ajira nyingi za kutosha. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa hapa nilikuwa najiuliza; mvuvi mwenye leseni ya mgebuka halafu akavua kuhe, anamrejesha ziwani ama anaondoka naye? Hebu tusaidie hilo.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni leseni ya kusafirisha, kama unataka ku-*export*.

NAIBU SPIKA: Sawa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray na Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nitajielekeza katika maeneo mawili ya lishe na sekta ya Asasi za Kiraia (*NGOs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa jithada kubwa ambayo imekuwa inaendelea kufanya katika kuboresha hali ya lishe nchini pamoja na kutokomeza udumavu na aina zote za utapiamlo. Kipekee kabisa napenda kutambua jithada kubwa alizofanya Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiwa Makamu wa Rais ambayo ilisababisha yeye kumuagiza Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais, TAMISEMI kusaini mikataba ya lishe kwa niaba yake na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa namna ambavyo wanaendelea kuratibu masuala ya lishe ambayo yanaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Wanafanya hivi kwa kupitia maeneo matatu.

La kwanza ni kusimamia utekelezaji wa mpango jumuishi wa lishe wa Kitaifa; la pili ni kusimamia vuguvugu la uongezaji kasi ya kuboresha hali ya lishe duniani; la tatu ni kujumuisha jumbe ya lishe katika jumbe za mbio za Mwenge wa Uhuru; na la nne latika kutekeleza viapumbele vyataga lishe vilivyoweka katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kipekee kabisa napenda kukishukuru Chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kuwa chama pekee ambacho kimeweka kipaumbele kikubwa katika lishe. Mnaweza mkaarejea kurasa za 7, 40, 139-141 ambapo Chama Cha Mapinduzi kimeweka malengo madhubuti ya namna gani itaelekeza Serikali kwenda kuboresha hali ya lishe nchini na kutokomeza udumavu na aina zote za utapiamlo. Waheshimiwa wanaweza kurejea Zaidi kwenye kurasa hizi nilizozitaja, kurasa za 7,40, 139-141. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tanzania tuna changamoto kubwa sana ya lishe duni inayosababisha kutuweka katika hatari ya kutokuwa na kizazi na nguvu kazi shindani. Wengi humu tunaongelea changamoto za ajira, lakini ikiwa watoto wetu wana lishe duni na wako dumavu hiyo nguvu kazi na kizazi cha kesho tutavipata vipi? Ndiyo maana ni lazima kutoa kipaumbele kwa ajenda hii ya lishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuikumbusha Ofisi ya Waziri Mkuu itamke rasmi ina maoni gani kuhusu janga hili la lishe bora. Ofisi ya Waziri Mkuu itakwenda kufanya nini kuhakikisha kwamba sekta na Wizara zote

zinazohusika na suala hili wanakwenda kutekeleza yale yaliyoandikwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo langu la pili la Asasi za Kiraia; napenda kuipongeza sana Serikali kwa wito wa utashi wa kushirikiana na sekta binafsi ili kukuza ustawi wa maendeleo ya jamii na uchumi wa Taifa letu. Hata hivyo, naomba nitumie fursa hii kuikumbusha Serikali kuwa kuna sekta nyingine ambayo nayo inaweza kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kuitambulisha Sekta ya Asasi za Kiraia kwa maana ya *NGOs*, *CSOs* na *CDOs* kwa sababu sekta hii ina sifa zote za kuwa chachu ya kuinua na kukweza dira ya mipango ya maendeleo ya Taifa. Nasema hivi kwa sababu hata kwenye Ilani hii ya Chama Cha Mapinduzi imetambua mchango mkubwa wa sekta ya Asasi za Kiraia, imetambua sekta ya Asasi za Kiraia ni muhimu katika kutekeleza mipango ya maendeleo. Mnaweza mkaarejea kurasa za 124 na 128 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, Chama Cha Mapinduzi ndicho chama pekee ambacho katika nafasi zake za Viti Maalum, kimetenga nafasi ya kuwa na Mwakilishi wa kundi la Asasi za Kiraia. Humu Bungeni niko mimi nikiwakilisha kundi la Asasi za Kiraia kwa upande wa Tanzania Bara, lakini pia yupo Mheshimiwa Khadija Aboud anayewakilisha kundi hili kutoka Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa *NGOs* kwa kazi kubwa inayofanya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya *NGOs* ya 2019 na kwa mara ya kwanza imeweza kuchakata na kubainisha ni kiasi gani cha fedha kinachoingia nchini kwa ajili ya sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miezi sita tu katи ya Julai, 2020 mpaka Machi, 2021, jumla ya mikataba 178 ilichakatwa na kufanyiwa upembuzi na Ofisi ya Msajili

wa *NGOs*. Iliweza kubaini jumla ya shilingi bilioni 546, narudia; katika kipindi cha miezi sita, Ofisi ya Msajili wa *NGOs* iliweza kubaini jumla ya 546,758,508,000 ziliingia nchini kupitia *NGOs*. Kwa hiyo moja kwa moja sekta ya *NGOs* ina mchango mkubwa sana katika kuendeleza Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa Ofisi ya Msajili wa *NGOs* na Baraza la Taifa la *NGOs*ili waendeleze kusimamia utekelezaji na uratibu katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, naomba nikiri kwamba awali nilikuwa na hofu juu ya maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto kumezwa na afya, lakini namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kulitambua hilo na kuweka Naibu Waziri anayesimamia Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ajira, Sekta ya Asasi za Kiraia inaajiri watu wengi. Kwa taarifa ya Wizara ya Afya, 2017, katika mashirika 300 tu yalichangia zaidi ya ajira 5,317. Vile vile sekta hii ya Asasi za Kiraia pia ni tanuru ya kuandaa viongozi wa Kitaifa. Viongozi hawa wa Kitaifa ni kuanzia Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa; Mheshimiwa Waziri, Profesa Kabudi; Mheshimiwa Waziri, Profesa Kitila Mkumbo; Mheshimiwa Waziri, Ummy Mwalimu; Mheshimiwa Waziri, Selemani Jafo; Mheshimiwa Naibu Waziri, Olenasha; Mheshimiwa Naibu Waziri, Ummy Nderiananga; Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Profesa Kilangi. Kwa hiyo hii moja kwa moja inaonesha kwamba sekta hii inatoa mchango mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali, vile ilivyowakaribisha sekta binafsi waandae mpango kazi na sisi pia sekta ya Asasi za Kiraia tupewe fursa kama hiyo tukaribishwe rasmi, maana tupo tayari kushirikiana na Serikali na tayari tunaandaa mpango kazi ambao tutapenda kuuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, kabla ya kwenda kumwona Mheshimiwa

Rais, Samia Suluhu Hassan, kama ambavyo nilishaomba awali.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, ndani ya Bunge hili tuko Wabunge wengi sana ambao tumepitia sekta ya Asasi za Kiraia. Hivyo, naona tunayo fursa ya kuanzisha kikundi cha Wabunge Vinara wa AZAKI kwa maana ya *NGOs*, *CBOs* na *CSOs* ili kuimarisha utekelezaji wa mwongozo, uhusishwaji wa Asasi za Kiraia katika shughuli za Kamati ya Bunge na huu ni mwongozo ambao umeandaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa fursa hii.
(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nami umenipa wazo, watu wakisimama humu ndani wengine wanajiita wanafunzi wangu, naona na mimi niandae kundi la wanafunzi wangu humu ndani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nishukuru kwa nafasi uliyonipatia niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nami niungane na wenzangu katika kuwashakikishia Watanzania kwamba nchi yetu ipo katika mikono salama ya mama yetu, Samia Suluhu Hassan. Matumaini makubwa Watanzania waliyonayo kwa mpendwa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, na kazi kubwa aliyokuwa ameifanya katika nchi hii, niwashakikishie kwamba Tanzania kamwe haitafutika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote linapozungumzia maendeleo au vipaumbele vya nchi katika maendeleo ya wananchi wake pamoja na kiuchumi, kamwe huwezi kuacha kuzungumzia suala zima la elimu. Mabadiliko ya mtaala wa

elimu 2005 yaliyofanyika yalisitsitiza Masomo ya Stadi za Kazi na TEHAMA yafundishwe kikamilifu katika shule zetu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masomo haya yalikuwa na nia kubwa sana ya kuwandaa wanafunzi wetu kutoka shule za msingi kupata stadi mbalimbali ambayo ingewawezesha wenyewe waweze kuja kupata maarifa, ujuzi ili waweze kuutumia katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masomo ya TEHAMA na Stadi za Kazi; haya masomo yanapofundishwa kikamilifu katika shule zetu wanafunzi hupata ujuzi mbalimbali. Mfano, Somo la Stadi za Kazi, kuititia somo hili leo hii somo hili lingekuwa limefundishwa kwa ukamilifu na watahiniwa wakafanyiwa mitihani ya kuwapima kama wamepata ujuzi na maarifa, tungekuwa na wasanii mbalimbali, wanamuziki, wachoraji, mafundi ujenzi na wapishi wallibobe. Kutokana na changamoto mbalimbali somo hili leo halifundishwi kikamilifu na limekuwa ni somo la *option*, kwamba kuna shule zinafundisha lakini kuna shule zingine pia hazifundishi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na somo la TEHAMA ambalo ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano basi niombe Serikali ione umuhimu sasa wa kuhakikisha kwamba haya masomo yanafundishwa kikamilifu katika shule zetu ili Watoto waanze kupata ujuzi katika umri ule wa shule za msingi na kuendelea. Hii itasaidia Watoto wetu wapate ujuzi na mwisho waweze kujitegemea katika maisha yao, ukilinganisha na kwamba sasa hivi tuna tatizo kubwa la ajira katika nchi yetu tukiwapatia taaluma hii Watoto wetu watapata maarifa na ujuzi wa kutosha ili waweze kusimama wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya nchi yetu ni elimu bure kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne na hii elimu ni haki sawa kwa watu wote. Naomba njikite kwenye elimu maalum kwa watu wenyewe ulemavu, pamoja na kwamba Serikali ni yenye jukumu la kuhakikisha kwamba watu hawa wenyewe ulemavu wanapata elimu stahiki na watu ambaeo hawana ulemavu lakini bado kuna changamoto nyingi mno katika utekelezaji wake. Na hii imesababisha

kwamba hata watu wale wenye ulemavu Watoto hawa hawapelekwi shule, imebidi wazazi sasa ukipata Watoto wenye ulemavu ni kuwaficha, hatimaye wale Watoto hawapati haki zao za kupata elimu hii inayotolewa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maeneo yale ambayo elimu hii hutolewa bado kuna changamoto nyingi mazingira yao si rafiki kwa Watoto hao kupata elimu, ikiwepo madarasa wanayotumia, ukosefu wa meza za kusomea, hata wale ambaao wenye uoni hafifu hawana lenzi za kusomea pamoja na vitabu vile ambavyo ni sahihi kwa ajili ya Watoto wale wenye ulemavu wa macho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe hawa Watoto ili waweze kupata elimu sawa kama Watoto wa kitanzania ni vema Serikali sasa ione ni namna gani kuweka karibu huduma hii ya elimu maalum katika maeneo yetu ikipendeza nishauri kwamba shule zetu za elimu maalum walau kila wilaya ipate shule maalum ili kila mtoto ambaye anapata ulemavu aweze kupata elimu hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii itaturahisishia kwamba hata walimu ambaao wamesomea elimu maalum sasa hivi wanapelekwa kwenye shule zetu za mchanganyiko ambaao hawana tatizo hilo la elimu ya watu wenye ulemavu. Walimu hawa watumike ipasavyo endapo tutakuwa na shule zenye elimu, watu wenye elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu hawa wakipelekwa kwenye shule hizo tunauhakika watafanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa mno badala ya kuwachanganya wale Watoto wenye uhitaji maalum na Watoto ambaao hawana uhitaji huo inasababisha kwamba yule mwalimu anapewa masomo mengi kufundisha Watoto wenye elimu maalum na wakati huo huo afundishe na masomo mengine. Utendaji wa mwalimu unakuwa mgumu na hivyo kufanya yule mtoto hawezи kufanya vizuri darasani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nigosie suala la Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule, huwezi kuongelea elimu bora kama huna udhibiti ubora wa shule. Idara zetu za Udhibiti Ubora wa Shule, niipongeze Serikali kwa kuwanunulia magari, kwa kuwajengea Ofisi, Ofisi zetu za Idara ya Udhibiti Ubora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo Ofisi hizi hufanya vizuri kwa upande wa shule za msingi tu. Ukiangalia shule zetu za msingi asilimia 90 wanakaguliwa. Lakini ukija kwenye shule zetu za Sekondari ni asilimia 30 tu ndo huwa hukaguliwa na hawa wakaguzi wa udhibiti ubora. Hivyo, huchangia kwamba shule zetu nyingi hazikaguliwi katika shule za sekondari hivyo basi, inasababisha kutogundua mapungufu yaliyopo kwenye elimu kule shule za Sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii inachangiwa kwamba hawa watu wa udhibiti ubora wako ngazi ya kanda sasa ngazi ya kanda kuna kanda zingine sina mikoa miwili kuna kanda zingine zina mikoa mitatu. Sasa mfano mkoaa wetu wa Manyara ukiangalia kanda ya Kaskazini Mashariki tuna mikoa miwili, leo hii Mkaguzi wa Kanda akague mikoa miwili kwa maana Manyara na Arusha, Mkaguzi huyo atoke Arusha aende mpaka vijijini na hivi sasa hivi katika kila kata kuna shule ya sekondari, lakini mkaguzi huyo huyo alioko kanda akague shule za sekondari zilizopo kwenye kata zetu, kwanza anatembea umbali mrefu sana kwenda kukagua shule zetu lakini pia wanatumia gharama kubwa kwenda kufanya kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nishauri Serikali sasa ione umuhimu wa kuanzisha Ofisi zetu za Udhibiti Ubora kwa kila mkoa ili hawa watu huduma zao ziwe karibu na waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na elimu bora ni lazima pia uangalie maslahi ya walimu. Maslahi ya walimu...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kengele ya pili imeshagonga.

MHE. REGINA N. QWARAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu, kwanza nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja hotuba nzuri ambayo imewasilishwa na Waziri wetu Mkuu ambaye imetupa matumaini kwa kipindi kilichopita utekelezaji wake na kipindi ambacho tunachokwenda cha bajeti cha mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi tunafahamu Serikali iliyoko inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na Ilani yetu imejipambanua vizuri sana, Ilani ya 2020 – 2025 yenye ukurasa 303 kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Igalula Serikali kupitia hotuba ya Waziri Mkuu imewasilisha ni jinsi gani imejali katika sekta ya afya. Na katika hotuba yake imesema kwa kipindi kilichopita wameweza kujenga zahanati zaidi ya elfu moja na mia moja na kidogo. Lakini vilevile wameweza kujenga vituo vya afya zaidi ya mia nne katika nchi nzima ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Jimbo langu la Igalula, Jimbo lenye wakazi zaidi ya laki tatu waliopisa kura waliojiandikisha mwaka 2020 walikuwa zaidi ya laki moja na kidogo. Lakini Jimbo langu lina zahanati 17 tu ambazo zinatoa huduma kwa wananchi zaidi ya laki tatu, ukigawa uwiano wa zahanati hizo ni zaidi ya kila zahanati inaenda kuhudumia zaidi ya watu 20,000 ambayo kwa kuzingatia Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kufikia na kufikisha huduma bora kwa wananchi wetu si sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Igalula ni waungwana sana wamekuwa wakiibua miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya zahanati na shule. Na wamekuwa wakijitolea sana kwa kuwa wao ndio wanaona ndio vipaumbele vyao. Nilipochaguliwa na wananchi wa Jimbo la Igalula nimefaya ziara katika vijiji takribani 30 kati ya 58 kuangalia nini mahitaji yao na kila nilipokwenda wanahitaji shule na zahanati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hotuba ya Waziri wetu Mkuu ambayo amewasilisha katika Bunge hili. Niombe Serikali, juzi wakati tunachangia mpango wakati wa majumuisho Mhehimiwa Ummy Mwalimu alisema mwaka huu atajielekeza katika kutatua na kuweka vifaa tiba katika vituo vyetu nya afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo jema zaidi, lakini niwakumbushe kuna maboma mengi ambayo yameibuliwa na wananchi wanahitaji yamalizike. Tukisema twende tukupeleke kwenye vifaa tiba kwenye kituo cha afya kimoja katika jimbo la Igalula hatuwasaidii wana Igalula. Leo hii aliyekuwa Waziri wa Ofisi ya Rais, nani hii Jafo, alikuja katika Kata ya Igalula, aliwakuta wananchi wamechangia kwa nguvu zao wodi ya mama na mtoto akavutiwa na uwekezaji ule na juhudzi zile aliweza kutupatia fedha na sasa tumejenga kituo cha afya kilichopo katika Kata ya Igalula. Niwaambie kituo cha afya kimekamilika tangu mwaka 2019 mpaka leo hakijaanza kazi. Sasa lengo la Serikali ni kuongeza huduma kwa wananchi na si kuua huduma kwa wananchi. (*Makofî*)

Meshimiwa Naibu Spika, wameweke vigezo, kulikuwa kuna zahanati jirani wanasema tuhamishe vifaa tupeleke kwenye kituo cha afya sijajua hayo maelekezo yanatoka huku juu au wenyewe maamuzi yao. Lengo la kuongeza vifaa, vitoa huduma ni lengo la kuwasaidia wananchi, haiwezekani palikuwa na zanahati na tunasema tuna zahanati elfu moja na ushee pamoja na ile zahanati halafu unakwenda kuiua, unasema vile vifaa tuhamishie kwenye vituo nya afya, hata ukiangalia mwongozo wa afya, vifaa nya kwenye zahanati na kituo cha afya ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kuitia kituo chetu cha afya katika Kata ya Igalula tupate vifaa tiba na ile zahanati iendelee kuwepo na wananchi waendelee kupata huduma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maboma ambayo Serikali imeomba tuwasilishe kuitia halmashauri zetu. Niombi yale maboma yote ambayo yapo katika hatua ya umaliziaji na ni nguvu ya wananchi watu wengine, wananchi wengine baadhi ya kata na vijiji wamejenga zaidi ya miaka sita, mingine miaka minne mitano, wakiwa wanapita pale wanaangalia nguvu zao zimepotea basi Serikali kuitia bajeti hii iweze kuweka fedha ya kwenda kumalizia yale maboma ikiwemo maboma ya zahanati na shule, hivi hivi niombi Serikali iweze kutusaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la miundombinu juzi wakati wanachangia hapa Wabunge wenzangu kuna mbunge mmoja alisema ye ye katika Mkao wa Dar es Salaam haitaji kilimo kwasababu hana eneo la kulima. Alisema anahitaji barabara ili aweze wanachi wake waende kutafuta kipato warudi nyumbani wakiwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wanahitaji miundombinu ya barabara, barabara zetu za vijiji tofauti na za Dar es Salaam. Barabara zetu za vijiji wanahitaji kiwango cha changarawe ili ziweze kuitika muda wote. Tukija kwenye masuala ya sekta nitachangia zaidi kutokana na muda niseme tu itoshe ninaunga mkono hoja hotuba ya Waziri Mkuu. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wabunge wenzangu niungane nao kwenye kuiunga mkono hoja ya Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo naomba nijielekeze kwenye hotuba yake ukurasa wa hamsini ambapo amejaribu kuelezea kwa kina namna ya mafanikio ya miradi mikubwa ukiwemo mradi wa reli, lakini kwa masikitiko makubwa kwenye eneo hili nimeisoma kurasa hiyo nimeona ameizungumzia sana *SGR* lakini naomba nilikumbushe Bunge hili na ninaomba niikumbushe Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba tunayo lugha tunayoitumia waswahili kwamba cha kale dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo reli mbili kubwa, tunayo reli ya kati ambayo inasimamiwa na *TRC* na tunayo reli ya *TAZARA* hizi reli, ni reli ambazo zimeweza kutoa huduma katika nchi hii kwa muda mrefu na zilikuwa na zina faida kubwa sana kwenye maeneo ambayo yamekatiza. Nikumbushe tu na Wabunge wengi naamini wataungana nami mkono kwamba wengi kati ya tuliohapa tumefanya biashara kwenye reli hizo ambazo nazitamka kwenye vituo mbalimbali zilizokuwa zimepitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zimesaidia stesheni zile kuwa sehemu za masoko ya kuuzia biashara za wakulima mbalimbali waliokuwa kwenye maeneo hayo. Nikitoa mfano kwenye maeneo ya Jimbo langu kwenye Stesheni ya Ruvu, Kwala, Ngeta, Msua, Magindu watu walikuwa wanakwenda kuza mahindi yao. Kwa hiyo, ni moja ya sehemu kama masoko yalikuwa yanawaingizia kipato wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Serikali pamoja na nguvu kubwa waliyoivekeza na namna ambavyo wanaendelea kuifanyia ukarabati reli hii niwaombe waendelee kuongeza nguvu ili reli hii itumike na ikiwezekana kwa sasa waongeze ratiba ya kutumika ya abiria kutumika katika reli hiyo. Kwani sasa hivi ukiangalia ratiba imeharibika inapita kwa wiki mara moja kwa hiyo, maeneo mengi ya vijijini ambapo watu wanaitumia reli hii wamekosa kufanya huduma hiyo ambayo walizoea kuifanya kwa siku nyingi. Kwa hiyo, ningewaomba sana tuweze kuongeza nguvu ya kuwekea utaratibu wa miundombinu mizuri ili tuweze kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambambana hilo lipo jambo moja linaendelea sasa hivi kwa kweli kwenye eneo lille na ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake walichukue hili. Kuna watumishi kwenye Shirika la Reli na hasa hili la *TRC* kwa kweli kumbukumbu zinaonyesha mwaka 2007 Shirika hili lilikabidhiwa kwa shirika moja linaitwa *TRL* mkataba ulikuwa watumishi wale kabla hawajaenda kufanya kazi kwenye maeneo kwenye Shirika la *TRL* walitakiwa wamalizane kabisa na Shirika la *TRC*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana Shirika hili watumishi wale mpaka leo wapo, waliachwa na hajalipwa mafao yao na wamepokewa tena shirika lingine na wanaendelea kufanya kazi. Ningewakumbusha Serikali ebu waende wakazungumze na watu wale na ikiwezekana wawasaidie kulipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mwaka 2009 hao *TRL* walishindwa kuliendesa shirika na walirudisha tena *TRL* bado matatizo yakawa ni yaleyale wale waliofanya nao kazi malipo hawakuwapatia na mpaka hivi navyozungumza malipo yao hawana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa kuliko vyote wanachochama ambacho wenyewe ndio kinawasimamia maslahi yao kinaitwa *TRAU*chama hiki kimefumiliwa, viongozi wake wanatishwa na wakionekana wanasmamia maslahi ya wenzao wanahamisha kwenye shirika hili na kuwapatia shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Serikali na hasa wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu waende wakazungumze na watumishi wale, wawasikilize wanamatizo mengi. Ninayezungumza natokea kwenye ukanda huo nimeishi kwenye maeneo hayo nawafahamu vizuri changamoto wanazozipata watumishi hawa. Zamani walikuwa wanapelekewa mpaka maji na treni kwenye maeneo wanayofanya kazi, sasa hivi hawana hizo huduma. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali iende ikawaangalie watu hawa na waweze kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza katika eneo ambalo nataka nilizungumzie sasa hivi ni suala zima la miradi ambayo Serikali imeielezea miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jimbo langu wakati anapita ambaye ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano leo kwenye kipindi cha kampeni alitoa ahadi na ahadi ile naomba niithibitishie Serikali yake kwamba tumetekeleza vile ambavyo ametuelekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alitwambia kulikuwa pale na mradi wa kujenga soko mradi ule uliingiliwa na changamoto mbalimbali na Serikali inajua. Rais wetu alitueleza kwamba endapo tutakuwa tumerekebisha kasoro zilizopo basi atakuwa yuko tayari kutuletea zile fedha na tuendelee na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii niseme changamoto ambazo zilikuwa zinataka zisumbue kwenye eneo lile tumezimaliza na eneo tunalo na tuko tayari kwenda kuendelea na ujenzi. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutumia Wizara ya TAMISEMI, Naibu Waziri kama itampendeza aende pamoja na mimi baada ya Bunge hili akaone zile changamoto ambazo tumezimaliza ili tuweze kuendelea na mradi ule ambaao ni mradi muhimu kwetu kwani utaongeza pato la halmashauri katika eneo letu na kuongezea mapato ya Serikali nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo dogo lingine kwenye maeneo yetu tunao matajiri ambaao wamemiliki mashamba makubwa sana, mashamba ambayo yanaleta mgogoro mkubwa sana wa kimaslahi kwa sasa, wananchi wameingia mle wako katika muda mrefu sana na yale maeneo hawajatumia kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo shamba moja linaitwa la *TAN CHOICE* la hawa watu wanaitwa *Trans-continental* liko Kikongo. Yule bwana hafahamiki, hajulikani aliko anatumia vibaraka wake kuwatisha wananchi

wanaendelea na shughuli zao mle ndani. Naomba Serikali ije imalize tatizo lile ili wananchi waliowekeza kwenye eneo lile waweze kuongeza kipato cha nchi hii kwasababu wanalima na wanalipa kodi mbalimbali na maeneo yale wengine wameshaweka visima mle ndani, wameshajenga majumba mazuri, na wanaendeleza maeneo yale, kwa hiyo ningeomba sana Serikali ifike sehemu iweze kuja kutusaidia. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna eneo ambalo hata Mheshimiwa Marehemu Hayati Dkt. Magufuli alipita pale Soga. Kuna shamba la *Mohamed Enterprise* hii imekuwa kero ya muda mrefu Mheshimiwa Rais alisema jambo hili limalizwe lakini mpaka leo halijamalizwa. Na Wizara ya Ardhi wanalijua lakini sijui tatizo liko wapi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Serikali iende kwenye maeneo yale itumalizie matatizo haya ili wananchi waishi kwa amani waendelee na shughuli zao. Kwasababu sasa hivi wanazidi kuendelea, wengine wanavunjiwa majumba yao na mambo mbalimbali yanaendelea kufanyika kwa hiyo, ningeomba wizara inayohusika tukamalize tatizo hili. Baada ya kusema maneno haya naunga mkono hoja. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza ya mchango wenu wa bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nitaje majina ya baadhi ya Wabunge tutakaoanza nao mchana; Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Cecilia Paresso na wengineo tutaendelea kuwataja kadri tutakavyokuwa tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge kuna wageni ambao walitajwa asubuhi lakini hawakuwa wamepata fursa ya kuingia humu ndani nitawatambulisha kwenu sasa.

Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango na huyo ni mke wake anaitwa ndugu Neema Nchemba kutoka jijini Dar es Salaam. Karibu sana, karibu sana wifi yetu na shemeji yetu, Waheshimiwa Wabunge hapa na Taifa kwa ujumla litangaziwa kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ana mke. Nadhani ndio lengo la mkuleta hapa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge ambaye ni rafiki na mdau wa maendeleo kutoka Tokyo nchini Japan ndugu Mio Sunoda, karibu sana, karibu sana. Huyu sasa katoka Japan lakini naona anafanana kabisa na sisi kwa namna alivyovaa maana yake wajasiriamali wanafanya kazi nzuri, karibu sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo lingine linalowahu Wabunge Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa kuteuliwa na Wabunge wa Viti Maalum wote wakitoka hapa waelekee Msekwa. Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wanasubiri hapo. Tangazo lilitangazwa jana lakini linarudiwa sasa kuwakumbusha tukitoka hapa tuelekee Msekwa kuwasiliza viongozi wetu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili Alasiri leo.

(Saa 07.04 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, tutaanza na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Hadija Taya, Mheshimiwa Ally Jumbe ajiandae.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mchangiaji wa kihistoria leo kwa kuwa mchangiaji wa kwanza katika session hii ya jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kwanza kabisa kuipongeza Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji mzuri. Kwa kweli hotuba hii imetupa dira nzuri ya kuonyesha kama Serikali wapi tulikotoka, nini kimefanyika na yale ambayo tunakusudia kwenda kuyafanya katika kipindi kijacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo sitakuwa mzungumzaji wa mambo mengi sana, lakini nataka niguse tu katika maeneo kadhaa hasa katika miradi mikubwa ambayo Serikali wameweza kuitekeleza na wanakusudia kuitekeleza. Baada ya hapo, nitagusia kidogo mambo mawili, matatu katika jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wazungumzaji wengine kusema kwamba ni ukweli uliokuwa wazi kwamba *legacy* aliyoiacha Hayati Dkt. John Pombe Magufulি itakuwa inaenda kujieleza yenye. Kwa tafsiri hiyohiyo, ni matumaini yangu kuwa tunategemea kuanza kuona *legacy* mpya ya mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hasa katika kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imeachwa na *predecessor* wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niguse miradi ya kimkakati, kwa mfano mradi wa *SGR*, ni muhimu sana kwani unakwenda kufanya *total transformation* ya *social economic transformation* katika nchi yetu. *Especially* katika maeneo yote yale ambayo yatakuwa yanapitiwa na mradi

ule, tunategemea kwa namna moja ama nyingine kutakuwa na mabadiliko makubwa sana ya kijamii na kiuchumi vilevile. Hivyo, ni mategemeo yangu kuona Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan wanakwenda kukamilisha miradi hii. Hii itatuwezesha sisi kama Serikali au kama Taifa kuwa na mapato ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba vilevile nizungumzie mradi mzuri sana wa ndege. Mradi huu wengi sana wamejaribu kuongeaongea na wale rafiki zetu wengine ambaao wako *form six*, walio-graduate kule marafiki zangu, waliweza kuzungumza mengi sana katika mradi huu. Nataka ni semet tu mradi huu mama yetu ameanza vizuri sana, alianza kwa salam nzuri ya kuwasalimia Watanzania, kwa kusema nawasalimu Watanzania kwa salaam ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alisema kazi inaendelea katika majibu hayo. Katika majibu hayo mama ameanza vizuri, tayari yale malipo ya ndege tatu yameshakamilika, hivyo tunategemea kwenda kuona ndege nyingine zinaongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena katika jambo hili la mambo ya ndege. Katika sekta nzima ya mambo ya *aviation*, sekta hii siku zote tafsiri yake pana ni kwamba inakwenda kuchochaea uchumi wa nchi. Tunavyokuwa na *National Flag Carrier* maana yake ni kwamba tunakwenda kuitangaza nchi. Hivyo basi, ni semet tu kama Serikali wamefanya jambo la busara na Mheshimiwa Rais alivyoweza kuzilipa ndege hizi tunakwenda kuona sasa mabadiliko makubwa yanakwenda kupatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatoe shaka Wabunge wenzangu, lakini vilevile na Watanzania kwa ujumla, kale ka-hasara kalivyokuwa kamezungumziwa, najaribu ku-refer kule katika Ripoti ya *CAG* isije sana ikatumiza vichwa. Wenzetu Kenya mwaka jana waliweza kutengeneza *loss* ya Dola milioni 338; mwaka 2019 walitengeneza *loss* ya Dola milioni 258; mwaka 2018 walitengeneza *loss* ya Dola milioni 100 lakini bado wako

stable, tafsiri yake ni kwamba wanafanya vizuri katika sekta *tourism*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke ufahamu vizuri hapa kwa Watanzania pamoja na wale Wabunge wenzangu ambaao ni *form six*. Tafsiri yake ni kwamba katika *accounts* kuna kitu kinaitwa *net off* maana yake ni kwamba kama kuna hasara inapatikana katika sekta moja inakwenda kuwa *compensated* katika sekta nyingine. Sisi kama Tanzania tumefanya vizuri na maono mapana ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kuimarisha suala zima la *tourism*. Hivyo, naiomba Serikali, twendeni tukapambane ili tuweze kuhakikisha tunakwenda ku-*boost internal tourism* ili sasa ndege zetu hizi zilizopatikana ziende kufanya vizuri kama kwa *neighbor* zetu wa Kenya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie mradi wa *hydroelectric power*. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwenda katika eneo ambapo mradi ule unafanyika, maelezo aliyojatoa ni ya faraja na ya kuwatia matumaini hasa Watanzania na vilevile wajomba zangu wa Rufiji na sisi watu Kibiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unafanyika katika maeneo makubwa mawili, kuna *upper stream* na *downstream*. Sisi tupo kule katika maeneo ya *downstream*, kuna hekari takribani 150,000, napenda sana kuiona Serikali sasa inakwenda kujielekeza katika mradi ule ili sisi watu wa Kibiti na Rufiji tuweze kunufaika katika masuala mazima ya umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ni cha msingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unavyokwenda kukamilika na tumeambiwa kwamba fedha zipo na mimi sina shida na sina shaka na Serikali ya Awamu ya Sita najua fedha zipo na mengi yameshaanza kufanyika. Ni imani yangu kwamba tutakwenda kuwa na mradi wa umwagiliaji ili tuweze kuhakikisha mradi huu ya *hydroelectric power*

unakwenda sambamba na mradi na mradi ule wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa mambo yangu ya jimboni. Nimshukuru tu Mheshimiwa Rais ameanza vizuri, kama alivyoanza kusema kwamba kazi inaendelea, ni kweli kazi inaendelea. Hivi ninavyoongea tayari shilingi milioni 594 zimeshapelekwa katika kumalizia jengo la Mheshimiwa Mkurugenzi wetu wa Wilaya. Sambamba na hilo tumeweza kupewa fedha takribani shilingi milioni 500 tunakwenda kujenga wodi tatu katika Hospitali ya Wilaya. Tumepewa fedha nyine shilingi milioni 180 katika kukamilisha maabara 6. Fedha hizi zimepatikana kutokana na mama huyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi, tumeweza kupewa fedha nyine takribani shilingi milioni 136 katika mradi wa maji. Hivi navyozungumza tayari katika Kata ya Dimani maji yanatoka, mambo yetu yanakwenda bambam. Nani kama mama?

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, mama huyu ameyafanya mambo mazuri na sisi ni mategemeo yetu anakwenda kuyafanya mazuri zaidi katika kuhakikisha kwamba kauli yake inayosema kazi inaendelea ni kweli kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya *it's not a rocket science*, ni vitu ambavyo viko wazi, tayari tumeshalipa ndege tatu nani kama mama?

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu kubwa Zaidi ni kwamba mama yetu Samia Suluhu Hassan anakwenda kutengeneza *legacy* nyine ambayo ameiacha *predecessor* wake ya kukamilisha miradi mikubwa hii ya *SGR* na *Hydroelectrical power* na mingine kama nilivyokuwa nimezungumza. Kama hiyo haitoshi

ametuambia Mheshimiwa Ummy Mwalimu hapa tunakwenda vilevile kujenga Vituo vyat Afya katika wilaya zile ambazo bado hazijafikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, napenda kusema naunga mkono hoja. Tumuombee mama yetu ili aweze kutusogeza mbele. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Taya atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Jumbe na Mheshimiwa Priscus Tarimo ajiandae.

MHE. KHADIJA S. TAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote ambaye ametufikisha hapa leo tukiwa na afya njema na uhai ambao ametupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo napenda nijikite katika mambo mawili, matatu. Mojawapo nataka nizungumze juu ya watu wenye ulemavu na ajira. Katika kusoma na kufuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nimegundua kwamba ni msikivu sana, amefanya kazi nzuri sana, amefanya kazi ambayo Mungu anamtaka yeye afanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ilishauri mambo kadhaa wa kadha lakini nashukuru moja ambalo umesema unaenda kulitekeleza ni hili la kuleta *data* kamili ya watu wenye ulemavu. *Data* kamili ya watu wenye ulemavu itatusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hiyo *data* kamili ya watu wenye ulemavu, kutakuwa na wasomi, wafanyakazi, watoto wadogo na wagonjwa ambao tutawatambua ili kutekeleza kwa urahisi kabisa malengo ambayo tumejiwekea kwa watu wenye ulemavu. Naomba niseme kwamba hali ya watu wenye ulemavu ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke msisitizo katika suala la ajira. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameendeleza yote mazuri yaliyofanywa na Awamu ya Tano. Katika kuchagua na kujali Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu, amechagua watu watano katika Baraza la Makatibu Wakuu, hii pekee inaonesha dhahiri anatuamini sisi watu wenyе ulemavu. Naomba Serikali iangalie suala hili kuanzia hapo, kwamba tumejaliwa watu watano wenyе ulemavu basi ishuke mpaka chini kwenye watumishi ili tuweze kuonekana na kuonesha uwezo wetu ambapo tunaamini kabisa uwezo tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuangalie lile suala la asilimia tatu, je, limetimizwa na kwa ukubwa gani? Kwa sababu nikiangalia *private sector*, hata humu ndani tu kuna Wabunge wana makampuni makubwa, je, wametimiza ule wajibu wa asilimia tatu? Hili suala tulifuatillie, tusiwe tunaweka sheria ambazo hatuwezi kuzifua tililia kama zinatekelezeka. Tuweke sheria ambazo tunaweza tukazifua tililia tukajua kabisa hii idadi ya watu wenyе ulemavu ya asilimia tatu inatekelezwa Serikalini pamoja na *private sectors*. Kwa *private sector*, mtu amewekeza pale akiamini mtu mwenye ulemavu hawezi, basi tuangalie namna gani ya kuwapa hawa watu *motivation* au kuangalia namna yoyote ile hata ya kuwapunguzia kodi fulani hivi ambayo inaweza wao kuwafanya waendelee kuajiri watu wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu nafahamu watu wanaoniomba kazi na wanataka ada ya shule na kadhalika. Kwa hiyo, hizi *data* zitatusaidia sana, nawaomba ushirikiano katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nishukuru baadhi ya Wabunge ambao tayari wameendelea kuzungumzia watu wenyе ulemavu na wale ambao wameendelea kujitoa katika majimbo yao kama kutoa miguu kwa watu wenyе ulemavu wa viungo, kwa mfano, namshukuru sana Mheshimiwa Antony Mavunde. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie watu wenyе ulemavu kwa jicho pana zaidi. Kwanza, tupo wachache sana na sidhani kama

Serikali hii chini ya Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan itashindwa kulisimamia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nizungumze juu ya Jiji la Dodoma au Makao Makuu ya Dodoma. Sote humu ndani tunafahamu kwamba Bunge la Kumi na Moja liliazimia kuweka Sheria ya Makao Makuu, basi hii sheria isiwe tu kwenye makaratas iendane na utekelezaji wake. Utekelezaji wake ni kuendelea kufufua vitu ambavyo vitaonyesha kweli hii ni Makao Makuu. Tuangalie Uwanja wa Msalato, *ring road*, upatikanaji wa maji. Hili la upatikanaji wa maji ni shida sana, kuna maeneo ambapo siku nne hakuna maji, tunaishije hapa na sasa hivi tuna kiwango kikubwa sana cha watu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali hii itambue na iendeleze lile wazo la Mwalimu Julius Nyerere la kuhamia Dodoma ambalo lilitkelezwa Awamu ya Tano, tuendelee kutekeleza yale yote ambayo waasisi wetu wametuwekea katika mipango yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Watanzania wote ambao wamejitokeza kwa wingi kuomboleza msiba wa kipenzi chetu. Hii imetuonesha kabisa kwamba Rais wetu alikuwa anakubalika, amefanya kazi kubwa kwa ajili wa Watanzania na kweli alikuwa ni Rais wa wanyonge. Kwa kuangalia hilo, naamini Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Rais wetu mpendwa ataendeleza yote kwa sababu ni mwanamke shupavu na jasiri. Naomba wanawake wote tumsaidie kusimamia yale yote ambayo tumejiwekea katika llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache niliyozungumza, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mheshimiwa Ally Jumbe, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Dunia na Afrika nzima inashangaa na

kustaajabu ukuu wa Mungu ambaao amebariki Taifa hili mpaka sasa hatujaingia kwenye *lockdown* na tunakaa kwenye Bunge hili. Naomba tuendelee kumshukuru Mungu na sifa na utukufu vimwendee yeje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Watanzania na Wabunge wote tusijisahau, haya yanayotokea ni kwa sababu ya mtu mmoja tu, Mungu huwa anamwangalia mzawa wa kwanza wa familia, matendo yake ndiyo yanayoshuka chini. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alimwamini Mungu, alisema Watanzania hatuna haja ya kuingia kwenye *lockdown* hata kama Mataifa mengine yanaingia twende tumuamini Mungu na yale maneno naomba tuendelee kuyaishi ndiyo yaliyotufikisha hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu haya yote pia Rais Dkt. John Pombe Magufuli hakufanya yeje peke yake, alikuwa na msaidizi wake ambaye alikuwa pia anamuonesha na kushauriana naye, naye si mwingine, ni mama yetu kipenzi, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan. Huyu mama ndiye yule ambaye aliahidiwa kwamba atampokea kijiti Mussa, sasa Mussa amebaki yeje anaendelea na ndiyo maana naomba leo niwasalimie kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WABUNGE FULANI: Kazi iendeleee.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waziri Mkuu anafanya kazi kubwa sana na anachapa kazi usiku na mchana. Ndiyo maana katika yote niseme naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, nilipenda niongelee mambo mengi sana lakini nimejikuta nipo kwenye masikitiko makubwa sana. Kata kumi za Wilaya ya Kyela leo ni siku ya tatu wananchi wako kwenye maji, wako kwenye mafuriko. Naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole, lakini naomba sasa hata kama taarifa hazijafika basi Ofisi ya Waziri

Mkuu, Kitengo cha Maafa kiiangalie Wilaya ya Kyela kwa jicho la huruma. Wilaya ya Kyela Kata kumi za Katumbasongwe, Bujonde, Kajunjumele, Matema, Isaki, Mwaya, Ikama, Ipinda na Makwale. Kata hizi zote wananchi wametoka kwenye nyumba zao, hawana chakula wala mahali pa kulala wako nje na mpaka barabara zote hata barabara yetu ya lami ipo kwenye maji sasa hivi na kuna sehemu imeanza kubomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu kuna haja ya kuipendelea Wilaya ya Kyela kwa namna moja au nyingine kwa sababu moja tu. Wilaya ya Kyela ndiyo iko chini kabisa kwenye uwanda, iko mita 450; mvua zote zinazonyesha Illeje, Songwe, Rungwe na Busokelo matokeo yote mabaya yanaelekea Kyela. Hata barabara zilizoko Kyela sasa hivi zimegeuka kuwa mito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kyela bado haijapata pesa za *development* kwenye barabara zake. Miaka mitano iliyopita mpaka mwaka huu hakuna pesa hiyo. Naomba sasa Serikali iiangalie Kyela tofauti na sehemu zingine kwani yenye we iko tofauti na sehemu zingine, iko chini mno. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala dogo tu ambalo ni la Kimungu. Kuna watu wanashangaa kwa nini Tanzania hiko hivi? Viongozi wote wanafanya vizuri. Nataka niseme, ndugu zangu, kila Rais aliyetokea Tanzania alikuja kwa mkono wa Mungu na kwa kazi yake maalum. Hakuna Rais aliyeku ja kivyake vyake kwa sababu nchi hii imabarikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Kwanza alikuja kwa ajili ya Uhuru na kutuunganisha Watanzania wote ili tuwe kitu kimoja. Akafuata Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi; baada ya kuungana Watanzania wote, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi aliona Watanzania mmoja mmoja, hawana uchumi wa kutosha, akatufunga wote, tukapata fedha, tukajifunza kutumia fedha. Nakumbuka kwetu ndiyo wakati ambao watu

walianza kujifunza kuvalaa viatu, tulikuwa tunaviita Ahsante Salim.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa, akaona kwamba nchi haina fedha, lazima nchi ijikamilishe, Serikali iwe tajiri. Akaifanya Serikali ya Tanzania ikaanza kuwa na uchumi wake na kulipa madeni. Akaja Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete akaifanya Tanzania ijulikane nje. Hiyo ni kazi ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu walikuwa hawajui hata kwamba Mlima Kilimanjaro uko Tanzania. Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alitufanya watu wa nje wajue Mlima Kilimanjaro uko Tanzania. Likaja Bulldozer ambalo kazi yake ilikuwa ni kuifanya Tanzania ijitegemee na hapa ndipo tulipofika. Haya hayajafika kwa kudra tu, ni Mungu aliyapanga kwamba yatakuwa hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nataka kukishukuru sana Chama cha Mapinduzi. Chama hiki ni chama ambacho Mungu alikibariki, kwa sababu ni chama pekee ambacho kinafuata mifumo ya vitabu vya Mungu. Nimesoma kwenye Biblia; Kutoka 18:21-23 ndiko zilikoanzia nyumba kumi kumi. Maana alisema watu waongozwe na nyumba kumi kumi, elfu elfu na hamsini hamsini.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Priscus Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ennocent Kalogeris na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma ajiandae.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi wa Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa salam zangu za pole kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu na Serikali na Watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza Rais wetu Hayati Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pole hizo, nitoe pongezi kwake Rais sasa Mheshimiwa Mama Samia kwa kuchukua nafasi yake kama Rais. Vile vile nawapongeza Mawaziri wote na viongozi wote ambao wengine wamebakil kwenye nafasi zao, wengine wamebadilika na wengine wameingia ili kuweza kulisongesha gurudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyo vipengele kama kumi ambavyo nitaviongelea kama muda utaruhusu. Naomba nianze na kilimo. Tumeshakubaliana kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Yako maeneo ya kufanya kazi na mengine ya meshatajwa au kusemewa na viongozi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni eneo la utafiti. Nafikiri ni muda muafaka sasa Wizara itumie nguvu kubwa kwenye maeneo yote, wajue ni mazao gani yanalamika kirahisi wapi na kwa njia ipi. Nchi ambazo zinaweza kutusaidia sana kwenye hilli tukichanganya na wataalam wa ndani kutoka kwenye vyuo vyetu pamoja na *SUA* ni pamoja na *Egypt*, Israel na Netherland ambao wamefanikiwa sana kwenye kilimo pamoja na mazingira yao kuwa magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine muhimu sana kwenye kilimo ni la umwagiliaji. Bwawa la Nyumba ya Mungu lilijengwa na Serikali yetu miaka ya 1960, nafikiri ni mwaka 1967. Eneo lile lilipojengwa limekuwa ni kichocheo kikubwa. Mzungumzaji aliyejita ameongelea mafuriko huko kwao Kyela. Serikali ikiweka nguvu katika namna ya kuyachukua haya maji na kutengeneza mabwawa kwenye maeneo yenye kilimo, itasaidia sana kuondoa utegemezi wa kilimo hiki ambacho kinategemea mvua na ambavho hakina tija sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo, nafikiri kuna vitu ambavyo tuna uwezo navyo, ambavyo tuna mahitaji navyo sana hapa ndani. Tuna upungufu wa mafuta ya kula. Kwa hiyo, tukiwekeza kwenye alizeti, tayari soko lipo, la ziada litakuja tu baadaye. Tuna upungufu wa ngano; tukiwekeza hapo maana yake soko la ndani lenyewe linaanza na linatosheleza. Hata sukari, tuna upungufu na tunatumia fedha nydingi sana kuagiza kila mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha miaka kama ni mitano au kumi hili tatizo linaisha, tunaweza kabisa na tutakapofanikiwa hilo, basi nyongeza itakayopatikana, itaweza kuuzwa nje na kutupatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kugawa maeneo ya klmkakati, yaani *block zone* pamoja na kuwashirikisha wakulima wadogo. Ningependa sana kama ningeona mkakati wa kuwavutia wakulima wakubwa wa ndani na wa nje kwa kuwatengea maeneo na kuweka sera ambazo zitawavutia waje walime hapa kwetu. Wakilima, watatusaidia kwenye soko la ndani na vile vile kwenye kuuza nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ambalo linawezekana hapa na ninalitolea mfano kwenye taasisi ile ya *TAHA* ni kutumia hii *block zone*. Ukishawaweka watu kwenye *block* ni rahisi kuwafuatilia na kuapelekea wataalam wanaowashauri kama inavyofanya Taasisi ya *TAHA* kwenye mboga mboga pamoja na matunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishaweza kuwekeza vizuri tukaweka hizi sera vizuri kwenye kilimo, tunahamia kwenye viwanda. Viwanda vitakuwa ndiyo watumiaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo. Hapa ndiyo sera tunayokwenda nayo, lakini sijaona sera au *incentives* zinazosababisha watu watoke maeneo mengine waje waweke viwanda vyao hapa. Sijaona. Ni muda muafaka sasa Wizara ione namna ya kuendelea kutafuta na kuweka mazingira yatakayovutia wawekezaji wa nje na wa ndani kwenye viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, tukiweka viwanda vya vile vitu ambavyo tuna upungufu navyo ndani, maana yake tunahakikishia wawekezaji kwamba soko lipo; hivyo ambavyo nimetaja hapo juu kwenye kilimo; suala la mafuta, sukari na vitu vingine ambavyo tayari tuna uhitaji navyo sana ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengine yanatia hasira. Nami nilisema mara ya kwanza na ninarudia tena. Naunga mkono wale waliobinafsishiwa viwanda kwa nia ya kuviendeleza ili vitoe ajira na viingize kodi wakashindwa, wanyang'anywe tuvitangaze tena upya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Moshi kuna Kiwanda cha Magunia, kimefungwa, hakifanyi kazi; kuna Kiwanda cha Viberiti, Kibo Match, kimefungwa na wana nyumba pale zimefungiwa chini, hazifanyi kazi. Ili kulitilia nguvu hili, ni muda muafaka sasa tuvichukue, halafu tutangaze upya viwanda hivi viweze kuanza kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la afya. Hili kidogo niliongelee kwa choyo kwa kuangalia Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa huu una Hospitali ya Rufaa moja, inajulikana kama Mawenzi, imejengwa miaka mingi iliyopita, 2022. Hospitali ile imekuwa ya kizamani sana na miundombinu yake iko kwenye hali mbaya sana. Kinachosikitisha zaidi, kuna Jengo la Mama na Mtoto ambalo lingekuwa na huduma nyingine za kisasa katika *design* yake kama *IMR, X-Ray* za kisasa na vitu kama hivyo; lakini imeanza kujengwa 2008 mpaka leo haijamalizika na ni jengo moja na sijaiona kwenye ripoti ya *CAG* kwamba ni nini kilisababisha inachukua muda mrefu namna hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iende ikaangalie pale Mawezikuna nini? Tangu mwaka 2008 jengo moja halimaliziki. Naomba sana kwa sababu Mkoa wa Kilimanjaro hatuna Hospitali ya Rufaa inayoendana na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Moshi Mjini au Moshi kama Wilaya hatuna Hospitali ya Wilaya, tunatumia hospitali za binafsi sasa hivi. Mheshimiwa Rais aliyetangulia mbele za haki, Hayati Dkt. Magufuli alituahidi. Nami naomba ahadi hiyo iendelee kuhamishiwa kwa viongozi waliopo na sisi tupate Hospitali ya Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya suala la afya, nakwenda kwenye miundombinu. Kwanza naipongeza Serikali kwa mafanikio iliyopata. Kwenye SGR, ATCL, Bandari zinazoendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na barabara nyingi zinazojengwa. Natamani sana nione Wizara zinazohusika zikifanya juhudi ya kuhakikisha tunakuwa na *economic diplomacy* ya kuwashawishi kwa mfano watu wa Kongo. Kwamba ni kwa nini wapitishie mizigo yao kwa barabara kupitia Zambia badala ya sisi kuboresha bandari ile ya Kigoma na Rukwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliongelee kidogo. Upande huu wa Mashariki wa nchi yetu tayari kumeshafunguka, lakini upande wa Ziwa Tanganyika pale ambapo tunapakana na Kongo ambapo ni milking cow, inatakiwa zile bandari ziboreshw. Pale Rukwa reli iende mpaka pale bandarini, ziwekwe meli za kuweza kuvusha vitu viende kule Kongo. Balozi wetu pale atusaidie kuongea na watu wa Kongo nao wafungue barabara kwa upande ule wa kwao mambo yaende. Hakuna sababu ya mizigo kutoka kwenye bandari ya Dar es Salaam, ipitie Zambia ndiyo iende Kongo. Ni hela tumezikalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hilo tuliwekee nguvu kidogo liweze kuleta...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ajiandae.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu kwa mema mengi ambayo analitendea Taifa letu la Tanzania. Vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa nchi hili katika kipindi cha miaka mitano. Amekuza uchumi wan chi, ametupa ujasiri Watanzania na kubwa zaidi ametufanya tujiamini na kujitambua kwamba sisi sio masikini ni Taifa tajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii vile vile kumpongeza aliyekuwa Makamu wa Rais na sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amirijeshi Mkuu wa Awamu ya Sita, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa wakati ule ya kumsaidia aliyekuwa mtangulizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi nataka niwaambie Watanzania na wapenda maendeleo katika Taifa hili kwamba Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan anatosha kwa nafasi ambayo anayo kwa sasa na kubwa zaidi, tutorajia makubwa kwa maendeleo ya haraka na kwa kasi kubwa zaidi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo sisi Wabunge na yeye mwenyewe na Hayati Dkt. Magufuli walipita kuwaahidi Watanzania na tukakipatia Chama cha Mapinduzi ushindi mkubwa wa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vile vile kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye leo hii ametuletea bajeti na tunaijadili, kwa kazi kubwa ya usimamizi wa shughuli za Serikali katika Bunge na nje ya Bunge katika kipindi cha miaka mitano. Ndani ya hotuba yake kumeja yale ambayo yametekelzeza katika kipindi cha miaka mitano na yale ambayo tunaenda kuyatekeleza ndani ya miaka mitano katika kipindi cha mwaka huu mmoja ambao tunao katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Spika ambaye hayupo, niwape pongezi nanyi kwa kazi kubwa ambayo mliifanya katika Bunge la Kumi katika kuisimamia Serikali na kutunga sheria ambazo zimesababisha leo tumefika tuko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu nawaomba niwakumbushe, kazi kubwa ambayo tunayo kwa sasa, hata Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipokuja kufungua Bunge hili aliambia jambo moja; ana imani kubwa na Bunge hili. Sasa Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hayupo, ametangulia mbele ya haki, tuelekeze nguvu zetu na tuonyeshe imani hiyo ambayo Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alitupa Bunge hili tujielekeze kumpa nguvu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan aweze kutekeleza yale ambayo tumewaaahidi wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kuchangia hoja. La kwanza, nichangie katika mipango ya miradi mikakati. Tuna Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo kwa namna moja au nytingine liko katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini na liko katika Jimbo langu la Morogoro Kusini. Ni mradi mzuri na mradi ambao kwa kweli ukikamilika utaleta mafanikio makubwa ya kujenga uchumi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuthibitisha hilo nataka niseme tu mimi mwenyewe, ndani ya Halmashauri yetu, ndani ya kipindi hiki kifupi tumepata shilingi bilioni moja

na karibu milioni 100 kama *Service Levy* ambapo fedha hiyo tayari asilimia 10 imekwenda kwa vijana na asilimia 40 imekwenda kwenye miradi ya maendeleo ya Halmashauri na nyingine zimeenda kufanya shughuli nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, CAGamezungumza. Kuna 4% kama huduma katika shughuli za kijamii (corporate responsibility), ambayo inatakiwa itoke katika mradi huo iende katika shughuli za wananchi. Naiomba Serikali ikasimamie hili ili kusudi tuweze kuipata fedha hii katika Halmashauri tuweze kufanya shughuli nyingi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huu mradi wa *Standard Gauge*, ninaamini kabisa kwamba Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi zikishirikiana kwa pamoja wanaweza kutoa fursa kwa wananchi ambapo mradi huu utapita wakaweza kufanya kazi za maendeleo ambazo zitawaongezea uchumi na wakati huo huo mradi huu ukafanya katika misingi hiyo. Naomba tuangalie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la utawala. Katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijiji tuna jengo la Halmashauri. Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika mwaka wa fedha uliokwisha tumepata shilingi milioni 700. Mkandarasi yuko site, kazi inaendelea.

Naomba njue, katika awamu hii ya mwaka huu wa fedha, Halmashauri yetu imetengewa shilingi ngapi ili mradi huo uende moja kwa moja, tusije tukasimama ili tuweze kufanya shughuli za kuleta maendeleo kama vile ilivyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni afya. Katika mwaka wa fedha uliokwisha tumepata shilingi bilioni 4.3 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ambayo imekamilika na ujenzi wa vituo sita vya afya ambavyo vimekamilika. Sasa hivi kuna suala la vifaa tiba, kuna suala la dawa, ambulance na matabibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji hospitali ile ianze kazi ikiwa imekamilika, pia tunahitaji vituo hivyo vya afya vifanye kazi vikiwa vimekamilika, kufikia lengo ambalo Serikali inataka kutoa huduma kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini na Halmashauri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulioomba katika bajeti hii shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga wodi tatu katika Kituo cha Afya cha Mikesi, Kituo cha Afya Kisaki na Kituo cha Afya cha Kisemo. Tukipata fedha hizi ni kwamba tutakuwa na uwezo wa kujenga, kukamilisha na hivi vituo vya afya vitafanya kazi na wananchi watapata kile ambacho tunakihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, Halmashauri ya Morogoro Vijiji iko katika jiografia mbaya sana. Naiomba Serikali, pamoja na kwamba tumepata vituo vya afya sita, bado tuna uhitaji wa vituo vya afya tu. Tunahitaji Kituo cha Afya kwenye Kata ya Kasanga; Kata ya Bwakilajuu na Kata ya Singisa. Kata hizi ziko milimani na ni mbali kufikika, kwa hiyo, wananchi wetu wanapata wakati mgumu sana katika kupata huduma za afya. Tukiweza kuwafikishia huko, tutakuwa tumewasaidia sana. Naiomba Serikali ione ni jinsi gani ya kufanya na kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nizungumzie kidogo kilimo. Mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao una ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo. Nimeona katika mpango ambao tumeletewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kuna fedha zilikwenda Njage Wilaya ya Kilombero, kuna fedha zilikwenda Mvumi Wilaya ya Kilosa, kuna fedha zilikwenda Kigubu Mvomero na kuna fedha zilikwenda Kilangazi Kilosa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fedha hizo kwenda, lakini Mkoa wa Morogoro bado una maeneo makubwa kwa ajili ya kufanikisha kilimo cha umwagiliaji na ambacho nina uhakika ndiyo kilimo cha uhakika na cha kutusaidia. Niombe sana kuna mradi wa Kongwastro, mradi mkubwa sana unahitaji fedha...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nashukuru sana kwa kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nguvu, uwezo, uhodari na umahiri wa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutambua Tanzania yetu jinsi tulivyoweza kuridhika na kujidai na kujivuna kwa kuweza kupata Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Jemedari Mkuu mwanamke kuiongoza nchi yetu. Yeye ni Rais mwanamama wa mwanzo katika *block* hili la Afrika Mashariki. Niseme kwamba Mheshimiwa Jemedari wetu Mkuu Mheshimiwa Rais Samia ninaweza ku-quote '*is one of our own*' ni mwenzetu. Anatoka kwenye *block* ya akinamama. Uhodari wake na umahiri wake na ujasiri wake kwenye kazi tunamjua tangu asubuhi. Kwa hivyo niwatoe wasiwasi kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu viatu hivi vimemfaa sawasawa, tena vimekuwa *high heels* atakwenda mdundo wa kuchumpachumpa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kumpa ushirikiano kama vile tulivyokuwa tunampa kipenzi chetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye ametangulia mbele ya haki. Kwa nukta hiyo, namwombea rehema. Mungu ampumzishe kwa amani na natoa pole sana kwa familia ya Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mchango wangu kwa kugusia *program* za kukuza ujuzi wa

vijana ambayo inaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni dhahiri vijana wengi wanapotoka vyuoni wanakuwa hawana ujuzi wa kutosha katika kufanya kazi zao na hivyo kuweza kushindwa kuhimili ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Programu hii inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu imetumia gharama kubwa sana kwa kuwawezesha vijana hawa kupata nauli, fedha ya chakula wakati wanapokwenda kufanya mafunzo ya uanagenzi katika mashirika mbalimbali. Kwa sababu baadhi ya wanufaika hawalipii gharama hizi, lakini ni hii programu imewawezesha vijana wengi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uko umuhimu wa kuongezwa bajeti ili kuweza kuwafaidisha vijana wengi waweze kupata hii programu ya uanagenzi. Katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu iko shida moja ambayo tumeiona sisi na hii nayo inatokana na tatizo la kukaimisha watumishi kwa muda mrefu na tatizo la kutoajiri watendaji wakuu wanaostahili na hivyo kuleta shida katika kuchukua hatua wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida hii ya kukaimisha kwa muda mrefu iko kwa taasisi mojawapo naweza kuitaja ni ya *OSHA*. Mkurugenzi anayekaimu *OSHA* amefanya kazi muda mrefu tangu sisi tunaingia hapa, tulipowezeshwa kipindi cha mwanzo, huyu anakaimu na anafanya kazi nzuri mpaka sasa hivi. Niulize, hivi huyu Mkaimu mwanamama tena wa *OSHA* ataendelea kukaimu mpaka lini? Awamu ya Tano Mkaimu huyu alikuwepo, Awamu hii tulivyoingia kwa bahati ya kuwezeshwana wajumbe wetu watu wazuri sana tumemkuta tena anakaimu. Sasa nishauri Ofisi ya Waziri Mkuu ichukue hatua ya kuwa-*sort out* hawa watu mapema sana, ingawa shida hii ipo pia kwenye taasisi nytingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nigosie masuala ya watu wenye ulemavu. Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua za dhati kuimarisha kitengo cha kuratibu masuala haya na jambo zuri nipongeze Wizara hii imeongeza bajeti kutoka milioni 978.50 kwenye mwaka 2019/2020 hadi bilioni 1.29 kwa mwaka 2021/2022. Hili ni jambo zuri na hili

kundi litafaidika kwa programu mbalimbali zitakazoandaliwa.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko shida nyingine inayoikumba ambayo haijafanyiwa kazi ambayo ni kutokuanzishwa kwa kanzidata. Kwa hiyo tunashauri kuanzishwe kanzidata ili kuweza kuwajua watu hawa wenyewe ulemavu kwa nchi nzima. Hii itasaidia kuratibu vizuri mipango kwa kuwatambua na kujua nini shida zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye jambo letu hili ambalo linatuadhibu sana katika Taifa hili, nalo ni maambukizi ya maradhi ya UKIMWI. Tunahitaji huduma kukabiliana na kadhia hii, kwa hivyo Mfuko huu wa UKIMWI lazima uweze kutunishwa. Hapa nazungumzia Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI wa ATF, Serikali ichangamkiele kutenga fedha zaidliz za ndani na kuzitafuta kama tozo kutoka sehemu yoyote ambayo itaona inafaa mradi Mfuko huu uweze kutuna kwa sabbau kazi yake ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba kusisitiza kampeni ya kuwezesha wanaume zaidi kufanyiwa tohara. Kwa sababu ugunduzi wa kisayansi umegundua maambukizi ya UKIMWI yanatokana na shida hiyo. Kwa hivyo hilo jambo lifanyiwe kazi, kampeni tuipige, tuhakikisha na kama itabidi pia basi tutakwenda kujifunza namna gani ya kucheza jando kwa watu wa Mtama huko. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa za kulevy; hii ni kadhia kubwa sana inayolikumba Taifa letu. Fedha za kutosha inabidi zitengwe ili kudhibiti na kuhakikisha kwamba kundi hili, Mfuko huu wa Kudhibiti Dawa za Kulevy unaafanyiwa kazi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wenzangu waliota pole kwa kuondokewa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ngumu sana kusahau yale ambayo yamefanywa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa Watanzania wote bado wana kumbukumbu ya urithi ambaao ametuachia kwa miradi mikubwa ambayo ameitekeleza hapa nchini. Naamini karibu kila Mtanzania ameguswa kwa sababu Dkt. John Pombe Magufuli alifanya kazi ya kujitoa kuwatumikia Watanzania kwa nia moja na kupeleka miradi karibu kila sehemu. Hakuna asijejua dhamira ya Mheshimiwa Rais aliyokuwa nayo. Amejenga barabara, karibu kila mkoa kuna alama alizoziacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati amejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo litawanufaisha Watanzania wote kwa kupata umeme ambaao utakuwa na gharama nafuu. Bado amejenga meli kwenye maziwa makuu, ziwa Victoria kuna ujenzi wa meli mpya na amekarabati meli ya MV Victoria na MV Butiama. Ziwa Nyasa kuna meli mbili ambazo zimejengwa, Ziwa Tanganyika kuna mpango wa kukarabati meli ya MV Lihemba na kuna ujenzi mpya wa meli ndani ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, amejenga bandari na kukarabati bandari; Bandari ya Mtwara, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, haya yote yamefanywa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Amenunua ndege ambazo kimsingi zinaonekana na zimepata alama ya Taifa letu, huko nyuma tulikuwa na ndege moja tu, ameacha ndege nane

na ndege tatu zilishanunuliwa japo kuna maneno mengi ambayo wananchi wanazungumzia ambayo hawafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege lilianza kuwekezwa upya na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa hiyo ustawi wa shirika hili hauwezi kustawi kwa muda mfupi kwani uwekezaji wake umetumia gharama kubwa na hasara ambazo zinasomeka kwa sasa ni za kawaida kwa mashirika ya ndege. Jirani yetu Shirika la Kenya Airways wamepata hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 600 katika kipindi hiki ambacho tulikuwa na matatizo ya *Covid*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie sana ujenzi wa reli. Wapo ambaao wanapotosha ukweli, mimi na Kamati yangu kwa ujumla tumeshuhudia mradi wa reli ambaao umejengwa kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ulishakamilika. Hatua ambayo imefikiwa kwa sasa ushauri wangu kwa Serikali naomba katika kipindi wanakamilisha zile asilimia 97 ambazo zimefikia kwa sasa, tunaishauri Serikali wajipange kwa wakati ili wanunue vichwa vyta treni, wanunue mabehewa ili treni ile ianze kufanya kazi. Pengine yale maneno yanazoyungumzwa yatakuwa yamekatika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kipande cha reli cha kutoka Morogoro – Makutupora nacho kimejengwa kwa sasa karibu asilimia 60. Maendeleo ni mazuri sana, naishauri Serikali kwamba pamoja na jitihada ambazo zinajenga reli kipande cha kutoka Mwanza – Isaka, tunaomba Serikali sasa iijipange haraka kuhakikisha kipande cha kutoka Makutupora – Tabora kinajengwa ili reli iweze kukamilika. Tunafahamu mipango ya reli kipande kingine ni kukitoa toka Tabora kwenda Kigoma na kutoka Kaliua kwenda Mpanda na Mpanda hadi Karema ambako kunajengwa bandari. Niiombe sana Serikali iweke mahusiano na nchi jirani ya *DR Congo* kuhakikisha wanatengeza mahusiano ya kibiashara ili tuweze kuitumia vizuri fursa ya bandari. Naamini Serikali iliratibu vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naomba Serikali iangalie ni mradi wa maji wa kutoka Ziwa

Tanganyika kuleta maji Mkoa wa Katavi. Huu ni mradi ambao utawasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Katavi na mikoa jirani. Mradi huu ukikamilika utatoa fursa kubwa sana. Mradi mwininge ambao tunautegemea sana Mkoa wa Katavi ni Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Tayari Serikali imetoe fedha, lakini tunaomba kasi ya utoaji wa fedha iongezeke ili tuweze kupata huduma ile ya kimsingi inayohitajika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo. Huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi hii kama hujazungumzia kilimo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia mazao makuu ya pamba, tumbaku, kahawa, korosho, mkonge na mazao mchanganyiko. Mazao haya yanahitaji usimamizi mkubwa sana na Serikali inahitaji iwekeze ipasavyo ili kuweza kukuza uchumi. Unapokuza uchumi kwa mkulima utakuwa umetengeneza uchumi kwenye maeneo yote ambayo yatazaa viwanda kutokana na rasilimali iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kilimo kunahitajika sana kitengo cha masoko kiweze kuimarishwa ipasavyo kwani eneo kubwa ambalo kuna shida kubwa sana kwenye mazao pindi yanapozalishwa ni uhaba wa masoko. Niombi Serikali ihakikishe inafuatilia masoko hasa ya nje kwenye mazao haya ambao ni ya kimkakati hasa yale ambayo sio ya chakula ambayo yanahitaji mfumo mzuri wa mawasiliano ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tukihitaji kutengeneza uchumi wa nchi hii ni kuwasaidia wafugaji na wavuvi. Kwenye maeneo haya bado Serikali hajiajwekeza fedha za kutosha kwani tukiwekeza kwenye maeneo haya ya ufugaji tutawasaidia sana wananchi. Maeneo ambayo tunahitaji Serikali ipeleke fedha za kutosha tuboreshe *ranch*, *ranch* za Taifa zitakapokuwa zimeboreshwa zitawafanya sasa *ranch* waweze kununua mazao kutoka kwa wananchi wale wa chini wafugaji na vile vile tukiimarisha viwanda kwa ajili ya kuchakata samaki vitasaidia kukuza uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ajandae.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya na majukumu mengi ambayo wanayabeba kwa umahiri na weledi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kabisa kwamba timu hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiendana sasa na kauli mbiu mpya ya kazi iendelee chini ya mama yetu mama Samia Suluhu Hassan ambaye tunamuombea sana Mungu amjaalie hekima na maisha marefu, nina hakika tutakwenda vizuri watatufikisha salama tunapotakiwa kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia maeneo matatu. Eneo la kwanza ni juu ya suala zima la hifadhi ya jamii. Niipongeze Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii kwa muda mrefu imetufanya kazi nzuri hasa maeneo ambayo wamekuwa mabingwa zaidi wa kuwekeza la *real estate*. Eneo hili ni eneo ambalo ni *stable* kwenye uchumi, huwa haliyumbi sana, hata likiyumba huwa linarudi sawasawa, kwa hiyo nawapongeza wamefanya kazi nzuri, wamesaidia sana suala la kuungeza makazi bora. Tunafahamu kwamba nadhani mwaka 2018 *urbanization rate* ilikuwa asilimia 32.6 bila kuwa na juhudzi za kupata makazi bora tunaweza kuishia kukaa kwenye *slums*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na-*declare interest* kwamba niko kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, kwa hiyo tulipata fursa ya kutembelea miradi ya ujenzi ya NSSF ya Dungu, Toangoma na Mtoni Kijichi. Miradi ile ni mizuri na ilibeba maono makubwa. Hata hivyo, tukiangalia hatua ambazo ile miradi mbalimbali imefikia, mbele bado ni parefu na nadhani iko haja ya Serikali kufanya *intervention* kusaidia

ile miradi. Ushauri wangu ni kwamba kwa vile ziko fedha nyingi za kukopesha watu katika mambo ya *mortgages* hasa kuitia TMRC na benki zinazo hiyo fursa ya kukopesha lakini zinashindwa kwa kukosa wateja kwa sababu ya masharti kuwa makali. Ningeshauri katika hatua hii Serikali iandae *stimulus package* kwa ajili ya mabenki ambayo yako tayari kuwakopesha watu kununua zile nyumba. Tusipoweza kukopesha watu wakanunua zile nyumba nadhani ile miradi haitakwenda vizuri, haitatimiza makusudi yale ambayo yalikuwa yamelengwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *stimulus package* ni la kawaida kabisa kwenye uchumi mahali popote pale kunapokuwa na kamgogoro/kamyumbo fulani. Kwa hali hii iliyotokea tunahitaji kuziwezesha benki zetu zikopeshe watu kwa chini ya asilimia 10 ya riba ili waweze kunua zile nyumba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni juu ya suala la Mahakama. Tumezunguka kama Kamati tumeona maboresho kwenye Idara ya Mahakama kwakweli upande wa majengo na TEHAMA wanafanya vizuri sana, lakini liko eneo moja ambalo labda hapo kabla sijaenda nishukuru kwamba hata katika Jimbo langu la Mwanga pia tumepata jengo la Mahakama zuri, mkandarasi anasubiriwa tu kuingia *site*, lakini tayari mkataba umeshasainiwa. Hata hivyo kiko kipande kimoja ambacho naona kimeachwa pembedi kwa sababu tu ya sheria na pengine kitakuja kutusumbua mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, illiamuliwa hapo awali kwamba, Mabaraza ya Ardhi yatolewe nje ya Mfumo wa mahakama. Kwa kweli, uamuzi huu pamoja na kwamba, umefanyika lakini haujawa na tija sana. Kwanza mabaraza haya yako machache, kuna wilaya nyingi ambazo hazina mabaraza ya ardhi ikiwa ni pamoja na wilaya yangu ya Mwanga. Ushauri wangu ni kwamba, Mabaraza ya Ardhi haya yarudishwe chini ya mahakama, ili yasiachwe nje ya haya maboresho ambayo yanafanyika yakaja kuachwa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hayo yanaendelea ni jambo ambalo linawezekana kabisa tu kwa kutumia *circular* la Mheshimiwa Jaji Mkuu, mahakimu wale wa mahakama za wilaya wakapewa mamlaka ya kuendelea kusikiliza masuala ya ardhi. Kama mahakama kuu imewezezana hilo hata hizi mahakama za chini inawezekana, migogoro ya ardhi ni moja ya sehemu kubwa sana inayozisumbua jamii zetu na hasa kwangu. Sisi ni wapare tunapenda na tunaweza kesi, tunahitaji baraza la ardhi pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho limeshazungumziwa na baadhi ya watu hapa, ni eneo la maafa. Yako maeneo ambayo kila mwaka yanakumbwa na maafa. Mojawapo ya maeneo hayo ni kata ambayo ipo kwenye Jimbo langu la Mwanga, Kata ya Kileo. Yako mafuriko ambayo huwa yanaanzia Mto Hona, kila mwaka wananchi wale wanapata mafuriko wanakuwa ni watu wa kusaidiwa nguo na chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tulifanya jitihada za kwenda kutembea mguu kwa mguu na viongozi wale madiwani wa kata ile ya Kileo pamoja na viongozi wa kata ya Jirani kwa Mheshimiwa Dkt. Kimei, Kata ya Kahe Mashariki. Tukatembea mguu kwa mguu pamoja na wataalamu kutoka Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Pangani ambayo nayo ni Mamlaka inayofanya vizuri sana, tunaipongeza. Tulibaini kwamba, eneo linalohitaji kudabuliwa pale ili tuondokane na shida hii ni kilometra 1.72 ili mto ule uweze kuitisha maji mafuriko yale yakome.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunavyozungumza hatujaweza bado kupata *grader*la kufanya hiyo kazi. Wako wafadhili binafsi ambao wametusaidia tukadabua sehemu kubwa ndio ambayo mpaka sasa hivi inafanya mvua zilizonyesha tusipate mafuriko. Lakini nilikuwa naongea na Mheshimiwa diwani wa pale anasema Mheshimiwa Mbunge tuko kwenye *dilemma*, tuombe Mungu alete mvua au aache kwasababu, ikija tutapata mafuriko ikikosa tutakosa chakula. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe mwito kwamba, maeneo kama haya yatazamwe ili maafa haya yasiwe ni suala la kila mwaka kwamba, ikifika mvua zikikaribia watu wanajijua kabisa kwamba, wanakaribia kulala nje na kupoteza vyakula. Kwa hiyo, huo ndio wito wangu kwa eneo hili ambalo liko ndani, maafa haya ambayo yanatokea kwenye Jimbo la Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia zote. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa Rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele yako, mbele ya Bunge Tukufu hili kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa hotuba nzuri iliyojaa matumaini, iliyosheheni kila kitu. Naamini kabisa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ikienda kutekelezeka hii naamini kabisa kwamba, tayari sio hatuko kwenye uchumi wa kati, tuko kwenye uchumi wa juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kwenye suala zima la afya. Niipongeze Serikali yangu tukufu kwa kujenga vituo vya afya vingi nichini pamoja na zahanati. Ombi langu, hebu sasa Serikali ione namna gani itapeleka vifaa tiba na dawa katika hospitali zile ili, naamini kabisa Serikali ikishapeleka dawa na vifaa tiba naamini kabisa wananchi wetu watapata huduma stahiki na wataishi na afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye tiba asili. Enzi za mababu zetu walikuwa wanatumia dawa hizi za asili, lakini

mababu zetu wale walikuwa wanaishi miaka mingi sana tofauti na sasa. Kwa nini sasa sisi hatuwezi kuwaenzi mababu zetu kwa kutumia tiba zetu za asili?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii watu wanasema tunaenda kidigitali. Ushauri wangu niombe sasa tiba zetu za asili hizi zitumike. Mfano mzuri mwaka jana, nakumbuka ilikuwa mwezi wa tatu, Taifa letu lilikumbwa na ugonjwa wa *corona*, lakini Rais wetu Hayati Dkt. Magufuli alisimama kidedea na kutamka kwamba, taasisi za dini waombe misikitini pamoja na makanisani. Pamoja na hayo akasisitiza nyungu ziendelee na wale ambao wana fani zao za tiba za asili waendelee nazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli ilifanyika vile, nadhani umeona mafanikio makubwa sana; hivyo basi, kwenye mpango huu, kwenye hotuba hili sijaona hata bajeti ya tiba ya asili. Nikuombe Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, baada ya hotuba hii...

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mariam Ditopile.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kumpa Taarifa muongeaji. Ni kweli kwa dhahiri tumeona mchango wa dawa za kienyeji kwenye kutibu gonjwa hili la *Covid 19*, hasa dawa ambayo yeye mwenyewe ndio ameibuni ya *Shekilindi Bosnia Covid 19 Anti-Covid*. Naomba nimpe Taarifa hiyo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, napokea Taarifa hiyo, lakini nataka nimwambie sio dawa za kienyeji ni tiba ya asili, tiba mbadala tiba ya asili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia hususan katika suala hili. Dawa hii imefanya vizuri sana, imefanya vizuri kiasi kwamba, hata wataalamu wetu wa dawa hawa wa kisasa naamini wali-*appreciate* kwamba, dawa Hii ni safi na salama. Niombe sasa, huoni sasa umefikia wakati wa kupaisha dawa zetu? Huoni sasa umefikia wakati Serikali i-*support* watu wa tiba asili na tiba mbadala kwa ajili ya kunusuru Taifa letu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, na nikuhakikishie dawa zetu hizi zinafanya vizuri, lakini nataka nikuhakikishie kwamba, wataalamu, watafiti nikiwemo mimi, tumegundua dawa zenyé kutibu magonjwa mengi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Kwanza kabisa inatibu *corona*, inatibu UKIMWI, inatibu *cancer*, inatibu kisukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Asante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Parezzo, Mheshimiwa Lucy John Sabu ajiandae. Waheshimiwa maombi ya wachangiaji bado yako mengi hapa na kwa muda wetu ambao tumefunga leo, inabidi wachangiaji wanaofuata ni dakika tano.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia jioni hii ya leo, lakini kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima, afya, hatimaye nimeweza kusimama mahali hapa siku hii ya leo. Nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ni hotuba

ambayo imetuonesha tulikotoka, tulipo na tunakotaka kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, tumeona wametenga bilioni mbili na milioni 600, lakini milioni 600 ni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za ofisi na bilioni mbili ni kwa ajili ya maafa. Niombe sana kwasababu kila mwaka tunapata mabadiliko ya tabia nchi, tunapata maafa na majanga mbalimbali, niombe sana fedha hizi ziongezwe ili ziweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika Jimbo langu la Mvomero katika Kata ya Muhonda na Kata ya Sungaji vijiji zaidi ya vitatu viro kwenye hatari. Na mwaka jana tulipoteza nyumba zaidi ya 150 ziliondoka na mto, lakini mwaka huu vijiji vile ambavyo viko pembezoni yam to viro kwenye hatari kubwa sana ya kuondoka na mto kama mvua zitaendelea kunyesha mvua kubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana wenzenetu wa mazingira watusaidie kwenda kuona yale maeneo ili kuweza kuokoa nyumba ambazo zipo katika maeneo hararishi. Tunaweza tukapoteza vijiji kwa pamoja zaidi ya vitatu kwa hiyo, niombe sana waweze kusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunatambua kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa hili, lakini tuna tatizo moja ambalo tukichangia wengi tunajisahau, Maafisa Ugani ambaao kimsingi hawa ndio wataalamu wa kilimo na sisi wananchi wetu wanalima kupitia jembe la mkono. Maafisa Ugani wengi wanakaa maeneo ambayo hakuna kilimo, wanatoka katika vijiji wanakwenda kufanya mpango wa kuishi katika maeneo ambayo kwao ni rafiki, wale wakulima wetu kule walipo hawana wataalamu na tunajua kila mwaka kunakuwa na mabadiliko ya kalenda ya kilimo kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Wilaya yetu ya Mvomero ina tatizo kubwa sana la tembo. Tumepata bahati

ya kupakana na Hifadhi ya Mikumi, lakini bahati hii sasa imegeuka kuwa laana kwa watu wa Mvomero, tumeshapoteza zaidi ya watu 23 mpaka sasa hivi. Na jana niko hapa nimetumiwa *message* mwananchi mmoja amekanyagwa na tembo kichwani na nimewachangia nikiwa hapahaha ndani ya Bunge, lakini hali ni mbaya hakuna mwananchi yejote ambaye analima katika maeneo ya Tarafa nzima ya Mlali zaidi ya kata sita hakuna mtu ambaye anashughulika na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana kwa Serikali waende wakatusaidie. Tusipoenda kuwasaidia kuwaondoa wale tembo ambao wako katika lile eneo la Tarafa ile ya Mlali tutashindwa kulima. Nilienda kumuona Waziri wa Maliasili, alinipa ushirikiano, alituma timu yake ilikwenda, lakini tatizo bado liko palepale, lakini mbaya zaidi sheria ambayo iliwekwa kwa ajili ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inasema eka moja shilingi 150,000/= lakini mbaya zaidi mtu ambaye amelima chini ya eka moja hawezi akalipwa fidia kwa mujibu wa sheria. Sasa niombe sana tufanye mabadiliko kidogo katika eneo hili kwa sababu, tunajua wakulima wetu wengi wanalima chini ya eka moja. Lakini mtu mwenye chini ya eka moja akipata madhara ya tembo basi hawezi akapata fidia yoyote, lakini wale ambao wamefariki dunia wanatakiwa kwa mujibu wa sheria walipwe shilingi 1,000,000/=, lakini mpaka sasa hivi wananchi wengi bado wanadai hizi fedha na hawajui lini watalipwa hizi fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna hawa watu wanaoitwa *TFS*. *TFS* ni tatizo sana nchi hii, hawa ni Wakala wa Misitu Tanzania, sisi tunapotoka kule vijijini shule zetu nyingi hasa za pembezoni hazina madawati na tunayo misitu ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoenda kuomba vibali kunakuwa na urasimu mkubwa sana wako tayari kuona miti inaanguka na kuoza, lakini sio kutoa kibali kwa ajili ya kuvuna na kutengeneza madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hawa ndio wanasi mamia hifadhi zetu Tanzania. Wanaacha wananchi wetu wanaingia kwenye hifadhi, wanaanza kusafisha shamba, wanapanda, wanalima, kama ni mahindi ama mpunga, wakifika kwenye hatua ya kuvuna ndio wanakuja na kuanza kuharibu mazao yao, lakini wakati wanafanya maandalizi ya kupanda wanawaangalia. Kwa hiyo, niombe sana hawa watii wa *TFS* kuna mambo mengi sana ambayo Serikali inatakiwa wafanye mabadiliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Haya, kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, imegonga ya kwanza.

NAIBU SPIKA: Zikiwa dakika tano wanagonga moja.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy John Sabu. Mheshimiwa Stanslau Haroun Nyongo ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu. Na kwasababu, muda ni mfupi basi nitachangia katika jambo moja na kama itatosha basi, nitaenda kwenye jambo la pili. Ninapenda kuishauri Serikali katika suala zima la wafanyabiashara wetu hapa nchini. Tunatambua umuhimu wa wafanyabiashara na lazima Serikali ilione hilo kwasababu hawa wafanyabiashara wakifanya biashara katika mazingira rafiki, kwa maana ya mazingira ya amani yenye kutenda haki ndivyo ambavyo watalipa kodi na wakilipa kodi ndivyo ambavyo hii mipango yote tunayoiongea humu Bungeni inaweza kwenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia huko nyuma jinsi ambavyo wafanyabiashara wengi wamepitia kadhia mbalimbali. Na tunamshukuru Mheshimiwa Mama Samia angalao ameliona hilo na ameanza kulisemea kuhusiana na changamoto ambazo wafanyabiashara wanazipata. Sasa pamoja na Mheshimiwa Mama Samia kulisemea, tunaomba watendaji walioko chini wanaosimamiwa na Mheshimiwa Rais haya anayoyasema yaende kutekelezwa kwa vitendo kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatendewa haki, wanafanyiwa makadirio ya kodi ambayo ni rafiki na yanalipika. Lakini kama haitoshi wanahakikisha kwamba, sheria, taratibu na kanuni zilizoko zinatekelezwa, ili mwisho wa siku huyu mfanyabiashara aliye ile kodi ambayo anastahili kulipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ni muhimu kitazamwe na Serikali ni lazima kuwepo na viwango vya kodi ambavyo ni *reasonable*, ili mfanyabiashara aweze kulipa, lakini pia tusifirkirie kuweka wigo makadirio makubwa ya kodi, tukipunguza makadirio ya kodi tutawafanya wafanyabiashara wengi walipe kodi na kodi itaongezeka. Ukifanya kodi kuwa kubwa maana yake utawapunguza wafanyabiashara, lakini ukipunguza utaongeza na wengine wengi watalipa kodi bila kusumbuana, bila bughudha yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Tano kulikuwa kuna *task force* ziliundwa, na hizi *task force* zimewafuata baadhi ya wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi zikawafanya uhakiki wa hesabu kwa miaka mitatu, mitano ya nyuma iliyopita. Tunatambua kuna tamko limeshatoka, lakini tunaomba hilo tamko liwe kwa vitendo, kuna wafanyabiashara bado leo wanaambiwa wana *document* wanaambiwa walipe. Hawa wafanyabiashara walishalipa kodi kwa utaratibu unaotakiwa wakapelekewa *task force* wakaanza tena kukagua kwa upya wanaambiwa tena walipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ilifanye hili kwa vitendo kwasababu, nimeona Waziri wa fedha

amelisema kupitia vyombo vya habari, lakini hawa watu watapataje *comfort* kama hawana hata *document* kutoka *TRA* kwamba, zile hesabu zako za nyuma sasa hatuzifanyi kazi tena tunatizama mbele. Kwa hiyo, niishauri Serikali wafanyabiashara wote ambao wamepitia adha hii tunaomba muwape *comfort* ama uhakika wa hayo kwa kuwaandikia barua ili wawe na amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kati ya mwaka 2019 na mwaka 2020 wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha katika Mkoa wa Arusha na maeneo mengine nchini hao nao ni kati ya watu ambao wameumizwa kwa kiwango kikubwa na hawajui hatima yao. walipelekewa *task force* wakanyang'anywa fedha zao tena ni unyang'anyi, wakachukua fedha zote zikaenda Benki Kuu, wakiuliza sababu hakuna sababu. Na tukumbuke utaratibu unasemaje, mfanyakibashara ye yeyote anapotaka kuanzisha biashara yoyote lazima apate *TIN Number*, apate leseni ya biashara, kabla ya leseni ya biashara maana yake atapata *tax clearance*. Maana yeke huyu hana shida yoyote anapewa hiyo leseni ya kufanya biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha katika Mkoa wa Arusha na maeneo mengine walikuwa wamefuata *procedure* zote za kuanzisha biashara, wakawa wana leseni zote tena leseni Hai, wanalipa kodi inavyotakiwa, lakini ikaja *task force* kwa bunduki, kwa magari mengine ambayo hayajulikani sijui namba zipi, wakakwapua fedha zao zikarudishwa *BOT*. Tunaomba kufahamu nini hatima ya wafanyabiashara hawa? Kwa sababu, walikuwa wanaendesha biashara kihalali kabisa, mmewachukulia fedha zao; Serikali inaema nini kuhusiana na hawa watu ambao mmewanyang'anya fedha? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi hata wako wengine ambao wamepoteza maisha kwa matukio ya namna hii. Mtu unamnyang'anya karibia bilioni kumi, ishirini na anafanya biashara kihalali matokeo yake mtu anafariki kwa *pressure*, kwa mambo kama haya. Na hawa mnawafidia

nini kwasababu wana familia wana watu waliowaacha kwa hiyo, ni vema mkalitizama hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi kuna wafanyabiashara wengine wapo magereza leo kwa kubambikiziwa kesi za uhujumu uchumi, kukwepa kulipa kodi wakati wanalipa kodi, hatujasikia nao hawa mnawafanya nini? Tunatamani kuona yale ambayo Mheshimiwa Mama Samia ameyanena basi tuyaone kwa vitendo kwa watu kama hao ambao wameonewa kwa namna moja ama nyininge haki itendeke, watoke wawe huru, kama kuna sheria ambazo tunahitaji kuzifanya marekebisho Serikali mzilete hapa Bungeni tufanye marekebisho Watanzania wafanyabiashara wafanye biashara kwa uhuru, haki na amani lakini wakijua wajibu wao ni kulipa kodi ambayo inaweza ikalipika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy John Sabu atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mheshimiwa *Engineer* Aloyce Kamwelwe ajiandae.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mezani. Nami nitajikita katika uvezeshaji wa wananchi kiuchumi hususan katika ujuzi kwa vijana na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa juhudini mbalimbali ambazo imekuwa ikizifanya hususan kwa vijana kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi Kitaifa. Kupitia programu hii, nafahamu kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kukuza ujuzi kwa vijana na ili waweze kujajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikiri kuwa mnufaika wa vijana hawa ambao wamekuwa wakipatiwa ujuzi kupitia vyuo vya *VETA* hususan kwenye kurasimisha ujuzi lakini pia *VETA* wamekuwa ni watu ambao wanawasaidia vijana hawa kuwashikiza hususan kwa waajiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana hawa kupatiwa ujuzi na kujajiri ni vitu viwili tofauti. Nikichukulia mfano, tulipokuwa na ziara ya Kamati tulitembelea *TIRDO* (*Tanzania Industrial Research and Development Organization*) ambapo tulikutana na vijana ambao wana ujuzi ama ubunifu wameweza kutengeneza taa ambapo zina uwezo hata kama ukiwa nje ya nyumba yako, wame-*install program* kwenye simu ukai-*request* kwamba zima ama washa taa hata kama ukiwa nje ya nchi. Changamoto inakuja kumekuwa na vijana wengi ambao wana ujuzi wa aina mbalimbali lakini wanashindwa kujajiri kwa kukosa mtaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi napenda kuiomba Serikali yangu na kuishauri kwa kuwa tuna Programu ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana ije na utaratibu wa kutengeneza fursa za kimkakati. Kwa mfano, tunao vijana ambao wana ujuzi wa ufundi seremala na kuna baadhi ya maeneo ambayo yana upungufu wa madawati, Serikali inaweza ikatengeneza fursa kwa vijana hawa wenye ufundi wa useremala kwa kutengeneza kambi rasmi na kuweza kuchukua vijana hawa kuwapa *tender* ya kutengeneza madawati kwa kuwapa *materials* na vitendea kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya vijana hususan kwenye Halmashauri zetu. Tunaishukuru Serikali yetu Sikivu, kipindi cha nyuma tulipiga kelele sana Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu makundi yalikuwa yakiundwa na watu kumi kumi lakini tarehe 26 Februari, kuititia Ofisi ya Wizara ya TAMISEMI ililengeza masharti ya mikopo na kuboresha zaidi kutoa nafasi kwamba hata wakiwa vijana watano wana uwezo wa kukopa mkopo huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matamanio ya vijana wenzetu ni kuwa mkopo huu uwe ni wa mtu mmoja mmoja. Kama Serikali imeweza kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja hususan kwenye mikopo ya vyuo vikuu, naomba na hili Serikali ilifanyie kazi. Hii ni kwa sababu mikopo ya watu kwenye makundi inakuwa ina mambo mengi, kila mtu anakuwa ana

interest zake kwenye *ideas* ambayo wanafanya kwenye biashara husika. Niiombe sana Serikali yetu sikivu iweze kutusaidia kwenye jambo hili ili liweze kuwa la manufaa zaidi kwa vijana wenzetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, niiombe Serikali yetu iendelee kutoa elimu kwa vijana wote ambao wanachukua mikopo kwenye Halmashauri. Nasema hivi kwa sababu vijana wanakuwa na *interest* tofauti tofauti, hivyo, mkopo unavyochukuliwa bila elimu ya kutosha matumizi yanakuwa tofauti na marejesho yanashindwa kufikiwa kwa wakati muafaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja iliyopo mezani. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Aloyce Kamwelwe na Mheshimiwa Omar Issa Kombo ajiandae.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa na mimi nipende kutoa shukrani nydingi sana kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Maswa Mashariki na niendelee kuwapa pole kwa msiba uliotukuta sote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nitoe pongezi kwa Serikali kwa kukubali kuondoa TMX kwenye manunuzi ya mazao yetu. Tatizo ilikuwa kubwa sana na kule kwenye Jimbo langu kwa kweli ilikuwa ni tatizo, hata kwa wale wanaokwenda kuza choroko kilo tatu, nne, tano ilikuwa inawapa shida sana kuza mazao yao kwa kupitia mtandao huu. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa usikivu na kwa kutoa maamuzi haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa mambo kama mawili au matatu. La kwanza, naomba nitoe ushauri kuhusiana na bandari yetu. Serikali yetu imeamua kujenga reli ya *standard gauge*, reli hii ina manufaa makubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Reli hii inakwenda kujengwa

kwenda kwenye mipaka ya nchi yetu lakini bado reli hii itategemea mzigo mkubwa sana kutoka nchi za jirani kwa mfano nchi ya Kongo, kila mwaka tumekuwa tukisafirisha shaba kutoka Kongo zaidi ya tani 500,000 hadi 700,000 kupitia bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajenga reli hii ni lazima tuone namna ya kuungana na wenzetu wa nchi za jirani ikiwezekana na kadri tunavyokuwa tukijinasibu na Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa anasema nchi yetu ni tajiri, nchi tajiri lazima isaidie na nchi jirani kuwa matajiri ili na yenyewe iwe tajiri zaidi. Ikiwezekana kwa namna yejote ile tuingie mikataba kuhakikisha kwamba Kongo, Zambia na nchi nyingine kwa mfano Rwanda na wenyewe wanakwenda kwenye *standard gauge*. Nia yake ni kuhakikisha mizigo hii inakuja kwenye bandari yetu na bandari yetu iweze kusafirisha mizigo mingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Bandari yetu ina uwezo wa kubeba au kuhudumia tani zaidi ya milioni nne kwa mwaka ya mizigo migumu yaani *hard cargo* lakini kuna mizigo ya *liquid* zaidi ya tani milioni 4.5, mizigo hii inapitia kwenye bandari yetu kwenda upande wa nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalotaka kuzungumza leo, nimesoma Mpango wa Maendeleo, nimeangalia *strategyza* watu wetu ambazo wanaziandaa kwenye masuala ya bandari zetu nimeona ujenzi wa meli za kufanya huduma katika nchi yetu. Ni lazima sasa tufikirie kutengeneza reli kubwa za kusafirisha mizigo kutoka bandari yetu kwenda nchi nyingine za mbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukibeba shaba tukaitela kwenye bandari yetu ikakomea hapo zikaja meli nyingine kubwa zikabeba mizigo kupeleka nchi nyingine tunakuwa tumewapa biashara watu wengine. Faida ya pili meli kubwa zikibeba mizigo kutoka kwenye bandari yetu kwenda nchi za mbali mfano China, India na maeneo mengine zitakwenda kubeba bidhaa nyingine zitaleta kwetu;

huduma au bidhaa kutoka nchi nyingine zilizoendelea *cargo* hizo zitaletwa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli haiwezi kuja nchini kwetu bila kuwa na uhakika wa kubeba mzigو mwingine. Kwa hiyo, inapokuja kwenye bandari yetu ikakuta mzigو mingi imeletwa kwa *standard gauge railway* kwenda kuipakia kwenye ile meli nyingine itakwenda kutusaidia kuleta *commodities* nyingine kutoka nchi nyingine. Lazima hiyo biashara tuchungulie tuifanye. Tusiachie Rainier, Messina na Maersk wanakwenda kuchukua mzigو yetu kutoka kwenye bandari yetu kwenda kwenye bandari nyingine wanafanya biashara halafu sisi tumepaki tupo *idle*, tunaomba tufanya biashara kupitia bandari yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka kulingelea ni kuhusiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kushughulikia masuala ya UKIMWI. UKIMWI tumeudhibiti, sasa hivi magonjwa ya UKIMWI yanauwa kwa kiwango cha asilimia 4.2 tu. Magonjwa yanayouwa Watanzania wengi ni *non-communicable diseases* na ugonjwa unaoongoza ni wa moyo unauwa asilimia 30.6, unafuatiwa na *cancer* inauwa asilimia 15 inafuatiwa na magonjwa ya figo na magonjwa mengine pamoja na kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumtibu mgonjwa mmoja wa magonjwa ya moyo na kisukari kwa mwaka siyo chini ya shilingi milioni nne. Ofisi ya Waziri Mkuu ibebe suala la *non-communicable diseases*. Kitu kikubwa ambacho kinashauriwa na wataalam ni watu kufanya mazoezi na kula chakula bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Miaka Mitano pamoja na Wizara ya Afya nimepitia katika Kamati mipango yao, hatuoni juhudzi za kufanya mazoezi, hatuoni juhudzi za kuzuia magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba waingize hili katika mipango yao kila Wizara ije na mikakati ya magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Issa Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Omar Ali Omar ajiandae.

MHE. OMAR ISSA KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ambayo iko mbele yetu kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili Tukufu na kuweza kuchangia, naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa. Vilevile nichukue fursa hii kukishukuru sana Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kunihamini kuweza kupeperusha bendera katika nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Wingwi katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2020. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo la Wingwi kwa imani yao kwangu. Sambamba na hilo, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Wingwi kwa imani yao kwangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Ofisi yake kwa hotuba nzuri iliyojaa maono ya viongozi wetu pamoja na llani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Vilevile nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoanza kuchapa kazi katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wingwi na kwa niaba ya wananchi wa Pemba hatuna shaka hata kidogo kama Wanzanzibar kwamba Muungano wetu upo kwenye mikono salama chini ya Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili amelidhihirisha siku anamuapisha Mheshimiwa Makamu wa Rais alipomwambia aanze kuzifanya kazi changamoto za Muungano. Hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ataendelea kuboresha, kuuendeleza, kuuenzi na kuulinda Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli Serikali yetu inafanya jitihada kubwa sana katika kuuenzi na kuulinda Muungano wetu. Kuna mafanikio makubwa ambayo tunayapata sisi Wazanzibar lakini watu wanajitia kuwa hawaoni wala hawasikii wala hawataki kuona mafanikio makubwa ya Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli changamoto 11 zillipatiwa ufumbuzi lakini wanaposimama hawataki kuyasema haya. Changamoto nimeiona, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali iweke utaratibu wa kwenda kwenye vyombo vya habari kueleza mafanikio na yale mambo ambayo yanafanya na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Zanzibar ili wananchi waweze kuona na kufahamu na kuelewa waepukane na kupotoshwa. Nasema hili kwa sababu kuna upotoshaji mkubwa kwamba Serikali haifanyi kitu katika suala la Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kuipongeza Serikali kwenye mradi mkubwa wa umeme. Nafahamu mradi huu ukikamilika tutaweza kupata huduma hii kwa unafuu mkubwa zaidi. Sasa niilombe Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Serikali, kwa vile nchi yetu tuna pande mbili za Muungano; upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara, uandaliwe utaratibu maalum au watueleze ni jinsi gani sisi Wazanzibar tutaweza kufaidika pindi mradi huu utakapokamilika. Licha ya kwamba tunalo Shirika la Umeme kule Zanzibar lakini tunafanya kazi kwa ushirikiano. Niombe wakae meza moja na sisi watuangalie kama wenzao ili tuweze kupata huduma hii itakayokuja katika hali ya unafuu mkubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa *Engineer* Aloyce Kamwelwe ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii adimu angalau dakika tano na mimi nichangie hotuba ilio mbele yetu. Kwa sababu muda ni mchache basi mimi nitautumia muda huu kuongea mambo ya wapiga kura wangu walionituma kuwawakilisha hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kukaa hapa zaidi ya miezi mitatu, tunachokifanya hapa ni kugawanya keki ya Taifa letu. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali, tunapokwenda kuigawa keki hii lazima tujue jiografia ya nchi yetu inatofautiana sana, maendeleo ya kanda moja kwenda kanda nyingine inatofautiana sana, kutoka mkoaa mmoja kwenda mkoaa mwengine inatofautiana sana. Kwa hiyo, iweipo juhudhi ya makusudi kuangalia ni namna gani ya kuisaidia ile mikoa au zile sehemu ambazo kimaendeleo zipo nyuma au kiuchumi zipo nyuma ili tuweze kwenda pamoja tusiwaache wenzetu. Natoa mfano hata Rais wa Awamu ya Nne aliamua kwa makusudi kuelekeza nguvu nyingi Kigoma, amejenga barabara nyingi sana kule, ili kwenda nao pamoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tusisahau kuna *element* moja ilikuwepo tangu zamani kwamba Mikoa ya Kusini ilikuwa ni ya adhabu; miaka ya 80. Naomba niiambie Serikali ile *element* bado haijafutika, bado ipo pamoja na kwamba Serikali zote Awamu Tano zilizopita zimejitahidi sana kuipunguza lakini hiyo *element* bado ipo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo naongea zipo barabara kwenye nchi yetu zimepitiliza zaidi ya 20, *life span* ya barabara zetu ni miaka 20, tayari kwenye bajeti hii zipo barabara hizo zinakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu pengine kuondoa ile lami ili waweke nyingine kwa sababu

life span yake imekwisha. Hata hivyo, mnapokwenda kufanya hayo mjue kwamba Nangurukuru - Liwale tangu tumepata Uhuru hatujaona lami. Mnapokwenda kufanya hayo mjue kuwa Mkoa wa Lindi hakuna wilaya hata moja ambayo inakwenda mkoani kwa barabara ya lami, ukiondoa Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Lindi Vijiji ambazo ziko kwenye hiyo barabara kubwa ya Kibiti-Lindi. Kwa hiyo, mnapokwenda kufanya hayo mjue kuna mikoa bado ipo nyuma inahitaji juhudzi za makusudi kuisaidia ili twende pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwingine, Wilaya ya Liwale ni Wilaya tangu mwaka 1975 leo tunazungumza ni miaka 46, lakini Wilaya ile mpaka leo Mkuu wa Wilaya, *DED*, *OCD*, Mganga Mkuu, Hakimu wa Wilaya na Polisi *OCD* hawana ofisi. Kwa mfano mzuri wale Mawaziri waliowahi kutembelea Wilaya ya Liwale wote tunawapokelea kwenye ile *rest house* ya Selous, vitabu vyote wanakuja kusainia pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asimame Waziri aniambie kama ameshawahi kuiona Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Liwale; Ofisi ya *DED* wa Liwale, asimame Waziri ye yote aseme ameshawahi kuona jengo la Polisi Wilaya ya Liwale. Wote tunakusanya pale kwenye jengo la Selous. Tunaishukuru Selous, wametujengea *rest house* ambayo ndiyo inatumika mpaka leo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana...

MBUNGE FULANI: Aibu!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ile wilaya ni ya mwaka 1975 na Mwalimu Nyerere alimpa Waziri wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Rashid Mfaume Kawawa Wilaya ile ya Liwale, lakini wilaya ile iko hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombeni sana, tunapokwenda kugawa keki hii, tuiangalie mikoa ile ambayo iko chini. Mkoa wa Lindi na Mkao wa Mtwara ni mikoa

ambayo iko nyuma kwa barabara, ndiyo maana tukaomba barabara yetu ile ya korosho inayotokea Mtwara inakwenda Newala – Tandahimba – Masasi – Nachingwea - Liwale mpaka Ruangwa, muikumbuke ili tuweze kuinua uchumi wa watu wa kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Ali Omar atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Aloyce Kamwelwe* na Mheshimiwa Denis Londo ajiandae.

MHE. OMAR ALI OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu-Wataala aliyetupa uhai wa kuimillki siku ya leo tukawepo katika Bunge hilli. Pia niwatakie mfungo mwema kwa wale Waislamu na wenzetu ambaio sio Waislamu kwa kutuunga mkono kwa njia moja au nyininge katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kutoa kauli ya Mheshimiwa Marehemu Shaaban Robert; alizungumza katika kitabu chake cha Adili na Nduguze, akasema kwamba haja ikishughulikiwa kwa matendo humalizika upesi na ikishughulikiwa kwa maneno, huchelewa kama sadaka. Kwani tendo hukidhi haja maridhawa kulikoni maneno na mwenye matendo hula uhondo na asiye matendo hula uvundo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa ruhusa yako naomba nitoe kauli moja tu ya mshairi mmoja wa Kiarabu aliyesema kwamba *Inna Safina Tajir illa ljabas*. Hakika ya Safina haitembe katika nchi kavu. Nina maana ya kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, asiogope, asonge mbele na nina Imani kwamba Tanzania hii itapata maendeleo makubwa chini ya uongozi wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba sasa nijikite kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niende moja kwa moja katika ukurasa wa 71 ambaao ulikuwa unazungumzia kuhusu *cross cutting issues* au masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Visiwa vya Zanzibar; Kisiwa cha Pemba ni kisiwa ambacho kina ukubwa wa *square kilometer* 198 na Zanzibar 1,666. Visiwa hivi vimebarikiwa na neema kubwa; vimebarikiwa na neema ya visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka visiwa vikubwa hivi. Ila visiwa hivi vinapotea siku hadi siku. Suala la mazingira katika Visiwa vya Zanzibar ni tete. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mnamo mwaka wa 1970 huko, kule Tanga Kisiwa cha Maziwe kilipotea na sasa hivi tunajivunla visiwa vyetu vya Zanzibar; na kauli njema kabisa inayozungumzwa hata na *wahiribu* wakubwa pale Zanzibar wanasema, “*Zanzibar ni njema, atakaye aje.*” Hata hivyo ukiangalia visiwa hivi ambavyo tunavinadi kwamba Zanzibar ni njema, atakaye aje, kila siku vinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka maji ya bahari yanakula 5% ya visiwa vile. Kuna maeneo mengine ambayo, bahati nzuri mwaka wa 2019 Mheshimiwa Zungu alifika sehemu moja inaitwa Sipwese Kengeja. Akatembelea katika lile eneo na akaitaka idara inayohusika kufanya upembuzi yakinifu ili kuona athari kubwa ya kimazingira iliyopo katika eneo lile. Kisiwa kimoja tu, ni eneo moja tu hilo ambapo athari yake mpaka sasa hivi tunavyoongea ni kwamba maji ya bahari yanaingia kuzuia kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanaosoma katika shule, wanaotoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ambaao ni vijana wanaotoka Sipwese kwenda eneo lingine la kisiwa wanafunzi wanashindwa kwenda kusoma. Hata Magereza wameyahama maeneo yao, haiwezekani kulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima kubwa na taadhima, basi tufanye upembuzi yakinifu katika visiwa hivi nya Unguja na Pemba kuona je, athari ya mazingira iko kwa kiwango gani ili tuvhame visiwa hivi tuweze kuringia Muungano huu wa Zanzibar na Tanganyika? Kwani vikipotea visiwa nya Zanzibar, tayari tutakuwa hatuna tena nchi ya kusema kwamba tuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Aloyce Kamwelwe atafuatiwa na Mheshimiwa Denis Londona Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maneno machache ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kuungana na Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Katavi wamenituma pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais kwa kuondokewa na jembe letu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na ahadi yetu kwake yeye Mheshimiwa Rais, tutamuunga mkono, tutafanya kazi kwa bidii ili kuyaenzi yale yote ambayo yameachwa na Rais wetu Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba ambayo imegusa vipengele vyote nya dira iliyotolewa mwaka 2015 pamoja na dira iliyotolewa na hotuba ya Rais mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uchache wa muda, nitoe shukrani kwa yale yote ambayo yamefanywa katika Jimbo langu, hasa katika miaka mitano hiyo iliyopita

kwa kuanza na Wizara ya Ujenzi ambayo imeanza na inaendelea kujenga barabara ya kutoka Tabora kwenda Mpanda, barabara ambayo ni uti wa mgongo wa Mkoa wetu wa Katavi na hasa nipongeze kwa kukamilisha ujenzi wa Daraja la Ugala ambalo lilikuwa linafanya Jimbo langu lisifikasiwe na magari kwa muda miezi mitatu kila mwaka, lakini kuanzia mwaka huu pamoja na mvua hii, hatujapata hiyo shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba tu kwamba kuna barabara nyingine muhimu sana ambayo sasa hivi imeanza kutumika. Kuna mabasi yanatoka Mbeya yanapita Katavi yanakwenda Mwanza; na siku hiyo hiyo yatoka Mwanza pia yanaelekea kwenda Mbeya na barabara siyo nyingine, ni Inyonga - Maji ya moto kupita Mloo kwenda Kamsamba na inafika mpaka Mbeya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni *potential* kwa aina yake kwa sababu Ziwa Rukwa ndiyo Ziwa ambalo lina gesi ambayo ni ya muhimu sana inaitwa *Helium*. Ni nchi chache sana duniani ambazo zina gesi ya namna hiyo. Sasa ni muhimu sana kukumbuka kuanza kutengeneza miundombinu kwa sasa kabla hatujaanza kuchimba hiyo gesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru sana Wizara ya Nishati, juzi wamesaini mikataba yote kwa ajili ya *REA III*. Wamekamilisha sasa vijiji vilivyokuwa vimebaki katika Jimbo langu; Kijiji cha Ilunde, Kijiji cha Isegenezya, Kijiji cha Mapili ambacho mimi mwenyewe nimezaliwa, Kijiji cha Masigo na Kamalampaka, vyote vimeingizwa. Kwa hiyo, baada ya mradi huu kukamilika, jimbo langu litakuwa na umeme kwa asilimia 100. Nawashukuru sana Wizara ya Nishati; Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru Wizara ya Kilimo. Jimbo langu kwa asilimia 100 ni wakulima. Tunalima mazao ya chakula pamoja na mazao ya biashara na zao kuu la biashara ni Tumbaku. Kule tuna vyama vitatu

vinavyoshughulikia tumbaku. Tuna Chama cha Ukonongo, tuna Chama cha llela na tuna Chama cha Utense. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Ukonongo ndio ambacho kimekaa muda mrefu sana, lakini kilikuwa kimetengeneza deni kwa wakulima na hivi ninavyozungumza wakulima bado wanadai shilingi milioni 400. Namshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo, amefanya kazi kubwa na juzi Morogoro ametoa maelekezo. Kwa sababu *audit imeshafanyika*, kwa hiyo, nashukuru kwamba wakulima sasa watalipwa ile shilingi milioni 400. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imefikia uchumi wa kati, lakini imefikia uchumi wa kati kwa sababu ya ushirikiano tulionao sisi Watanzania lakini hasa nin kwa sababu ya hii mihimili mitatu ambayo ilifanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza kwa mhimili wa Bunge, umewajibika kwa kuchambua bajeti na kuzipitisha. Pia wakati wa utekelezaji, tukiwa kwenye Majimbo kule tulikuwa tunaangalia yale yaliyokuwa yamepangwa na Serikali kama hayatekelezwi tunakuja kutoa taarifa katika Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza mhimili wa Serikali ukiongozwa na Waziri Mkuu, ndio wametekeleza yote yaliyofanyika. Vile vile mhimili wa Sheria wa Mahakama ambaao umeleta utulivu kwa wananchi kwa kuondoa uonevu, ndio maana kila mtu amewajibika mpaka tumefikia sasa kwenye uchumi wa kati.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga.

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere ajilande.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mikumi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumnungu mwanafalsafa Frantz Fanon ambaye anasema kwamba kila kizazi kina jukumu la kihistoria. Ni jukumu la kizazi hicho kutafuta na kulifahamu jukumu lake. Aidha, ni jukumu la kizazi hicho kubeba hilo jukumu na kulitekeleza ama kulisaliti. (*Makofii*)

Mheshimwia Naibu Spika, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli akisaidiana na Makamu wake ambaye sasa ni Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, wanaingia kwenye historia ya nchi yetu kama wazalendo na viongozi amba walitambua jukumu lao la kihistoria, walilibeba na wallitekeleza. Maamuzi ambayo walichukua kuongoza Taifa letu katika vita dhidi ya wahujumu uchumi, vita za kiuchumi duniani, kurejesha imani ya wananchi kwa Serikali yao, kurudisha nidhamu ya utumishi Serikalini, ujenzi wa miundombinu ya barabara ya reli, ununuzi wa ndege, ujenzi wa vituo afya na miundombinu ya elimu, ni mambo ambayo yatawafanya waendelee kukumbukwa kwa vizazi vingi vijavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ameshaonyesha dira yake, ameonyesha azma ya Serikali yake katika kutekeleza miradi yote ya kimkakati na miradi ya kimaendeleo. Azma yake ni njema na azma hii sisi kama Bunge tunapaswa kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Bunge lako kuhakikisha kwamba kila mmoja ndani ya Bunge hili anatimiza jukumu lake la kihistoria katika kuhakikisha kwamba tunaenda

kuisaidia Serikali chini ya Rais Mama Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu yake, lakini pia kuhakikisha kwamba anafanya kila linalowezekana ili Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi itekelezwe. Ni jukumu la Bunge lako kuhakikisha kwamba tunaenda kutoa kila *support* ambayo Rais wetu anastahili ili nchi yetu itekeleze yale yote ambayo tumewaaahidi wananchi katika ilani ya chama chetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu siyo kisiwa, ni sehemu ya ulimwengu mkubwa ambao unaingia sasa kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda. Mapinduzi haya si lele mama, mapinduzi haya yanaenda kuwa katili kuliko mapinduzi yoyote ya viwanda. Tumejandaaje kuingia katika uchumi shindani na shirikishi katika mazingira ambayo bado vijiji vyetu vingi havijafikiwa na umeme lakini pia tuna tatizo kubwa la mawasiliano? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Jimbo la Mikumi katika vijiji 57 vya Jimbo langu, ni vijiji 23 tu ambavyo unaweza kupata mawasiliano ya simu ya uhakika. Maeneo makubwa ya Kata za Uleli Ng'ombe, Vidunda, Masanje, Kivungu, Kisanga na Tindiga hayana mawasiliano ya uhakika. Hata kwa upande wa umeme, ni vijiji 17 tu katika vijiji 57 ambavyo unaweza kupata umeme katika Jimbo la Mikumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii, tunapoenda katika uchumi shindani na shirikishi, hatuwezi tukahakikisha watu hawa wanashiriki kikamilifu katika uchumi huu wa mapinduzi ya nne ya viwanda bila kuhakikisha kwamba tunawaunganisha wananchi hawa kupitia mawasiliano na pia kuhakikisha kwamba tunawapa umeme. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, mengine ambayo...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele imegonga.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, tutamalizia na Mheshimiwa Francis Isack.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau kwa muda huu mfupi ili niweze kuchangia machache niliyonayo katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la elimu ambapo nitaongelea kuhusu ajira za walimu. Tunatambua na Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema hapa kwamba kuna uhaba mkubwa sana wa walimu katika shule zetu. Jambo ambalo nataka kuongelea ni namna ajira za walimu zinavyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za walimu hazizingatii mwaka wa kuhitimu. Inashangaza wakati mwingine mwalimu amemaliza chuo mwaka 2015 lakini anaajiriwa mwalimu aliyemaliza mwaka 2019. Kwa hiyo, kuna *gap* kubwa hapa na linafanya walimu wengine wakae mpaka wazeeke wafike miaka 45, kwa hiyo hawataajiriwa tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali kwamba katika kuajiri walimu, mwaka wa kuhitimu uzingatiwe; na ikiwezekana Wizara ya Elimu au kama ni TAMISEMI wafanye *research* waone ni walimu wangapi ambao wataajiriwa kutokana na mwaka wao wa kuhitimu. Wako waalimu ambao wana vigezo, maana mwalimu aliyemaliza mwaka 2015, ametoka chuo na yule aliyemaliza mwaka 2019 wana vigezo sawa, wametoka vyuoni. Kwa hiyo, unapoajiri wa mwaka 2019 na ukamwacha wa mwaka 2015 kwa mfano; Je, huyo ataaajiriwa lini? Kwa umri wake,

anaendelea kukua na mwisho atashindwa kuajirika kwa sababu atakuwa amevuka miaka 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kuhusu afya. Ni kweli mimi sijakataa, hata kwenye kampeni zangu sijakataa majengo ya hayakujengwa. Majengo ya zahanati yapo, tunachopaswa kuangalia ni je, katika majengo yale kuna nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu na hasa kwenye Jimbo la Bukoba Vijiji; nita-cite Bukoba Vijiji kwa sababu ndio kule kule ambako nimegombea mimi. Unapogombea, inakupa nafasi ya kujua watu wale ambao unataka kuwaongoza wamekaa namna gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa madawa upo, ukosefu wa wafanyakazi upo, lakini mimi nataka kujua hizi gharama za wananchi wanazolipia wanapokwenda kwenye matibabu katika zahanati hizi, ndio hoja yangu ya msingi. Napenda kujua haya maelekezo ya hivi viwango ambavyo nitavitaja saa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke anapopata mimba, nasemea Bukoba Vijiji na mahali pengine kama mpo mnasikia, kwamba ili uweze kuandikishwa siku ya kwanza ya kuanza *clinic*, unapaswa ulipe shilingi 10,000/= na ulipie shilingi 2,000/= ya daftari. Maana yake Serikali hii wameshindwa hata kile cheti cha *clinic* cha mwanamke cha kwenda nacho. Kwa hiyo, unapaswa ulipe shilingi 12,000/=. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, wanawake wanapokwenda kujifungua wanalipa kuanzia shilingi 30,000/= na kuendelea. Kwa hiyo, nataka kujua, hivi vigezo au hizi gharama nani alizipitisha? Maana yake ukienda ndani ya Halmashauri wanakwambia kuna Waraka. Ukiomba Waraka, wanasema hatutoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu maana hili jambo msilifanyie mzaha linaumiza watu huko vijiji,

wanawake wanajifungua ndani ya nyumba zao, wanakwepa hiyo 30,000/= kwani ni pesa nyingi. Ina maana tunataka kuwaambia watu waache kuzaana na dunia isiongeze, kwa sababu unapomchaji siku ya kwanza kwenda kliniki, huwa najiuliza hayo malipo ni kiingilio? Sasa nataka kujua hivi vigezo nani aliviweka na ni Wizara ipi, ni TAMISEMI au ni Wizara ya Afya? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimesikia kengele imegongwa, mambo mengine tutakutana huko TAMISEMI. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, tutamalizia na Mheshimiwa Francis Isack.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu. Kwanza nikushukuru wewe binafsi mama wa kazi, mama mzito, *software and hardware*, ambaye unafanya kazi kwa akili kubwa sana, mtu anaweza kukuona *simple* lakini uwezo wako ni mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Waziri Mkuu, huyu ni mtu mwema, Waziri Mkuu wetu niliwahi kumfananisha humu Bungeni kama Rashid Kawawa (Simba wa Nyika), ukimtuma kazi anafanya. Kufanya kazi na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli miaka yote hiyo, Mungu akubariki Mzee. Maana yake lile lilikuwa burudoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mawaziri wote, maana nimeona hapa Mawaziri wengine wameanza kuyumba, wana hofu mara baraza litakufa au litafanyaje. Fanya kazi kwa uwezo wako mambo ya Uwaziri ni dhamana, ikitoka unakuwa Mbunge kama sisi kuna kosa gani? Kwa hiyo fanya kazi kwa uwezo wako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie jambo moja muhimu, tutofautishe kati ya utendaji au utekelezaji wa Ilani wa Chama cha Mapinduzi au ilani anayoitekeleza Rais aliyeleo madarakani na nidhamu ya

diplomasia ya utendaji wa kazi, hivi ni vitu viwili tofauti. Leo Rais wetu Mheshimiwa Samia, akisema anakwenda Marekani hatuwezi kumzuia tukasema Rais Magufuli hakwenda, hiyo ni diplomasia ya utendaji, lakini leo Rais aliyeo madarakani akishindwa kutekeleza reli, akishindwa kujenga Bwawa la Nyerere, akishindwa kujenga shule zilizoko kwenye ilani, wananchi watatuhukumu kwenye Chama cha Mapinduzi, lazima atafanya tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Rais, Mheshimiwa Samia akisema Tundu Lissu njoo, usiwe kibaraka wa Nchi za Ulaya, njoo tukupe cheo hapa. Atakuja na atafanya, hatuwezi kuuliza. Kwa sababu kuna watu wa namna hiyo, wamefanya hivi na wakapewa na wakaishi. Hiyo ni diplomasia ya utendaji, lakini utekelezaji wa ilani upo pale pale, kwa hiyo, tutofautishe hayo mambo ndugu zangu ili twende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, linalofuata sasa hivi ni la Waziri Mkuu, naomba anisikilize. Mheshimiwa Lukuvi amwache Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere hata kama yeye anazungumza wewe unaongea na mimi huongei na Waziri Mkuu.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linamhusu.

NAIBU SPIKA: Unaongea na mimi siyo na yeye. Hata hivyo Mawaziri wake wako hapa wanakusikiliza usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana mikono mingi, masikio mengi na macho mengi, usiwe na wasiwasi.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo linaitwa kodi ya majengo. Kodi ya majengo haina tofauti na kodi ya kichwa, leo vijijini mama bibi kizee anaenda kuorodhesha nyumba yake ya vyumba viwili na sebule anaambiwa kwa sababu ana batil alipe kodi ya majengo, hii hapana. Hatuwezi kwenda kuwalipisha watu kodi ya

majengo watu wa vijjini, tunawa-*encourage* watu wasijenge majengo ya mabati, tunataka watu wabaki kwenye nyasi, haiwezekani. Hili naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukuwe na alitendee kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ripoti ya CAG tumeonyesha kwamba kuna trillioni 360 ambazo zinakaa pale kila mwaka kwa sababu mauzo hayapo. Ukichukua trillioni 360 ukazigawa kwa bajeti ya trillioni 32, ni miaka 11 ya bajeti ya Bunge hili, ziko pale! Naomba tuunde Tume...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ngoja tuweke takwimu vizuri, trillioni 360?

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Ndiyo, trillioni 360.

NAIBU SPIKA: Ukurasa gani huo ullosoma wa trillioni 360?

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, madeni yaliyo *pending* ya TRA ni trillioni 360...

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Getere kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jerry Slaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali ni kweli kwamba TRA ina mashauri ya kesi yaliyoko kwenye Mamlaka, Bodi na Mahakama mbalimbali yenye thamani ya shilingi trillioni 360. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Getere endelea na mchango wako.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana mtaalam, huyu ni mtaalam namjua, ni mtaalam mwenzangu huyu. Namshukuru sana. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndiyo kosa la watu kutochungulia mambo. Kuna bilioni 52.5 ambazo ziko kwa *DPP*. Sasa hizo fedha naomba tuunde tume ya kwenda kuchunguza trillioni 360 na bilioni 52.5. Hizo bilioni 52.5 ziko kwa *DPP* tuzichukue ziende kutengeneza madawati ya watoto, hizo fedha zipo wazi pale, kwa hiyo tuzichukue zikatengeneze madawati ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi niende pole pole. Bandari ya Bagamoyo. Tunaambiwa kwamba itakuwa bandari kubwa kuliko zote Afrika, sawa na vema; tunaambiwa kwamba meli kubwa zitatio nanga hapo kwenye hiyo bandari, sawa na vema; tunaambiwa kodi kubwa itakusanya, sawa na vema; tunaambiwa viwanda karibu 3,000 sijui na 100 vingine, sawa vema. Swali la msingi, nini Serikali yetu inapata kutokana na hiyo bandari? Nani atafuta maelezo ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwamba bandari hiyo ni mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza *TRA* ikishakuwa pale haikanyagi pale; pili ardhi yote hiyo ya bandari inachukuliwa, hatupati chochote; tatu maili 250 magharibi, maili 250 mashariki itakwenda kwao na jamani tukisema maili wale ambaao mnajwa hesabu ni kwamba, maili 250 ni kilomita 400, kilomita 400 inaenda. Nani atafanya maelezo hayo kwa wananchi, umma kwa Tanzania ujue kwamba faida ya bandari hiyo au maelezo hayo siyo halali. Naomba hiyo mikataba ya Bandari ya Bagamoyo iletwe Bungeni ili tuthibitishe kwamba haya wanayosema ni ya kweli au siyo ya kweli...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kengele imegonga.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kupata nafasi ya kufunga dimba kwa leo. Naomba nianze kwa kuwapa pole wananchi wote wa Mkoa wa Singida na hasa Waislam kwa kufiwa na Shehe wetu wa Mkoa na kesho tunakwenda kumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba njielekeze moja kwa moja kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, japo imegusa mambo mengi ya msingi, lakini nataka niende kwenye kipengele cha afya hasa katika suala la maboma ya zahanati. Wananchi wetu walihamasishwa sana kipindi cha nyuma kwamba wajenge zahanati kwenye vijiji na vituo vya afya kwenye kata, wakifika hatua ya lenta Serikali itamalizia. Wananchi wangu wa Mkalama walifanya hivyo na tuna maboma zaidi ya 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara zinazohusika, wangetekeleza ahadi hii ambayo waliwaahidi wananchi wetu, kwa sababu wananchi wetu sasa wamevunjika moyo na tukiwaambia mambo mengine ya maendeleo wanakuwa wazito, kwa sababu wanasema mltuambia tujenge, tumejenga na sasa maboma yetu yana zaidi ya miaka saba, mengine miaka mitano, nguvu zao wanazitazama na Serikali imeshindwa kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi majengo mengine wizara inakuja na ramani mpya, wanasema ramani hii ni nytingine, sasa lile jengo lenu ramani imekuwa ya kizamani. Suala la chumba cha sindano kuchomwa au kupokea dawa wala sidhani kama lina uhusiano sana na ramani. Naomba sana Serikali imalizie majengo haya ili wananchi wetu waendelee na tabia yao nzuri ya kuchangia maendeleo ya Serikali pale wanapoambiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwa haraka suala la watumishi. Tunaweka hizi zahanati, tunaweka majengo mapya, hospitali na nini, lakini watumishi hatujirri wakati nafasi zipo. Ningiombaa Wizara ya Utumishi zile nafasi ambazo ni *replacement* tunafahamu kwamba leo kuna watu

wanastaafu, leo kuna watumishi wametangulia mbele ya haki, watumishi hao tayari wana bajeti tayari kwenye Wizara, wana mishahara ipo, kwa nini *replacement* haifanyiki mara moja mpaka kusubiri uje uombe wakati zile nafasi zipo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe wafanye *recruitment* kwa sababu watu ambao wana sifa tunao wengi, wako mtaani katika wizara mbalimbali, wawe wanasubiri tu ikitokea mtu amefariki, mtu amestaafu, anajazwa moja kwa moja ili inapokuja kuombwa ajira mpya, ziwe ajira mpya kweli siyo zile za *replacement* ambazo tayari zilikuwa kwenye bajeti. Kwa sababu inakuwa shida sana kuajiri watu kwa sababu ya bajeti, sasa zile nafasi ambazo watu wamefariki kwa nini watu wasiajiriwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta zahanati ina *Nurse* mmoja halafu wananchi wanalamika zahanati inafungwa, *Nurse* huyo pia ana watoto, ana mume anatakiwa akamhudumie au mke, sasa akitaka kwenda nyumbani akifunga anaanza kulaumiwa, wakati pia ye ye ni binadamu ana mambo ya kijamii. Kwa hiyo ningeomba hizi *replacement* zifanyike haraka, kwa wakati, wala siyo za kusubiri kibali, kwa sababu ni nafasi ambayo ipo na Wizara ya Utumishi ipo, watu wafaniyiwe *recruitment*, wajazwe kwa wakati, inapofika kwa Rais tunaomba ajira ziwe mpya kwa maana ya mpya siyo zile za kujaza nafasi kama ambazo hizi zilizopo sasa hivi ni za kujaza nafasi. Kwa hiyo tuombe zingine mpya ili watu waajiriwe na kazi zipo kwa sababu tumejenga hospitali nyingi hazina watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa sababu naenda haraka sana, muda mwenyewe ndiyo wa mwisho, suala la hii miradi yetu ya kimkakati. Tumetengeneza miradi mingi lakini mradi mmojawapo ni wa mwendo kasi Dar es Salaam. Ni mradi mzuri wa kimkakati na hapa kwetu ni mradi ambao tulijua utatusaidia kuondoa suala la foleni Dar es Salaam, lakini leo hii ule mradi umekuwa ni kero, yaani kuingia kwenye mwendo kasi kama una ubavu huwezi, watu wanaanguka wanaabiwa wanafanya nini, niliingia mle juzi

nikaogopa wasije wakajua mimi ni Mbunge, wakaanza kuniambia sisi tunateseka na ninyi mpo. Naomba kampuni mbili zifanye kazi kwenye mradi ule, kama haiwezekani basi daladala zile zirudishwe za Posta - Kimara kwa sababu watu wanapata shida sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makof)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho kwa uchangiaji kwa siku ya leo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.15 Jioni Bunge lillahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 16 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*